# Nipashe

Jumatano Septemba 11, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580020
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Kauli za viongozi sheria mkononi zashutumiwa vikali

UKURASA 3


Wawili wapoteza maisha kwa vurugu Afrika Kusini
Ukurasa 19
DC Mtatiro asukuma ndani mafataki 12
Ukurasa 17
siasa
JUMATANO SEPTEMBA 11, 2019
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Ukurasa 14
Ndege kuzuiwa Afrika Kusini kulikoni?
ROBERT MUGABE, 1924-2019
• Kama Gaddafi, aliichanganya dunia kwa kupendwa, kuchukiwa kwa kiwewe
Na Anil Kija
MPIGANAJI Robert Mugabe hatimaye amejisalimisha na kuaga dunia wakati viungo vikiwa vimedhoofu kwa muda, kwa miezi kadhaa akawa anatibiwa katika hospitali jijini Singapore.
Ni hospitali aliyokuwa amechagua na kuizoea, iwe ni kutokana na masuala ya kitaaluma au urafiki binafsi, kwani alikuwa rafiki mkubwa wa Jamhuri ya Watu wa China, ambayo ina uhusiano wa kijadi na Singapore, ila hawana itikadi moja.
Wakati anatibiwa mara kadhaa zilitangazwa taarifa potofu za kifo chake, kuanzia alipoondolewa rasmi madarakani na jeshi mwezi Novemba 2017, taarifa za kifo zikaanza Machi 2018 na kuendelea tu.
Hulka ya kuwa mpiganaji ndiyo inayoweza kujumuisha maisha na kazi ya hayati Mugabe, kwa sababu kwa vipindi virefu vya maisha yake alikuwa katika mapambano.
Kuna wakati kulikuwa na kipindi kirefu cha amani bila mapambano ya wazi, na wengi walitazamia kuwa hali ingeendelea hivyo lakini ilikuwa ni taswira danganyifu, kwani masuala ya msingi ya mapambano yalikuwa hayajatatuliwa bado.
INAENDELEA UK.16
Ukurasa 20
Vyanzo mtandaoni vyaanika ujasusi wa Uholanzi, vinu vya nyuklia
Marehemu Robert Mugabe, Rais wa zamani wa Zimbabwe. PICHA: MTANDAO
Kagame, Museveni kuyaheshimu makubaliano ya nchini Angola? Ukurasa 18

UKURASA 13

# Vigingi Nape hadi msamaha kwa JPM

• **Asimulia** alivyopita kwa vigogo hadi kumwona Rais, picha zaonyesha alivyoingia, kutoka...*Uk. 2*



Rais John Magufuli akiagana na Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye baada ya mazungumzo yao, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Kundi la WhatsApp ladaiwa udanganyifu mitihani la saba

UK.2


## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**ASKOFU RUWA'ICHI AFANYIWA UPASUAJI**
ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadeus Ruwa'ichi, anapatiwa matibabu...

UKURASA WA 3
**LISSU KUKIMBILIA MAHAKAMA RUFANI**
SIKU moja baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutupilia mbali maombi ya mbunge wa zamani wa...

UKURASA WA 5
**TETEMEKO LA KATAVI LAJERUHI WATOTO 3**
TETEMEKO la ardhi lililotokea mkoani Katavi usiku wa kuamkia Jumatatu, limejeruhi watoto watatu baada ya...


## Faru tisa waletwa kutoka 'Sauzi'

UKURASA 4

**MICHEZO** KAGERE AANZA NA TUZO TFF, AJIBU ATOA NENO UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, akiangalia mmoja wa faru tisa walioletwa nchini katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, jana alfajiri wakitokea nchini Afrika Kusini. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**.

# Vigingi vya Nape hadi msamaha wa Rais

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amesema amemsamehe Mbunge wa Jimbo la Mtama mkoani Lindi, Nape Nnauye na kueleza jinsi mbunge huyo alivyohangaika kumtafuta ili kuomba msamaha huo.

Kauli ya Rais Magufuli aliitoa jana baada ya mazungumzo mafupi na mbunge huyo, Ikulu jijini Dar es Salaam. Akielezea njia alizopitia mbunge huyo kuomba msamaha huo, Rais Magufuli alisema Nape alikwenda kwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula, bosi wa zamani wa Usalama wa Taifa, Apson Mwang'onda na Mke wa Baba wa Taifa, Maria Nyerere.

"Nimeshamsamehe kwa dhati, Nape amekuwa hata akiandika 'message' (ujumbe) nyingi tu, ameshaandika message kuomba msamaha, saa nyingine anaandika saa nane za usiku, unamuona kabisa huyu mtu anaomba msahama," alisema na kuongeza:

"Leo kaniomba aje anione na saa zingine wasaidizi wangu wamekuwa wakipata hiyo habari, alienda kwa Mzee Mangula, amefika mpaka kwa Apson na Mama Nyerere, amehangaika kweli."

"Ni katika hiyo hiyo, sisi tumeumbwa kusamehe na leo mmemuona asubuhi amekuja hapa, nikaona siwezi kumzuia kumuona, ngoja niache shughuli zangu nimuone kwanza, nilikuwa na shughuli nyingi za vikao," alieleza.

"Kusamehe kunaumiza, lakini nasema kwa dhati kabisa nimemsamehe. Ameeleza yaliyokuwa yanamsibu, ameeleza baadhi ya watu aliokuwa wanamuhubiri, wengine wapo kwenye chama, lakini nimesema yote tunasamehe, huyu bado ni kijana mdogo ana 'future' (maisha baadaye), nikiendelea kumshikilia kwenye moyo wangu ni dhambi kubwa kwa Mungu, tumefundishwa tusamehe saba mara sabini," alisisitiza.

Rais Magufuli ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alimtaka Nape kwenda kufanyakazi zake vizuri ikiwamo kulea familia yake na kukitumikia Chama na wananchi wa jimbo lake.

Kwa upande wake Nape alimshukuru Rais Magufuli kwa kukubali kuonana naye na kumsamehe.

"Nilikuja kumuona kama baba yangu, lakini Mwenyekiti wa chama changu, rais wangu kwa sababu wote mnajua mambo yaliyopita yametokea mengi hapa katikati, nami kama mtoto wa CCM kama mwanaye, nilisema vizuri niongee na baba yangu," alisema Nape.

Baada ya mazungumzo yao, Nape alimshukuru Rais Magufuli kwa kumpa fursa ya kumuona na kumsamehe ikiwamo kumpa ushauri na kwamba aliyompa ni fursa na nafasi kubwa ya kumsikiliza.

INAENDELEA UK. 8

# Askofu Ruwa'ichi afanyiwa upasuaji

**Na Mary Geofrey**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadeus Ruwa'ichi, anapatiwa matibabu katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI).

Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, alisema katika taarifa yake jana kuwa Askofu huyo alipokewa juzi saa 5:00 usiku akitokea katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Moshi mkoani Kilimanjaro.

Alisema baada ya kupokewa, wataalamu wa MOI walimfanyia uchunguzi na vipimo na kubaini alihitaji upasuaji wa dharura.

"Jopo la madaktari bingwa pamoja na wauguzi wa MOI walimfanyia upasuaji mkubwa kwa muda wa saa tatu kuanzia saa 7:00 usiku hadi saa 10:00 alfajiri. Upasuaji huo ulifanyika kwa mafanikio makubwa," alisema Mvungi katika taarifa hiyo.

Alisema baada ya upasuaji hali ya Askofu Mkuu Ruwa'ichi inaendelea vyema na bado yuko kwenye chumba cha uangalizi maalum (ICU).

"Taasisi ya MOI inawatoa hofu Watanzania wote hususani waumini wa Kanisa Katoliki kwamba hali ya Mhashamu Askofu Ruwa'ichi inaendelea vizuri na tumwombee ili apone mapema na kurejea kwenye majukumu yake ya utumishi," alisema Mvungi.

Hadi sasa ni siku 26 tangu Askofu Mkuu Ruwa'ichi ashike wadhifa huo baada ya Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo kung'atuka madarakani Agosti 15, mwaka huu, baada ya Kiongozi Mkuu wa Kanisa hilo duniani, Papa Francisco, kuridhia ombi lake.

# Kundi la WhatsApp ladaiwa kutumiwa mitihani darasa 7

**Na Waandishi Wetu**

WATAHINIWA 947,221 wanatarajia kufanya mitihani ya darasa la saba leo na kesho, kundi la mtandao wa kijamii linalohusisha walimu na wadau wa elimu, limebainika wilayani Chemba mkoani Dodoma.

Kutokana na kubainika kwa kundi hilo, uongozi wa halmashauri huyo umekemea na kutaka kundi hilo livunjwe mara moja. Katika mitihani ya mwaka jana, lilijitokeza kundi kama hilo lililokuwa likitumiwa na walimu na waratibu kupeana majibu ya mitihani.

Barua ya Agosti 19, mwaka huu, iliyoandikwa na Josephat Ambikilile kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, iliwataka waratibu wa kata 26 zilizoko wilayani humo kuvunja makundi yote ya WhatsApp yaliyojihusisha na mawasiliano kwa walimu.

Katika barua hiyo, waratibu wameelezwa kuvunja makundi hayo yaliyojihusisha kutoa au kupokea taarifa zozote zinazohusiana na utendaji wa taaluma na utaalam zinazomgusa mwalimu wa Chemba katika utendaji wake wa kila siku hadi hapo watakapojulishwa vinginevyo.

"Ofisi imebaini kuwapo kwa makundi ya WhatsApp katika halmashauri yetu yanayotoa na kupokea taarifa mbalimbali za kielimu na kijamii kama vile walimu wakuu wanaovuliwa madaraka na walimu wakuu wapya, walimu wakuu walioko madarakani, maofisa elimu kata na walimu wakuu ngazi ya kata na wilaya na mengineyo yanayofanana na hayo," ilisema.

Barua hiyo iliwaeleza waratibu hao kuwa hatua kali za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi ya kiongozi wa kundi la WhatsApp na wanachama wa kundi husika.

Akitolea ufafanuzi wa barua hiyo jana mara baada ya kupigiwa simu na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Semistatus Mashimba, alikiri barua hiyo iliandikwa lakini si kwa lengo la kutolewa hadharani.

Alisema kwa sababu barua hiyo haikulengwa kutolewa hadharani, wanaendelea kumsaka aliyeivujisha kwenye mitandao ya kijamii ili achukuliwe hatua za kinidhamu.

**NECTA YAONYA**

Wakati hayo yakibainika, Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (Necta) limesisitiza kuwa vituo vilivyofanya udanganyifu mwaka jana katika mtihani huo vinaendelea na kifungo.

Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, alitangaza hayo jana jijini Dar es Salaam huku akisema watahiniwa katika vituo hivyo watafanyia mitihani yao katika vituo vilivyotangazwa mwaka huo na baraza.

"Vituo vilivyofanya udanganyifu katika mitihani ya mwaka jana vinaendelea na vifungo mpaka pale baraza litakapojiridhisha vipo salama kuendesha mitihani katika maeneo yao. Vituo hivi vilipokuwa vikirejea kufanya mitihani vilipewa vituo vingine vya wao kufanyia mtihani ambavyo tulivitangaza mwaka jana.

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

## Tundu Lissu kukimbilia Mahakama ya Rufani

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kutupilia mbali maombi ya mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, mwenyewe amezungumza na kusema mapambano bado yanaendelea.

Lissu alisema mlango mmoja ukifungwa mingine inafunguliwa.

Akizungumza juzi nchini Ubelgiji na chombo kimoja cha habari baada ya hukumu hiyo, alisema kauli ya mwisho ya mgogoro wa kisheria ni Mahakama ya Rufani Tanzania ambako ndiko wanakoelekea.

Juzi, Mahakama Kuu ya Dar es Salaam ilitupilia mbali maombi ya Lissu ya kibali cha kutaka kufungua kesi kupinga uamuzi wa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kumvua ubunge wa jimbo hilo.

Mahakama iliyoketi chini ya Jaji Sirilius Matupa, ilisema kwamba maombi hayo yangesikilizwa hadi mwisho na Lissu kushinda, Jimbo la Singida Mashariki lingekuwa na wabunge wawili kinyume cha Katiba.

Vilevile alisema maombi ya Lissu yamechelewa kufunguliwa mahakamani hapo na hayatekelezeki kwa sababu mleta maombi alitakiwa kufungua kesi ya kupinga uchaguzi badala yake ameleta maombi ya kutaka kupinga maamuzi ya Spika.

Akizungumza na chombo hicho Lissu alisema kwa maoni yake jaji amekosea aliposema alipaswa kufungua kesi ya uchaguzi.

"Kufungua kesi ya uchaguzi maana yake ni kwamba nina ugomvi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) au huyo aliyesemekana amechaguliwa au ameteuliwa kuwa mbunge," alisema.

Lissu alifafanua kuwa, kisheria hakuwa na ugomvi na Tume wala aliyechukua nafasi yake ya ubunge Singida Mashariki.

"Kisheria sina ugomvi nao kwa sababu Tume imeitisha uchaguzi kutokana na uamuzi wa Spika, huyu aliyechukua nafasi yangu aligombea kwa sababu Tume ilitangaza uchaguzi, Tume haina mamlaka ya kumkatalia Spika, akisema kiti kiko wazi.

"Kwa hiyo nisingeweza kufungua kesi ya uchaguzi kwa sababu sina ugomvi na Tume ya Uchaguzi wala huyo aliyechukua nafasi yangu. Ugomvi wangu ni yule aliyefanya uamuzi wa kunifuta ubunge, huo ndio ugomvi wangu kisheria.

Kuhusu hoja ya pili ya Jaji kuwa angeendelea na shauri jimbo lingekuwa na wabunge wawili kinyume cha Katiba, Lissu alisema, hoja hiyo haina maana wala mantiki yoyote.



Watuhumiwa askari sita wakiwamo, polisi watano na mmoja wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wakiwa chini ya ulinzi walipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, wizi wa mafuta ya ndege lita 2180 na utakatishaji wa zaidi ya Sh. milioni nne. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kauli za viongozi kuhusu kuua majambazi zashutumiwa vikali

**Na Romana Mallya**

WAKATI kauli za viongozi mbalimbali za kuwataka wananchi kuchukua sheria mkononi kuua na kujeruhi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimekosoa matamko hayo na kusema jambo hilo ni kinyume cha utawala wa sheria.

Hivi karibuni, kumekuwa na kauli mbalimbali kutoka kwa baadhi ya watendaji wa serikali wakishinikiza wananchi kuvunja sheria za nchi na kuua wenzao.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alipoulizwa kuhusiana na kauli hizo jana, alisema chombo chenye mamlaka ya kutambua mtu ni kibaka, jambazi ni mahakama pekee.

"Ndiyo maana akikamatwa na polisi tunamwita mtuhumiwa. Hatumwiti jambazi au kibaka. Nchi yenye utawala wa sheria inatambua mahakama ndiyo yenye mamlaka ya kumtambua jambazi.

"Kauli hizi ni za kukemewa kwa sababu zikiachiwa zitasababisha watu kuchukua hatua za kisheria mikononi," alisema.

Jana, Kamanda wa Polisi wa mkoa wa kipolisi Kinondoni, Musa Taibu, jana aliwataka wananchi wanaomiliki silaha wanapokutana na majambazi, wawaue.

"Ndugu zangu wananchi pale inapotokea kwamba kuna jambazi na wewe una bunduki, tumia akili za kuona ni namna gani unaweza kukabiliana na jambazi huyo. Mtandike risasi hakuna atakayekulaumu.

"Na bunduki yake ichukue tuikute, tukikuta ni mwili hakuna tatizo lolote. Huyo ni jambazi na alichokitaka kufanyiwa ndicho hicho alichostahili kupewa," alikaririwa kamanda huyo akisema.

Hivi Karibuni, Waziri Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangallah, alisema angekutana na mmoja wa majangili waliokamatwa Septemba 3, angempiga risasi na kumwua.

Dk. Kigwangallah alitoa kauli hiyo baada ya vipande 339 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.4 kukamatwa maeneo ya Chamazi ambavyo idadi yake ni sawa na tembo 117.

Kauli zenye viashiria vya uvunjifu wa sheria ni pamoja na iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliagiza: "Anayeingia nyumbani kwako kwa nguvu, amechagua kifo, hivyo mhusika hana budi kumwua."

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, alisema anajua kuna watu wanaishi kwa kutegemea wizi huku wakiamini kuwa wakipelekwa mahakamani wanapewa dhamana.

"Sasa nawaambia siku zao zinahesabika, watapigwa na kupewa ulemavu kwa kuvunjwa miguu," alisema mkuu huyo wa wilaya.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
10/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano tarehe 11/9/2019** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEASE CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA) LTD itasafirisha Mzigo kutoka INYONGA kuelekea DAR ES SALAAM** kupitia **TABORA-DODOMA.** Magari yenye namba za usajili

   **T 550 BES / 474 BCJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 16**
   **Upana - mita 2.8**
   **Kimo - mita 4.9**

3. Njia itakayotumika: **SUMBAWANGA** hadi **KABANGA kupitia MPANDA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115412302



**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na **muda ni kuanzia saa nne asubuhi.** Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD.**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Mangaza K Said | Nyumba | Kimara-Mtaa wa Temboni | 25/9/2019 | Champion A/Mart |
| Shina Rehege | Home Chattels | Mkumbusho yard | 13/9/2019 | RAISSA CO. LTD |
| Dickson Oscar Kabuguzi | Nyumba | Charambe-Rangi Tatu | 27/9/2019 | Champion A/Mart |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki na Eviction zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;- TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**RAISSA Co. Ltd: 0652 113 262;B MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).**
**CHAMPION Auctioneer: 0654200448/0756761328.**

215414002

# Waziri Mwakyembe ataka Watanzania kujifunza ukalimani

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amewata Watanzania kujifunza taaluma ya ukalimani ili waweze kujiwekea wigo mpana wa kupata ajira ndani na nje ya nchi.

Alisema hapa nchini kuna idadi ndogo ya wakalimani kulinganisha na mahitaji yaliyopo, na hivyo kusababisha changamoto kwa baadhi ya taasisi au ofisi zinazowahitaji.

Waziri Mwakyembe alitoa rai hiyo alipokuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya 15 ya wanafunzi wa darasa la saba wa shule ya Bethel Mission jijini Dar es Salaam na kueleza licha ya ukalimani kuwa na soko zuri la ajira duniani, bado kuna uhaba wa wataalamu wa fani hiyo nchini.

Alisema idadi ya wakalimani nchini haizidi 20 hali inayoashiria kuwapo kwa kiwango kidogo cha wataalamu hao kuliko uhalisia wa mahitaji.

"Ninawaasa wazazi kuendelea kuwalea watoto wao katika maadili mema kama ambavyo shule hii ya Bethel Mission imekuwa ikifanya ili kujenga taifa la watu waadilifu," alisema Waziri Mwakyembe.

Pia, Dk. Mwakyembe aliimwagia sifa shule hiyo kwa kuwa mstari wa mbele wa kuwalea na kuwajenga kimaadili watoto hasa katika kipindi hiki cha utawandawazi ambao maadii yameharibika.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Emmanuel Mshana, alisema mbali na shule hiyo kujivunia kwa matokeo mazuri kwa wanafunzi katika mitihani ya kitaifa, pia wamekuwa wakiwajenga nidhamu bora ili kuwa na kizazi bora.

Alisema shule hiyo imekuwa na ushirikiano wa karibu na wazazi ili kuhakikisha wanaosoma katika shule hizo wanahitimu wakiwa na ufaulu mzuri ili kuwafanya waweze kupata nafasi za kuendelea na ngazi za juu katika masomo yao.

"Mikakati ya baadaye ya shule hii ni kujenga sekondari ili kuwawezesha kuwaendeleza kimasomo wanafunzi wanaoanza nao kuanzia ngazi ya shule za msingi na awali," alisema Mshana.



Meya wa Manispaa ya Ilala, Omari Kumbilamoto (wa tatu kushoto), akishiriki matembezi ya amani ya kukumbuka kifo cha Imam Hussein na mjukuu wa Mtume Muhammad (S.A.W.W), katika Maadhimisho ya Siku ya Ashura, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Faru tisa warejeshwa nchini kutoka 'Sauzi'

**Na Godfrey Mushi,** HAI

FARU tisa kati ya 10 wenye vinasaba vya faru wanaopatikana Tanzania, wamerejea nchini wakitokea Afrika Kusini.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, alisema wakati faru hao wakirejeshwa jana katika maeneo yao ya asili, mmoja kati yao alikufa katika purukushani za kusafiri na hakufika.

Kanyasu alikuwa akizungumza jana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), baada ya faru hao kuwasili kwa ndege ya mizigo aina ya Boeing 747-400 (F), mali ya Kampuni ya Magna ya Uingereza.

"Tunashuhudia kupokelewa kwa faru tisa, faru hawa walikuwa 10, lakini kwa taarifa tulizokuwa nazo mmoja katika purukushani za kusafiri hakufika. Tumetaarifiwa kwamba alikufa, lakini tisa tunakiri kuwapokea wako hai," alisema na kuongeza:

"Hii ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kupokea idadi kubwa sana ya faru kwa mara moja ambao ni wenye vinasaba vya nchi yetu."

Wakati wa halfa fupi ya mapokezi na makabidhiano ya faru hao kati ya serikali na Kampuni ya Grumeti Fund iliyotoa faru hao, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, aliapa akisema:

"Tutawalinda faru hawa na tutalinda maliasili zetu kufa na kupona, na yeyote ana mawazo ya kujaribu kuja kufanya ujanja ujanja tutamdaka. Sasa hivi hakuna namna tutampata, tutawalinda usiku na mchana na kwa kila mbinu."

Pia Prof. Mkenda alitangaza mpango mpya wa serikali wa kukabiliana na wanyamapori hatari na waharibifu ambao wamekuwa wakivamia maeneo mbalimbali nchini.

"Nimemwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Wanyamapori kuanza rasmi operesheni maalum ya kupambana na wanyama hatari na waharibifu wanaovamia maeneo mbalimbali na kuleta hatari," alisema Katibu Mkuu huyo.

Makabidhiano ya wanyama hao yamefanyika katika karakana ya ndege uwanjani hapo, kati ya Naibu Waziri Kanyasu na Mkurugenzi wa Kampuni ya Grumeti Fund, Stephen Cunliffe.

Mapema akitoa taarifa kuhusu mpango wa kuwarejesha faru hao katika hifadhi za Taifa, Mkurugenzi wa Wanyamapori nchini, Dk. Maurus Msuha, alisema tukio hilo ni utekelezaji wa mpango wa kuhifadhi faru wa mwaka 2019/ 2023.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori (TAWA), Meja Jenerali mstaafu, Khamisi Semfuko, aliwasilisha salamu za Rais John Magufuli akisema, mkuu wa nchi anaishukuru sana Kampuni ya Grumet Fund kwa kuweza kurejesha hali ya hifadhi ziwe katika kiwango kikubwa cha faru.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira na wa Arusha, Mrisho Gambo, kila mmoja kwa nyakati tofauti walipongeza jitihada za serikali katika uhifadhi.

# Waziri atahadharisha kuhusu mabomu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, amewataka wananchi wa Kagera na mikoa mingine nchini kuendelea kuchukua tahadhari wanapoona vitu vyenye asili ya chuma ili wasikumbwe na milipuko ya mabomu.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana bungeni mjini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nungwi (CUF), Yussuf Haji Khamis, ambaye alisema kumekuwa na matukio ya watoto kuokota mabomu wakidhani ni vyuma chakavu na kisha kuwalipukia na kusababisha madhara makubwa ikiwamo vifo.

"Hivi karibuni watoto watano wamepoteza maisha na zaidi ya watoto 40 kujeruhiwa katika Shule ya Msingi Kihanga iliyoko mkoani Kagera. Je, serikali ina mpango gani wa kudhibiti na kukomesha tatizo hili?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Mwinyi alisema maeneo mengi duniani yanakabiliwa na changamoto ya kutapakaa kwa silaha ndogo ndogo yakiwamo mabomu ya kutupwa kwa mkono.

"Pamoja na Tanzania kuwa nchi yenye amani, baadhi ya nchi zinazotuzunguka zimejikuta zikitumbukia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe,"alisema.

Waziri huyo alisema hali hiyo imesababisha baadhi ya wakimbizi kukimbia na silaha yakiwamo mabomu ya kutupwa kwa mkono na kuyateketeza baada ya kujiona wako salama au kuwauzia wahalifu jambo ambalo limechangia kuwapo kwa mabomu hayo katika badhi ya mikoa, Kagera ikiwamo.

"Baada ya vita vya Kagera, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) lilitoa elimu kwa wananchi kutokuokota vitu vinavyong'ara, vifaa vya chuma na pindi wanapoona vitu hivyo watoe taarifa vituo vya polisi au kambi ya jeshi iliyo karibu," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kwa maeneo yaliyotiliwa shaka, wananchi walipewa tahadhari ya kutolima, kutopita au kulisha mifugo.

" JWTZ lilipeleka wahandisi wa medani kukagua maeneo hayo na kujiridhisha kama yako salama kwa wananchi kuendelea na shughuli zao za kawaida, hivyo inashauriwa wananchi katika mkoa huo na mingine kuendelea kuchukua tahadhari wanapoona vitu vyenye asili ya chuma," alisisitiza.

HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara 10 wa madini kizimbani

**Na Nedbart Msokwa,**

MBEYA

WATU 10 wanaodaiwa ni wafanyabiashara wa madini, wamefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya ambako watano wamesomewa mashtaka tofauti ya uhujumu uchumi.

Baadhi ya makosa hayo ni utoroshaji wa madini na wengine watano wakiwekwa chini ya uangalizi wa mahakama kwa kipindi cha mwaka mmoja, ili wawe na tabia njema.

Katika kesi ya kwanza ambayo ilisomwa juzi mbele ya Hakimu Mkazi, Andrew Scoout, inawahusu watuhumiwa watatu Mike Konga, Sauli Solomon na Emmanuel Kessy ambao walisomewa mashtaka matatu.

Wakili wa Serikali, Basilius Namkambe, alidai shtaka la kwanza ambalo linawahusu watuhumiwa wote watatu ni kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alidai kati ya Juni Mosi na Juni 30, mwaka huu, walijipatia fedha za Zambia Kwacha 290,000 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa raia mmoja wa Zambia kwa kumuuzia dhahabu.

Wakili Namkambe alidai kosa la pili ni utakatishaji wa kwacha 290,000 ambazo walizipata kwa udanganyifu kutoka kwa raia wa Zambia.

Watuhumiwa hawakutakiwa kujibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na Wakili Namkambe alidai upelelezi haujakamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Andrew Scoult aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 23.

Katika kesi ya pili, Mike Konga na Sauli Solomoni walisomewa mashtaka mawili ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha mbele ya Hakimu Denis Luwongo.

Wakili wa Serikali, Basilius Namkambe alidai kati ya Juni Mosi na Juni 30, mwaka huu walijipatia dola za Marekani 115,000 kwa njia ya udanganyifu baada ya kumuuzia Henry Clever, raia wa Ujerumani dhahabu kilo moja.

Wakili Namkambe alidai kosa la pili ni kutakatisha dola za Marekani 115,000

INAENDELEA UK. 26



Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, akizungumza katika kongamano la uwezeshaji kibiashara lililoandaliwa na benki hiyo, kwa ajili ya makandarasi na wadau mbalimbali wanaohusika na utekelezaji wa ujenzi wa miradi mikubwa ya maendeleo nchini, lililofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Tetemeko la Katavi lajeruhi watoto watatu

**Na Mary Geofrey**

TETEMEKO la ardhi lililotokea mkoani Katavi usiku wa kuamkia Jumatatu, limejeruhi watoto watatu baada ya kuangukiwa na ukuta wakiwa wamelala ndani.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alilieleza Nipashe jana kuwa, watoto wawili Cecilia Magashi (7) na Lucia Magashi (6) walijeruhiwa maeneo ya usoni.

Alisema pia nyumba kadhaa zimepata madhara, na wanaendelea kuzihakiki ili kufahamu idadi kamili kupitia kwa watendaji wa kata na maofisa tarafa.

Baba mzazi wa watoto hao wawili Magashi Enga (41) anayeishi Kijiji cha Gilabeta Kata ya Itenka, alilieleza Nipashe jana kuwa waliangukiwa na ufa.

"Nikiwa nimelala lilitokea tetemeko mke wangu akataka kutoka nje nikamzuia atulie, lakini nikakumbuka nyumba yangu nyingine ina ufa ambayo watoto walikuwa wamelala, nikatoka kwenda kuangalia nikakuta mke wangu mwingine akiwa analia, huku akijitahidi kuwaokoa watoto wetu," Enga alisema.

Alisema alilazimika kuvunja mlango na kuingia ndani ambako alianza kuondoa tofali zilizokuwa zimewalalia watoto hadi kusababisha kitanda kuvunjika.

"Tulifanikiwa kuwaokoa, lakini walikuwa wameumia maeneo ya usoni na mmoja mguu na niliwapeleka zahanati ambako walipatiwa matibabu na juzi walirejea nyumbani," Engo alisema.

Baba huyo mwenye watoto wanane na wake wawili, alisema watoto hao jana waliondolewa bandeji walizokuwa wamefungwa usoni na hali zao zinaendelea vizuri.

Juzi Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST), ilitaja madhara yaliyotokana na tetemeko hilo ni mtoto mmoja kujeruhiwa na nyumba kadhaa kuharibiwa.

Kwa mujibu wa Kaimu Meneja wa Utafiti na Uchumi wa Jiolojia, Gabriel Mbogoni, walipokea taarifa baadhi ya nyumba zilipata nyufa katika Kata ya Sibwesa na nyumba moja katika kata ya Mashimbo kijiji cha Isenga imebomoka na kujeruhi mtoto.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera wanafunzi wa darasa la saba

**KILA** la heri watoto wanaohitimu darasa la saba ambao leo mnaanza mitihani yenu. Ndivyo tunavyoweza kuwapongeza kwa kufanikisha na kukamilisha safari ya elimu ya shule ya msingi.

Wanafunzi wa shule za msingi wanaoanza mitihani leo ambayo itakamilika mwisho wa wiki hii wanapitia changamoto nyingi, ndiyo maana si wakati wa kuwakumbusha mlivyoteseka wala mlivyohangaika hadi kufikia hatua hiyo, bali ni wasaa mwingine wa kuwafariji na kuwashauri kufanya kile taifa linachowategemea.

Serikali inawezekana mabilioni ya fedha kwa ajili ya kufanikisha elimu ya msingi kwa hiyo si jambo jema wazazi na walezi kuwahimiza mabinti na wavulana kuandika majibu 'feki' ili kujaza vitabu vya mitihani.

Kwa mfano kuchora 'zombi' (misukule) kutukana matusi ya nguoni na kuchora michoro isiyoeleweka, huwasaidii watoto wala taifa.

Fedha zinazotolewa na serikali kila mwezi ili kusomesha watoto na nyingine wazazi wanazowekeza kwenye chakula, mavazi, madaftari ,vitabu na nauli ni muhimu zikaleta matokeo.

Ndiyo maana tunategemea walezi na wazazi wasiwahimize mabinti kuandika majibu ya uongo ili wasifaulu kwenda sekondari, kisa wanataka warudi nyumbani wakaolewe.

Aidha, wapo wazazi wanaowatisha watoto wao kuwa ukifaulu shauri yako, mimi sina hela za kukusomesha zaidi, faulu utajua mwenyewe.

Kwa wasichana wapo wanaokataliwa kusoma kwa kuwa wazazi au walezi wanawapendelea zaidi vijana wanaume kuliko mabinti nao na wanabaniwa kuwa wasijitahadi kwa kuwa shule kwao, darasa la saba ndiyo kikomo.

Tunawashauri wazazi wa Tanzania kubadilika ni wakati wa kuwaeleza watoto wetu haja ya kusoma. Tunatakiwa kuwafahamisha kuwa ni lazima kusoma kwani kila jambo katika dunia ya sasa ni lazima usome na uwe na utaalamu.

Wazazi wawahimize watoto kusoma na kufuatilia masuala ya taaluma si kuwakatisha tamaa na kuwarudisha nyuma kimasomo.

Kumwambia binti aache masomo ili akaolewe ni kama kumtia kitanzi. Kwanza ni uvunjaji wa sheria , lakini ni kumwingiza kwenye hatari za kupata matatizo ya uzazi ambayo wakati mwingine ni kifo.

Umri mdogo unaweza kuchangia vifo vya mabinti wakati wa kujifungua. Aidha, hata malezi ya mtoto anayelelewa na mama mwenye umri mdogo yanaweza yasiwe na manufaa kwani ni sawa na mtoto kumlea mtoto mwenzake.

Wazazi na walezi wafahamu kuwa maelezo kuwa elimu ni ufunguo wa maisha ni ukweli bila kipingamizi. Kwa elimu kijana anayopata ataweza kujiajiri, kumudu maisha yake na pia kuchangia uchumi wa familia na taifa.

Kwa hiyo huu uwe mwanzo wa wazazi na walezi kuwahimiza watoto wetu kusoma na kufanya vyema katika mitihani yao badala ya kuwahamasisha kutoa majawabu yasiyofaa kwenye mitihani.

Ikumbukwe utajiri pekee mzazi anaoweza kumpa na kumwachia mwanae ni elimu ambayo itamtengenezea taaluma na huo ndiyo ufunguo kwenye maisha yake.

Elimu ndiyo zawadi pekee ambayo hakuna wa kumnyang'anya. Ndiyo ambayo itainyanyua familia maskini , tena ndiyo barabara ya kuwatoa katika ujinga, umaskini na maradhi.

Kwa hiyo mtihani wa darasa la saba unaofanyika leo uwe mwanzo wa kuwahamasisha na kuwaandaa watoto wetu wa kike na kiume kusoma zaidi na kupenda shule zaidi.


Wanapomaliza mitihani hii tuwahimize kusoma, kujifunza zaidi na kujiandaa kuwa wabunifu, wataalamu na mabingwa kwenye Nyanja mbalimbali.

Ndiyo wakati wa kuwaeleza kuwa bila elimu hakuna maisha bora na ukikosea kwenye kujifunza, kujipanga na kujiendeleza kielimu unaweza usiwe na maisha bora.

Tunawatakia kila la kheri wanafunzi wote wanaomaliza darasa la saba leo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Ma-RC, DC mikoa ya pamba, chukueni somo la Mtaka

**NIMEVUTIKA** kuzungumzia habari iliyoandikwa na gazeti hili ukurasa wa 26 jana Septemba 10, iliyokuwa na kichwa cha habari kilichosomeka "Simiyu yauza pamba ya bil. 65/-"

Habari hiyo ilikuwa inarejea taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, baada ya kuwa amefanya ziara mkoani mwake ya kukagua hali ya maendeleo ya ununuzi wa pamba.

Kwa mujibu wa taarifa yake, mkoa huo ambao ni moja ya mikoa inayoongoza kwa kilimo cha zao hilo nchini, tayari umeshauza kilo 54,257,314.00 za pamba zenye thamani ya Sh. bilioni 65,108,775,600.00.

Aidha, taarifa inaendelea kubainisha kwamba pamba iliyokusanywa kwenye maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS), ni kilo milioni 132 yenye thamani ya Sh. bilioni 159.3.

Na kati ya kilo hizo zilizokusanywa kwenye maghala ya AMCOS, kilo milioni 83 zenye thamani ya Sh. bilioni 100, tayari zimeshasafirishwa kwenda kwenye viwanda vya kusindika pamba.

Vilevile taarifa hiyo ikafafanua kwamba kati ya kilo hizo milioni 83 zilizosafirishwa, kilo milioni 54 zenye thamani ya Sh. bilioni 65, bado hazijalipiwa kwa maana kwamba, wakulima hawajalipwa fedha zao.

Muungwana anasema amevutiwa na taarifa hiyo ya Mtaka kwa sababu ni miongoni mwa wadau ambao wamepaza sauti kwa muda sasa, kuhusiana na kadhia zinazoambatana na ununuzi wa pamba msimu huu.

Kadhia ya kusuasua kwa ununuzi wa zao hilo tangu msimu wa ununuzi uzinduliwe mwezi Mei, ambayo iliambatana na kitu kama 'kamgomo' kutoka kwa wanunuzi dhidi ya bei elekezi ya Sh. 1200 iliyowekwa na serikali.

Ni msimamo imara wa serikali ndio kimsingi umesaidia wakulima wanunuliwe kwa bei hiyo, kwani kama isingeonyesha msimamo thabiti kulikuwa na uwezekano kwa kilo ya pamba, kununuliwa hata kwa Sh. 500 msimu huu.

Aidha, kadhia hii iliambatana pia na ahadi ya serikali ya kununua pamba yote ya wakulima kufikia mwishoni mwa mwezi Julai, ahadi ambayo ilishindikana kutokana na kampuni za ununuzi kutokwenda na kasi iliyokuwa inatakiwa na serikali.

Taarifa hiyo rasmi ya Mtaka walau imempa mwanga Muungwana juu ya hali ilivyo katika suala zima la ununuzi wa pamba hadi sasa.

Anasema imempa mwanga hususani katika maeneo matatu kimsingi. Kwanza ni kuwa bado takribani nusu ya wakulima ambao wameuza pamba yao hadi sasa hawajalipwa fedha zao.

Hilo linathibitishwa na taarifa hiyo kwamba kati ya kilo milioni 83 zenye thamani ya Sh. bilioni 100, kilo milioni 54 zenye thamani ya Sh. bilioni 65 hazijalipwa hadi sasa.

La pili ambalo limempa mwanga Muungwana ni kwamba bado kuna pamba ambayo haijasafirishwa kutoka kwenye maghala ya AMCOS, kwenda viwandani.

Na la tatu ambalo Muungwana amelibaini kutoka kwenye taarifa ya Mtaka ni kwamba maelekezo ya serikali ya kuhakikisha wanunuzi wawe wameshainunua pamba yote kufikia sasa, hayajatekelezwa kikamilifu.

Ikumbukwe kwamba hapa tunazungumzia pamba ambayo tayari iko AMCOS, wakati kuna wakulima ambao bado hawapeleka pamba yao kuiuza kwenye vyama vya ushirika vya msingi, wakitaka wakiuza walipwe fedha zao palepale.

Kwa hali hiyo kuna ushauri ambao Muungwana anautoa katika kadhia hii ikizingatiwa kwamba huu ni mwezi Septemba.

Mwezi ambao kimsingi, wakulima wa zao hilo wanapaswa kuwa wanamalizia kuandaa mashamba yao, tayari kwa kilimo cha msimu ujao.

Muungwana anashauri wakuu wa mikoa katika maeneo yanayolima zao hilo kuweka hadharani taarifa ya ununuzi unavyoendelea hadi sasa.

Lakini kubwa anawasisitiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kusimamia shughuli nzima ya ununuzi, usafirishwaji na kubwa zaidi wahakikishe wakulima wanalipwa fedha zao.

Muungwana anasema hili ni la muhimu kwa sababu mbali na mengine, wakulima wanazihitaji fedha hizi ili ziwasaidie msimu ujao wa kilimo.

# Afungwa miaka 30 jela kumuua mpenzi kisa ugomvi wa malipo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kilanjelanje, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, Mwanyika Thobias (20), amehukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya kuua bila kukusudia, kutokana na kushindwa kulipia huduma ya penzi alilokuwa amepewa.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama hiyo, Paul Ngwembe, baada ya mshtakiwa kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia Shamshi Selemani Said (15), mkazi wa kijiji na kata hiyo.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea, hivyo kupitia Wakili aliyekuwa anamtetea Issa Chitula aliiomba Mahakama kuangalia adhabu itakayofaa kumpatia mteja wake, ikizingatiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza ambapo alifanya kosa hilo kutokana na kutingwa na 'shetani wa ujana'.

Mwanasheria wa Serikali, Yahaya Gumbo, aliomba mshtakiwa apewe adhabu kali ili liwe fundisho kwake na wengine wenye tabia ya kupenda kukopa penzi kutoka kwa kinadada wanaowatekelezea shida zao kwa kutotekeleza makubaliano yao, badala yake huwageuka na kuwapa kipigo kinachosababisha kifo.

Jaji Ngwembe akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 34/2018 kupitia kifungu cha (195) kanuni ya adhabu sura 16/2002, alisema anayakubali maombi kutoka pande zote mbili, lakini sheria imembana mikono, hivyo kumhukumu Mwanyika kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

Awali ilidaiwa na Gumbo kuwa Oktoba 21, 2017 katika Kata ya Kilanjelanje, Mwanyika alimuua bila ya kukusudia Shamshi, baada ya kushindwana malipo baada ya kutekelezewa kupewa penzi.

Gumbo aliiambia Mahakama kuwa Shamshi alitaka alipwe ujira wake wa Sh. 10,000, lakini mshtakiwa alimpatia Sh. 5,000, hivyo ukizuka ugomvi na kusababisha kifo cha msichana hiyo.



Meneja mradi wa kampuni ya Shahi Engineering, Agrej Singh, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kwa kosa la kushawishi na kutoa rushwa ya Sh. milioni 80, kwa Ofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yajipa miezi miwili utumiaji zebaki

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limepitisha azimio la kuridhia Mkataba wa Minamata wa mwaka 2013 kuhusu zebaki, huku serikali ikieleza kuwa imeshaanza maandalizi ya mpango mkakati wa kuondokana na matumizi ya kemikali hiyo na ndani ya mwezi ujao utakuwa umekamilika.

Akiwasilisha hoja ya kuomba kungwa mkono azimio hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene, alisema zebaki ni hatari kwa afya ya binadamu, viumbe wengine na mazingira.

"Wabunge wote wanaunga mkono azimio hili, hii inaonesha kwamba sote tumeshakubaliana kuwa zebaki ni kitu kibaya chenye madhara kwa binadamu, wanyama, mimea na mazingira.

"Lipo pia kundi la wachimbaji wadogo ambao wanaathirika moja kwa moja kwa kuishika zebaki, ambalo linahitaji kulindwa na serikali," alisema.

Simbachawene alisema kusudio la mkataba huo wa Minamata ni kuhakikisha kufikia mwaka 2030, kusiwe na matumizi ya zebaki na serikali kutoingia mkataba huo kunaweza kuikosesha nafasi na fursa za kushirikiana na mataifa mengine katika mikakati hiyo ya kimataifa ya kukabiliana na matumizi ya zebaki.

Alisema tayari wizara yake imeshaanza maandalizi ya mpango mkakati wa kuondokana na matumizi ya zebaki na ndani ya mwezi ujao utakuwa umekamilika.

Alisema zebaki ni miongoni mwa kemikali hatari zinazohatarisha zaidi afya ya jamii duniani kutokana na kudumu katika mazingira kwa muda mrefu, kusafiri masafa marefu kwa njia ya hewa, maji (mito, maziwa na bahari) na udongo, hivyo kuathiri afya ya binadamu na mazingira.

Alibainisha kuwa hadi sasa, tayari nchi 112 zimeridhia mkataba huo wa Minamata ulioanza kutekelezwa rasmi mwaka 2017.

Alisema hatua hiyo pia imezingatia Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 inayohimiza kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Akichangia hoja hiyo bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Semesi Sware (Chadema), alisema waathirika wakubwa wa zebaki nchini ni wachimbaji wadogo wa dhahabu ambao kwa asilimia 90 wanapatikana Kanda ya Ziwa.

Alisema kuna haja serikali kuchukua hatua kudhibiti matumizi ya zebaki nchini ili kuokoa maisha ya wananchi wake hususan wachimbaji hao ambao huishika moja kwa moja kemikali hiyo wakati wa kuchenjua kienyeji dhahabu.

# Kigoma kunufaika ujenzi wa madaraja

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa Halmashauri ya Kigoma, wanatarajia kunufaika na ujenzi wa madaraja ya mawe unaofadhiliwa na Serikali ya Ubelgiji chini ya mradi wa kilimo endelevu katika Mkoa wa Kigoma (Sakirp – Enabel) na kusimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura).

Akizungumza jana na waandishi wa habari wakati wa ukaguzi wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kigoma, Pendo Mangali, alisema mradi huo uliibuliwa na wananchi baada ya kueleza changamoto wanayokutana nayo katika kusafirisha mazao yao kutoka shambani hadi nyumbani na kwenye masoko.

Alisema kiongozi huyo amebainisha kuwa mradi huo wa ujenzi wa madaraja ya mawe unalenga kutatua kero ya usafiri na usafirishaji wa mazao na kwamba wananchi walihamasishwa na wakakubali kujitokeza katika kusomba mawe na kushiriki kujenga madaraja hayo.

"Nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wa Halmashauri ya Kigoma kwa kuwa wanafanya kazi sana, baada ya kugundua kuwa wanashindwa kusafirisha mazao yao kutoka shambani hadi sokoni kwa pamoja tuliamua kuanza ujenzi wa madaraja ya mawe," alisema.

Alibainisha kuwa baada ya kukamilika kwa madaraja hayo kazi itakayokuwa imebaki ni kufungua barabara za kuunganisha mashamba na hatimaye kuwezesha wananchi kufikisha mazao yao sokoni kwa urahisi na kukuza kipato chao.

Kwa upande wake, Meneja wa Tarura wilayani humo, Pharles Ngeleja, alisema ujenzi wa madaraja kwa teknolojia ya kutumia mawe ni wa gharama nafuu na kwamba unawashirikisha wananchi moja kwa moja kwa kukusanya vifaa vinavyopatikana katika mazingira yao.

Alisema wafadhili wanatoa vifaa vya viwandani visivyopatikana kwenye mazingira mfano saruji huku Tarura wakisimamia shughuli za ujenzi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wanaoshiriki katika ujenzi wa madaraja hayo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyabigufa, Johnphace Tunzwe, alisema kuwa changamoto ya usafiri ni kubwa hasa kipindi cha masika na tayari wameamua kujitolea kwa kukusanya mawe ili kujenga madaraja.

Naye, Meneja mshauri wa mradi huo chini ya Serikali ya Ubelgiji, Steven Hollevoet, alisema teknolojia ya ujenzi wa madaraja ya mawe ni ya muda mrefu hasa katika nchi za Ulaya na Asia na sasa wameileta Tanzania ili kuwafundisha wananchi kujenga madaraja kwa gharama nafuu kwa sababu vifaa vinavyotakiwa kama mawe na mchanga vinapatikana kwa urahisi.

Hadi sasa madaraja sita yamekamilika na tisa yapo katika hatua mbalimbali huku lengo likiwa ni kukamilisha 15 ifikapo mwezi Desemba, 2019.

# Tanzania sasa kuwa kinara hifadhi Afrika

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

WAZIRI wa Maliasili, Dk. Hamis Kigwangalla, amesema kwa Bunge kuridhia maazimio matatu ya kubadilisha hadhi sehemu ya mapori ya akiba kuwa hifadhi za taifa, Tanzania sasa itakuwa na hifadhi 24 na kuwa kinara barani Afrika kwa idadi ya hifadhi.

Akihitimisha hoja ya maazimio ya kubadili hadhi ya mapori ya akiba Kigosi na Ugalla kuwa hifadhi za taifa, Dk. Kigwangalla alisema kuridhiwa kwa maazimio hayo ni muhimu kwa sekta ya utalii na uhifadhi.

Kwa kupitishwa kwa maazimio hayo na Bunge jana mchana, kunaongeza hifadhi za taifa tatu, hivyo kufanya nchi kuwa na hifadhi za taifa nchini 22, kutoka 19 za awali zilizoko chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

"Kwa hiyo, tukichanganya na Marime Park ya Mafia na ile ya Mnazi Bay, zitakuwa zimefikia 24 na kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye hifadhi nyingi za taifa katika Afrika. Awali, Kenya ndiyo iliyokuwa ikiongoza kwa kuwa ilikuwa na hifadhi 23 za taifa.

"Hatua hii ni muhimu katika mauzo na kwa kuwa inamaanisha sasa itakuwa ni nafasi inayotutangaza kuwa na hifadhi nyingi kimataifa, inatupa nafasi ya urahisi katika kuuza zaidi," Kigwangalla alisema.

Hata hivyo, Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda (Chadema), alisema uamuzi wa serikali kubadili hadhi ya mapori ya akiba ya Ugalla na Kigosi kuwa hifadhi za taifa unakwenda kuwafanya Watanzania waliokuwa wanaishi kwenye maeneo hayo kuwa wakimbizi ndani ya nchi yao.

Mbunge wa Kaliua, Magdalena Sakaya (CUF), alisema kuwa kabla ya kuridhiwa kwa mapendekezo ya kubadili hadhi ya mapori hayo, serikali ilipaswa kusubiri kwanza ripoti ya mawaziri wanane waliotumwa na Rais John Magufuli kwenda kukagua maeneo ya hifadhi zenye migogoro ya kimipaka na wananchi. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kemilembe Lwota, alishauri kuwa ili kuepuka uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, serikali ihakiki mipaka husika kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo husika.

"Kuna vijiji viko ndani ya hifadhi na vimesajiliwa kisheria, wako wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi katika Mto Ugalla na wengine wanafuga nyuki katika mapori yote mawili (Ugalla na Kigosi).

"Kamati inaishauri serikali kuhakikisha wananchi waliomo ndani ya hifadhi hawabugudhiwi na wanawekewa utaratibu ambao hautaleta migogoro," alisema.

Akiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Ruge (Chadema), alisema kambi hiyo inaona kuwahamisha wananchi kutoka kupisha hifadhi hizo mpya ni kwenda kinyume cha kauli ya Rais Magufuli aliyesema wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi wasibughudhiwe kama wanafanya shughuli zao za kutafuta riziki.

Alisema kambi hiyo pia inaona kuna haja kuziunganisha mamlaka tatu za serikali zinazofanya majukumu yanayofanana katika sekta ya utalii, akizitaja kuwa ni Tanapa, Tawa na NCAA.

# Kundi la WhatsApp ladaiwa kutumiwa mitihani darasa 7

INATOKA UK. 2

"Baadhi ya vituo kwa mfano cha Hazina tulisema watafanyia Oysterbay, kituo cha Atlas walifanyia kituo cha Bongoyo, Ubungo Fort of Joining walifanyia kituo cha Mbezi," alisema.

Dk. Msonde alitoa wito kwa shule zote nchini zijiepushe na kufikiria, kupanga na kutekeleza njama za kuhujumu mtihani huo.

"Kamati zote za mikoa, halmashauri na jiji wamefundishwa vilivyo mwaka huu wataangalia kwa upana namna ya uzingatívu wa kanuni za mitihani. Wamiliki wa shule binafsi wasiingilie shughuli za mitihani waache vituo vyao ambavyo kwa sasa ni vya baraza ili mitihani ifanyike vizuri," alisema.

Kuhusu watahiniwa 947,221 waliosajiliwa mwaka huu kufanya mtihani huo wa darasa la saba, Dk. Msonde alisema wanatoka katika shule 17,051 Tanzania Bara. Alisema kati yao wavulana ni 451,235 sawa na asilimia 47.64 na wasichana ni 495,986 sawa na asilimia 52.36.

Alisema watahiniwa 902,262 watafanya mtihani huo kwa lugha ya Kiswahili na watahiniwa 44,959 watafanya kwa lugha ya Kiingereza ambayo wamekuwa wakiitumia katika kujifunzia.

"Watahiniwa wenye mahitaji maalum ni 2,678 kati yao 81 ni wasioona, 780 wenye uoni hafifu, 628 wenye ulemavu wa kusikia, 325 ni wenye ulemavu wa akili na 864 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwilini," alisema.

Dk. Msonde alisema katika mtihani huo, masomo matano yatatahiniwa ambayo ni Kiswahili, Kiingereza, Sayansi, Hisabati na Maarifa ya Jamii.

"Wasimamizi wahakikishe wanalinda haki ya watahiniwa wenye mahitaji maalum. Haki hizi ni pamoja na kupata mitihani yenye maandishi ya nukta nundu kwa watahiniwa wasioona na maandishi yaliyokuzwa kwa watahiniwa wenye uoni hafifu.

"Watahiniwa wote wenye mahitaji maalum waongezewe muda wa dakika 20 kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika 10 kwa kila saa kwa masomo mengine, kama mwongozo wa baraza ulivyoelekeza," alisema.

**WAONYWA UDANGANYIFU**

Wasimamizi wa mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi (darasa la saba) mkoani Shinyanga, wameonywa kufanya udanganyifu kwenye mitihani hiyo na kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua kali ikiwamo kufukuzwa kazi.

Wanafunzi wa darasa la saba hapa nchini wanafanya mtihani wao wa kuhitimu elimu ya msingi leo na kesho. Katika Mkoa wa Shinyanga, wanafunzi 30,764 wanafanya mtihani huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Kahundi, alisema maandalizi ya mtihani huo wa darasa la saba yako vizuri na kuwatahadharisha wasimamizi wasije wakafanya udanganyifu na kusababisha wanafunzi kufutiwa mitihani pamoja na wao kufukuzwa kazi.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Agnes Shayo (Tudarco), DAR na Marco Maduhu, SHINYANGA.**




Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akiwataka vijana waliojenga ukuta wa Mirerani kuripoti JKT Mgulani kesho. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Vigingi vya Nape hadi msamaha wa Rais

INATOKA UK.2

"Mheshimiwa Rais kama baba yangu, mzee wangu nakushukuru sana kwa fursa uliyonipa ya kunisikiliza, kunisamehe, kunishauri na kunielekeza ninafanyeje huko mbele ninakokwenda," alisema Nape.

Nape ambaye amewahi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, kwenye Serikali ya Awamu ya Tano, aliondolewa kwenye nafasi hiyo Machi 23, mwaka 2017.

Mbunge huyo anakuwa watatu kwenda kuomba msahama wa Rais na taarifa zake kutangazwa kwa umma.

Wengine waliokwenda kuomba msamaha ni Mbunge wa Bumbuli, January Makamba, ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Mazingira na Muungano. Aliondolewa kwenye nafasi hiyo, Julai 21, mwaka huu.

Mwingine aliyetajwa kuomba msamaha ni Mbunge wa Sengerema, William Ngeleja.

Msamaha huo unafuatia kuvuja kwa mawasiliano ya sauti zinazodaiwa kuwa ni za kwao kwenye mitandao ya kijamii baada ya kutoka kwa waraka ulioandikwa na waliowahi kuwa makatibu wakuu wa CCM, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana, kwenda kwenye Baraza la Ushauri la Wazee wakimtuhumu mwanaharakati mmoja kuwachafua.

Mawasiliano kati ya Nape na Kinana, yanadaiwa kujadili maandalizi ya waraka huo ulioelekezwa kwa Baraza hilo ambalo Mwenyekiti wake ni Rais wa Awamu wa Pili, Ali Hassan Mwinyi.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaishukuru NMB kwa misaada

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeipongeza Benki ya NMB na kusema imeendelea kuwa mkombozi kwenye jamii maeneo mbalimbali nchini kutokana na kutoa misaada sehemu zenye changamoto kubwa.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Jabiri Shekimweri, alipozungumza wakati wa kupokea msaada wa vifaa tiba vilivyotolewa na benki hiyo jana kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kikosi cha 826 Mpwapwa.

Shekimweri alisema benki ya NMB imeendelea kuwa mkombozi katika jamii kutokana na kutoa misaada kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya mahitaji.

"Mfano ni hivi vifaa tiba mlivyokabidhi leo, tunajua wote jinsi eneo la kutolea huduma za afya lilivyo na changamoto, watu ni wengi katika jamii wanaofika hapa kwa ajili ya matibabu ni kweli benki mnaigusa jamii moja kwa moja," alisema.

Hata hivyo alishukuru NMB kwa kuendelea kutoa misaada katika wilaya hiyo kwa sababu kwa mwaka huu ni mara ya tatu kwa kupata msaada wa mabati kwa baadhi ya shule za msingi pamoja na madawati.

Naye Mwakilishi wa Mkuu wa JKT, Kanali Festus Mang'wela alishukuru kwa msaada huo.

Kanali Mang'wela alisema kituo hicho kinahudumia watu wengi wakiwamo familia za askari, askari wenyewe na jamii inayokizunguka kikosi hicho.

Alibainisha kuwa vifaa walivyopokea vitawasaidia kutokana na kikosi hicho kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha sita wanaofika kwa ajili ya kozi maalumu ya kijeshi ya miezi mitatu tangu mwaka jana.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema wamekabidhi msaada huo wa vifaa tiba wenye thamani ya Sh. milioni tano.

Alivitaja vifaa hivyo ni vitanda vitano vya kawaida, mashuka 25, magodoro matano na vitanda vya kujifungulia kinamama viwili vyote vikiwa na thamani hiyo.

**Mfano ni hivi vifaa tiba mlivyokabidhi leo, tunajua wote jinsi eneo la kutolea huduma za afya lilivyo na changamoto, watu ni wengi katika jamii wanaofika hapa kwa ajili ya matibabu ni kweli benki mnaigusa jamii moja kwa moja**

# Bunge lashtukia Tanapa kutwishwa mzigo

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imesema uamuzi wa serikali wa kuanzisha hifadhi mpya ya Nyerere kwenye Pori la Akiba Selous unakwenda kuongeza mzigo mkubwa katika uendeshaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa).

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Kemilembe Lwota, akiwasilisha maoni ya kamati kuhusu azimio la kubadili sehemu ya Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, alisema kuanzishwa kwa hifadhi hiyo kutafanya Tanapa iwe na hifadhi 20 na hivyo kuwa na mzigo mkubwa kulinganisha na uwezo wake wa kuzihudumia.

Alisema kati ya hifadhi za taifa 19 zilizopo nchini kwa sasa, ni hifadhi tatu tu za Serengeti, Tarangile na Mlima Kilimanjaro zinazalisha ziada kwa ajili ya kujiendesha na kuzisaidia hifadhi nyingine 14 ambazo ni tegemezi.

Alibainisha kuwa hifadhi mbili za Ziwa Manyara na Arusha zinazalisha kiasi cha kujitosheleza kujiendesha zenyewe tu.

Alisema kamati pia inaona kuyachukua maeneo muhimu yaliyo chini ya Mamlaka ya Wanayamapori Tanzania (Tawa) ni kuipunguzia mamlaka hiyo uwezo wa kukusanya mapato na hivyo kuifanya ishindwe kujiendesha.

"Kwa mfano, katika mapendekezo ya kubadili hadhi sehemu ya Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, jumla ya vitalu vya uwindaji 37 vitaangukia katika eneo la Hifadhi ya Taifa na kubakisha vitalu 10 tu chini ya Tawa, hali ambayo kwa vyovyote vile itaathiri mapato ya Tawa ambayo yanategemea sana biashara ya uwindaji wa kitalii," alisema na kuongeza:

"Kamati inaishauri serikali niangalie uwezekano wa kuwa na mamlaka moja nchini inayosimamia uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori kama ilivyo kwa nchi jirani za Kenya, Zambia, Zimbabwe na Afrika Kusini tofauti na Tanzania ambayo wanyamapori wanasimamiwa na taasisi zaidi ya moja."

Kemilembe pia alisema kamati inapendekeza eneo lote la Pori la Akiba Selous na maeneo jirani kama Pori la Akiba Kilombero na mengine yanayopakana na Selous pamoja na bwawa la kufua umeme, vyote kwa pamoja vibadilishwe kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kama ilivyo kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Akiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu azimio hilo, Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika Wizara ya Maliasili na Utalii, Mch. Peter Msigwa, alisema wanaitaka serikali kuzisimamia taasisi na idara nyingine za uhifadhi ili kuipunguzia mzigo Tanapa kwa malengo ya kuiongeza ufanisi.

Mch. Msigwa alisema kambi hiyo pia inaitaka serikali kulieleza Bunge mpango ilionao kuipatia Tanapa motisha kama vile kuipunguzia kodi, ushuru na tozo mbalimbali ili ipate unafuu na hivyo kuhudumia hifadhi zilizoko chini yake ambazo haiwezi kujiendesha.

Alisema athari ya azimio la kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ni nchi kuwa hatarini kukosa fedha za utekelezaji wa miradi ya uhifadhi kutoka kwa washirika wa maendeleo duniani kwa kuwa Selous ni moja ya maeneo yaliyoainishwa na Umoja wa Mataifa kuwa urithi wa dunia.

Alisema utekelezaji wa azimio hilo utaiingiza nchi katika rekodi mbaya ya kutoheshimu mikataba na makubaliano ya kimataifa kwa kuwa tayari ilisharidhia Mkataba wa Unesco kuhusu Usimamizi wa Maeneo ya Urithi wa Dunia.

Mch. Msigwa alisema kambi yao inaona ingekuwa mantiki zaidi kubadili hadhi ya Pori la Akiba Selous kwa ujumla wake kuwa Mamlaka ya Hifadhi na siyo kukata vipande vipande.

Awali, akiwasilisha bungeni azimio hilo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, alisema kwa kuliridhia, taifa litaimarisha uhifadhi wa maliasili, husuan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji.




Mwendesha toroli akiwa amepakia mabomba yenye urefu kupita uwezo wa chombo katika Barabara ya Msimbazi, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kilichosababisha usumbufu kwa watumiaji wengi wa barabara hiyo. **PICHA: JOHN BADI**

# Madiwani watakiwa kuhamasisha tohara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuwahamasisha wananchi walioko katika kata zao, kuhakikisha wanafanya tohara ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) na kumkinga mwanamke kupata saratani ya shingo ya mlango wa kizazi.

Madiwani hao kutoka katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, Msalala pamoja na Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga na vijana wanaotakiwa kujitokeza kufanyiwa tohara hiyo ni wale wenye umri kati ya miaka 25 hadi 29.

Ofisa tathmini kutoka shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Youth Alliance (TAYOA), Emily Mushi, aliyabainisha hayo alipokuwa akizungumza na madiwani hao, watendaji wa kata na vijiji pamoja na wasimamizi wa vituo vya afya kwa kila halmashauri.

Alisema madiwani wanalo jukumu la kuwahamasisha wananchi hasa vijana wenye umri kati ya miaka 25 hadi 29 kujitokeza kwa wingi na kupatiwa huduma ya tohara kwenye vituo vya afya vilivyo jirani yao kama moja ya kupambana na maambukizi ya VVU.


Mushi alisema katika Mkoa wa Shinyanga wamelenga kuwafikia vijana 7,000 na kuongeza kuwa mtu anapofanyiwa tohara anakuwa na asilimia 60 ya kujikinga na maambukizi ya VVU na kumkinga mke kupata saratani ya shingo ya mlango wa kizazi kwa asilimia 30.

# Mkakati wa serikali kuwapatia ajira wenye ulemavu waanza

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imeanzisha kanzi data ya wahitimu wenye ulemavu wa fani mbalimbali ambao wana sifa za kupatiwa ajira kupitia Sekretarieti ya Ajira na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Watu wenye Ulemavu, Stella Ikupa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Leah Komanya, ambaye alihoji serikali ina mkakati wa kuhakikisha kifungu cha 31(1) cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 kinatekelezwa ipasavyo.




Akijibu, Ikupa alisema kifungu hicho kinahusu utoaji wa nafasi ya ajira kwa watu wenye ulemavu waliokidhi vigezo vya msingi vya nafasi zilizo wazi.

Alisema mikakati ya serikali ya kuhakikisha kifungu hicho kinatekelezwa ipasavyo ni pamoja na kuanzishwa kwa kanzi data ya wahitimu wenye ulemavu.

Alitaja mkakati mwingine ni kufanya kaguzi za kazi kupitia Sheria ya Taasisi za Kazi, kifungu cha 45(A) kinachompa fursa ofisa kazi kutoa adhabu za papo kwa papo.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kufanya uhamasishaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu kwa njia mbalimbali zikiwamo warsha, mikutano, makongamano, vipindi vya redio pamoja na runinga," alisema.

Aidha, alisema kwa kushirikiana na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kutoa tuzo kwa mwajiri bora ambaye ameajiri watu wenye ulemavu na kuwawekea mazingira wezeshi ya kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Ikupa alisema pia kwa kutumia programu ya ukuzaji ujuzi kwa kukuza ajira kwa kutoa mafunzo ya kitalu nyumba kwa vijana, wakiwamo wenye ulemavu katika halmashauri mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri wao wenyewe au kuajiriwa.

"Pia kutoa mafunzo kupitia Vyuo vya Ufundi kwa Watu wenye Ulemavu vya Yombo Dar es Salaam na Sabasaba Singida kwa watu wenye ulemavu ambayo yanawajenga katika kujiajiri na kuajiriwa," alisema.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akimsikiliza Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Dk. Edmund Mndolwa, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGEi**.

## Serikali yaiwezesha Benki Kilimo bil. 103/-

BUNGE limeelezwa kuwa ili kuhakikisha kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), inakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa mikopo, serikali imeipatia kiasi cha Sh. bilioni 103 kupitia mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbeya Vijijini (CCM), Oran Njeza.

Katika swali lake, Njeza alisema ili kuboresha kilimo na ujasiriamali inahitajika elimu kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuwa na vyanzo vya uhakika kwa mtaji.

"Je, Benki ya Kilimo ina mtaji kiasi gani? Na je, benki hiyo ina mkakati gani wa kuwafikia wakulima wadogo wa Wilaya ya Mbeya?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Dk. Kijaji kwa sasa benki hiyo inaendelea na mchakato wa kukamilisha masharti ya kupatiwa awamu ya pili ya mkopo wa Sh. bilioni 103 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika.

"Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imefikisha huduma zake mkoani Mbeya na kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kutoka Sh. milioni 799.9 Desemba 2017 hadi Sh. bilioni 2.54 kwa taarifa ya mwisho ya Aprili, 2019," alisema.

Alieleza kuwa mikopo hiyo imetolewa kwa miradi saba ya kilimo na kuwanufaisha wakulima 509 wa wilaya za Mbozi, Momba na Mbarali.

"Napenda kulifahamisha Bunge kwamba Benki ya TADB imefanikiwa kufungua ofisi ya Kanda ya Juu Kusini mkoani Mbeya," alisema Dk. Kijaji.

Alibainisha kuwa malengo ya ufunguzi wa ofisi hiyo ni kuhakikisha kwamba benki inasogeza huduma zake karibu zaidi na wateja wake ambao ni wakulima wote wa Nyanda za Juu Kusini, ikiwa ni pamoja na wakulima wadogo wa Wilaya ya Mbeya Vijijini.

Aliwahimiza wadau wote wa kilimo nchini wakiwamo wakulima wa Wilaya ya Mbeya Vijijini kuwasiliana na benki hiyo ili waweze kupata maelekezo sahihi ya uandaaji wa miradi itakayokidhi vigezo vya kupatiwa mikopo.

# Mbunge ahoji mkataba wa miradi majisafi

MBUNGE wa Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood, amehoji lini serikali itasaini mkataba wa kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Manispaa ya Morogoro kutokana na kukabiliwa na kero kubwa ya maji.

Akiulizwa maswali bungeni jana, Abood alisema mradi huo ambao serikali inatekeleza kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo la AFD unatarajiwa kuwakomboa wananchi kutokana na kero ya maji inayowakabili.

Aidha, alisema serikali iliahidi kuleta mradi wa maji katika jimbo hilo ambao utamaliza kero ya maji katika maeneo mbalimbali yakiwamo Kihonda, Tungi, Lukobe na Mkundi katika Kata ya Mindu.

"Je, ni lini mradi huo utaanza? Na je, mradi huo unategemewa kugharimu kiasi gani?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema jana (juzi) serikali ilifungua mchakato wa kuwapata wataalamu washauri ili mradi huo uanze kutekelezwa.

"Kazi zitakazotekelezwa ni kuongeza kina cha bwawa la Mindu, ujenzi wa mtambo wenye uwezo wa kusafisha na kutibu maji, upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji, ukarabati wa mabwawa ya majitaka," alisema.

Alieleza gharama za mradi ni EURO milioni 70 na taratibu za kusaini mkataba wa kifedha zinaendelea na zitakapokamilika utekelezaji wa mradi utaanza.

Aweso alisema ni kweli serikali iliahidi kutekeleza miradi mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Morogoro Mjini.

Alisema katika kutekeleza ahadi hiyo, serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (Moruwasa) imeandaa mipango ya muda mfupi na mrefu.

"Katika mipango ya muda mfupi, katika mwaka wa fedha 2018/19 serikali imetekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika kata za Kihonda na Mkundi," alisema.

Alibainisha kuwa mradi huo umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.9 na umewanufaisha wakazi wapatao 17,000 wanaoishi maeneo ya Kihonda, Kilimanjaro, Kiegea na Kihonda Kaskazini.





# Rivacu yakataa zuio la stakabadhi ghalani

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

CHAMA Kikuu cha ushirika mkoani Manyara (Rivacu) kimekataa zuio la Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini ya kuzuia vyama vya ushirika kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani kununua mazao ya biashara.

Mwenyekiti wa Rivacu, Michael Tsaxara, imelikataa zuio hilo wiki iliyopita alipozungumza na Nipashe.

Alisema Tume ya Ushirika imeweka zuio kwa vyama vya ushirika kuanzia Septemba 3, kwa madai havina maghala ya kutosha, hivyo alisema kuweka zuio ni kukiuka waraka wa mrajisi namba 1 wa mwaka 2019 kwa biashara za mazao ya dengu, choroko, ufuta, soya na mbaazi msimu wa 2019/2020 kupitia mfumo wa vyama vya ushirika.

Tsaxara alisema viongozi walioweka zuio la wakulima kuuza mazao yao kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa kisingizio kwamba hamna maghala ya kutosha hawajasema kweli.

Mkoani Manyara kuna maghala ya kutosha na kila kijiji kina ghala.

Aidha, alisema iwapo watazuia mfumo huu Rivacu itapata hasara ya zaidi ya Sh. milioni tano ambazo zilitumiwa kununulia vifungashio. "Kinachotushangaza aliyeweka zuio mfumo huu usiendelee kutumika hajatushirikisha sisi wa vyama vya ushirika," alisema Tsaxara.

Alisema kusitishwa kwa mfumo huu kutasababisha hasara kwenye vyama vya msingi na halmashauri maana zilikuwa zinapata ushuru na Rivacu yenyewe itapata hasara kwa kuwa wanunuzi hawataendelea kufanya kazi wakati Rivacu imeishaingia mkataba.

"Sisi hatuna tatizo la maghala hata kidogo kusema hakuna si kweli na waliosema hawajui labda wanajua walichopewa," alisisitiza Mwenyekiti wa Rivacu.

Msimamizi huyo wa ushirika alisema wao waliohamasisha mfumo huo kwa zuio hilo watashindwa kurudi kuutetea kwa wananchi maana maghala yapo halafu waambiwe hamna ni kitendo cha aibu.

Ofisa Shughuli wa Rivacu, Vivian Mahuto, alisema kusitishwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani ni kuwanyima ajira vijana ambao wanafanya kazi kwenye maghala na si kweli kwamba hamna maghala.

Alisema mfumo huu ni mzuri na kwa wakulima wa ufuta umezaa matunda kwa wakulima maana wameuza kwa Sh. 2,790 mpaka 3,000 na Rivacu ilitaka kuzindua mfumo huu Septemba 5, ila zuio hilo likawa kikwazo ambapo bei ya mbaazi ingetegemea soko linasemaje.

Lilian Macha, mkulima kutoka Masakta, alisema serikali isikubali zuio hilo kwa kuwa ni uongo na kwamba wana maghala ya kutosha.




Mkuu wa Wilaya wa Arusha, Gabriel Daqarro (wa pili kushoto), akibadilishana mawazo na Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa Benki ya NBC, Linley Kapya, wakati wa hafla ya chakula cha usiku iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Arusha juzi. Kushoto ni Meneja wa Tawi la NBC Arusha, Mirage Msuya na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega. **MPIGAPICHA WETU**

# KKKT, Jumuiya ya Kikristo zataka ukatili kutokomezwa

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na Jumuiya za Kikristo Tanzania vimewataka Watanzania kutokomeza ukatili wa kijinsia, kuanzia kwenye familia.

Kuondoa ukatili kutaleta amani na kufikia malengo ya serikali ya uchumi wa kati, ifikapo mwaka 2030 na kuondokana na umaskini.

Pendaeli Lukumay, Mratibu wa Programu ya Haki na Usawa wa Kijinsia inayotumia 'Time Travel Method' kupinga ukatili wa kijinsi Tanzania, kupitia KKKT alisema jana mjini hapa.

Aliwataka Watanzania waache ukatili wa kijinsia katika jamii kwani husababisha kukosekana kwa amani na kukwamisha shughuli za kiuchumi.

"Ukatili wa kijinsia una madhara kwa ujenzi wa uchumi na hasa sasa tunapohimiza ujenzi wa viwanda, kwani kama nyumbani kuna ugomvi hakuna maendeleo yatakayofanyika na hivyo husababisha kuongezeka kwa umaskini," alisema Lukumay.

Alitaja mifano ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii, kuwa ni ubakaji wa kwenye ndoa, udhalilishaji, kuhamisha ugomvi wa mzazi na mzazi hadi kwa watoto, kutoshiriki kikamilifu kwenye malezi ya watoto (hasa kwa baadhi ya wanaume.

Mengine ni kutowapa watoto nafasi sawa, kisa wamezaliwa nje ya ndoa, ulawiti, ndoa za utotoni, kunyima wanawake nafasi za maamuzi, ndoa za utotoni na mauaji ya watoto.

Lukumay alisema programu ya 'Time Travel Method' iliyoanzishwa mwaka 2018 itatekelezwa kwa miaka mitatu kwa kutumia kongamano la urithi wetu na sehemu za kihistoria kupinga ukatili wa kijinsia.

"Time Travel Method' ni njia tunayotumia kwenye mradi wetu, tunahusisha urithi na sehemu za kihistoria kupinga ukatili wa kijinsia, njia ya majadili kama mazungumzo hutumika kwa makundi mbalimbali ya wanawake, wanaume, vijana wa kiume, kike na watoto," alisema.

Makundi yote hujiachia kwa kuzungumza masuala ya mila na desturi nzuri na zile za kuacha na hiyo imesaidia kuleta matokeo chanya kwani ni tofauti na semina ambayo unapowaita washiriki hupata nafasi finyu, kutoa mawazo yao, tofauti na hiyo njia ambayo ni uhuru kwa mazungumzo.

Alisema mradi huo wa haki na usawa Tanzania unatekelezwa kwenye dayosisi 15 ambazo baadhi ni Dayosisi ya Kusini (Njombe), Kusini Kati ( Makete), Iringa, Ruvuma, Ziwa Tanganyika (Sumbawanga) na Kusini Mashariki (Mtwara).

Lukumay alisema mradi huo umelazimika kuegemea zaidi upande wa Nyanda za Juu Kusini, kufuatia uhitaji zaidi wa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsi na kwamba dayosisi hizo ni changa pia.

Njia ya 'Time Travel Method' ilianza nchini Sweden kati ya miaka ya 80 kwa kupitia shule kwa ushirikiano wa makumbusho na kuenea kwenye nchi 20 za Ulaya, Amerika, Afrika na Asia na katika Afrika njia hiyo hutekelezwa Kenya, Uganda, Afrika Kusini na Tanzania.

# Tanesco kudhibiti wezi na vishoka

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme (Tanesco), mkoa wa Arusha, limetangaza operesheni ya kuwabaini wezi wa umeme na vishoka, wanaowadanganya wateja kwa kujifanya maofisa wa shirika hilo.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa Tanesco, mkoa wa Arusha, Lucas Kusare, aliwaambia wanahabari kuhusu changamoto mbalimbali zinazolikabili shirika hilo.

Kusare alisema mbali na vishoka pia shirika hilo litawakamata wateja wanaoiba umeme, ikiwa ni pamoja na wale wote wanaojihusisha na vitendo vya kuhujumu miundombinu ya shirika kwa kuiba nyaya na mafuta ya transfoma.

"Pia tuna taarifa kuwa kuna wafanyakazi wa Tanesco wasio waaminifu ambao wanashirikiana na vishoka katika kuhujumu miundombinu ya shirika, nao tutawabaini na kuwachukulia hatua za kinidhamu na tutakaowakamata tutawafikisha mahakamani," alisema Kusare.

Akizungumzia kukatikatika kwa umeme mara kwa mara, katika maeneo mbalimbali mkoani hapa, Kusare alisema kwa kiasi kikubwa inasababishwa na wateja wengi kutojua kutumia rimoti za mita za umeme.

"Mita hizi za sasa zinatumia rimoti na tulizifunga juu ya nguzo lengo likiwa ni kukabiliana na vishoka na wezi wa umeme na ndio maana mteja anaongeza umeme kwenye mita yake, kwa kutumia rimoti, lakini imebainika kwamba nyingi zimeharibika kutokana na wananchi kushindwa kutumia ipasavyo," alisema.

Mkuu huyo wa mawasiliano alisema hali hiyo imekuwa ni changamoto kubwa sana kwao na kwamba kwa sasa wanawasiliana na Tanesco makao makuu, kuangalia namna ya kutatua tatizo hilo.

Aliongeza kuwa mbinu zinazotumiwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya kifaa hicho wanapoongeza umeme.

Alisema kwa siku wamekuwa wakipokea taarifa zaidi ya 50 juu ya kuharibika kwa vifaa hivyo, ambapo baadhi wamekuwa wakivipokea na kuvifanyia matengenezo madogo na kuwapa mwongozo juu ya matumizi sahihi ya vifaa hivyo.

Pia alitoa wito kwa makandarasi wote waliopewa kazi na shirika hilo, kuhakikisha kuwa wanafanya kazi zao kwa kufuata masharti na taratibu walizopewa na kuepuka kuwatumia vishoka ili kuepuka kusitishiwa mkataba wa kazi.

# Chama chasotea hati ya ardhi miaka 13

**Na Godfrey Mushi, ROMBO**

WAKATI Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiwa ametoa ofa ya kupelekewa majina ya maofisa ardhi wanaochelewesha hati za ardhi, mambo ni tofauti kwa Chama cha Ushirika wa Mazao (Amcos) cha Tarakea kilichoko Rombo, mkoani Kilimanjaro.

Chama hicho kinalia kukwamishwa na Idara ya Ardhi ya wilaya hiyo na Serikali ya Kijiji cha Kibaoni kupata hati miliki ya ardhi ya eneo lao kutokana na kufuatilia kwa miaka 13 sasa bila mafanikio.

Bodi ya chama hicho, imeweka wazi kwamba tatizo liko kati ya serikali ya kijiji na ofisi ya ardhi ya wilaya ya Rombo.

Kaimu Mwenyekiti wa Tarakea Amcos, Adam Sudi, alisema walianza mchakato wa kutafuta hati hiyo mwaka 2006 na mwaka 2007 walilipa ada ya upimaji katika idara ya ardhi ya Sh. 700,000 na kuwekewa alama za mipaka (beacons) na kisha kupewa fomu ili kuipeleka ofisi ya kijiji kupata baraka, lakini mpaka sasa hawajawahi kurejeshewa fomu hiyo, licha ya kuulizia kila mara.

"Tumehangaika sana mpaka tumemwandikia barua yenye kumbukumbu namba TRCS/HW/R/B/5/32 ya Desemba 19, mwaka jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo kukumbushia barua yetu ya Oktoba 5, 2018 inayohusu jambo hili, lakini hadi sasa hatujapata jibu. Tunamwomba Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi aje atusaidie kumaliza utata huu, tujue tunakwama wapi.

Katibu wa Tarakea Amcos, Bertha Shirima, alisema nia yao ya kutaka Waziri Lukuvi kuingilia kati ni kutimiza maagizo yake aliyoyatoa ya kutaka kufikia Februari, mwaka huu, maeneo yote nchini yawe yamepewa hati miliki ili wahusika walipe kodi.

"Sisi tunataka kuanzisha duka kubwa la pembejeo na 'hardware' (vifaa vya ujenzi) ili kuwasaidia wakulima, kama tutapata mkopo kutoka benki lakini tunakwama kuendelea na mchakato kwa sababu ya kukosa hiyo hati. Tunamshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, alipokuja hapa na alitoa amri kwa idara ya ardhi kutoa hati hiyo ndani ya siku 14, lakini hadi leo watendaji wa idara hiyo hawajatii agizo hilo," alisema Shirima.

"Agosti 10, 2006 tulipata barua kutoka Ofisi ya Ardhi Wilaya ikituonyesha gharama, upimaji, upitishaji kibali wizarani, ulipaji na upatikanaji wa hati miliki na Novemba 11, chama hiki kilikabidhi hundi namba 062643 yenye thamani ya Sh. 700,000 ambayo ilikabidhiwa kwa ofisa ardhi," aliongeza.

Mmoja wa wakulima wanaotegemea chama hicho, Didas Kireti, alieleza masikitiko yake kuhusu njama za makusudi za kukwamishwa kwa mchakato wa kuiendeleza Tarakea Amcos, akisema hatima yao hivi sasa iko mikononi mwa Waziri Lukuvi na Rais John Magufuli ambao wanaweza kuwahoji wahusika na kuchukua hatua.

Alipotafutwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kibaoni, Mathew Matoli, kutoa ufafanuzi kuhusu madai ya ofisi yake kukwamisha mchakato huo, simu yake ilikuwa ikiita bila majibu.

Hata hivyo, juhudi za kumtafuta kujibu madai hayo zinaendelea lakini pia gazeti hili limechukua hatua ya kwenda kumtafuta Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Rombo kupata kauli yake kuhusu kukwama kwa hati hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Pendo Mangali (wa pili kushoto), akiwa na wataalamu kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), wakati wa ukaguzi wa daraja la Rubumba lililopo Kijiji cha Nyarubanda Kata ya Nyarubanda wilayani humo, Mkoa wa Kigoma jana. **PICHA: TARURA**.

# Magari tisa, pikipiki vyataifishwa na serikali

**Na Paul William,** MOSHI

MAGARI tisa na pikipiki saba zilizonaswa zikisafirisha bidhaa mbalimbali za magendo katika mkoa wa Kilimanjaro, baada ya kuingizwa nchini kinyume na sheria za forodha, serikali imezitaifisha.

Taarifa iliyotolewa jana na Meneja Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kilimanjaro, Edwin Lwato, ilisema magari hayo na pikipiki zilikamatwa katika mwaka wa fedha uliopita wa 2018/19.

Kwa mujibu wa Lwato, vyombo hivyo vya moto vilikamatwa saa chache tu baada ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, kumaliza ziara yake kutembelea na kukagua ofisi za forodha katika mipaka ya Holili na Tarakea inayozitenganisha Tanzania na Kenya upande wa Kaskazini.

Magari yaliyonaswa na kutaifishwa ni lori la mizigo aina ya Canter lenye namba za usajili T 848 ARE na Canter UAL 279, gari ndogo aina ya JEEP, Toyota Noah T 933 BUP, Toyota Mark II T 524 ASS, Toyota Noah T 928 DDW na Toyota Mark X lenye namba T 890 CGT. Lingine ni gari aina ya Nissan Sunny lenye namba za usajili T 752 BJN.

Meneja huyo alisema vyombo hivyo vya moto muda wowote kuanzia sasa, vitatangazwa katika magazeti ili kuuzwa kwa njia ya mnada kwa ajili ya kulipia kodi iliyokuwa ipotee.

"Kila mwaka mamlaka imekuwa ikiongeza jitihada kubwa kuhakikisha bidhaa zote zinazoingia nchini zinafuata sheria hali ambayo imesababisha bidhaa za magendo kupungua kwa kiasi kikubwa, huku akisema changamoto kubwa ni baadhi ya wafanyabiashara kuendelea na biashara hiyo," alisema Lwato.

Pia meneja huyo alisema TRA Mkoa wa Kilimanjaro, imeendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara mbalimbali ili kutambua umuhimu wa kulipa kodi kwa manufaa ya maendeleo ya taifa na kuachana na uingizaji wa bidhaa bila kufuata sheria.

Akizungumzia zaidi mikakati ya mamlaka hiyo, Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema mamlaka imekuwa ikiendelea na operesheni yake ya mtaa kwa mtaa yenye lengo la kuwaelimisha walipakodi na kusikiliza changamoto zinazowakabili katika upande wa kodi.

Aidha, alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni baadhi ya wafanyabiashara kuwa na mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD), lakini wanafanya ujanja na hawazitumii kama ilivyokusudiwa.

# Leseni 10,000 zaozea ofisi TRA

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Kilimanjaro, imesema kuna zaidi ya leseni 10,000 za madereva wa magari ambazo zimekamilika, lakini wahusika wamezitelekeza bila kuzichukua kwa muda mrefu sasa.

Meneja wa TRA mkoani wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema jana kuwa ziko leseni ambazo zilitelekezwa au kuachwa kwa muda mrefu hadi muda wake wa matumizi kwisha na maofisa wake kulazimika kuziteketeza kwa kuzichoma moto.

Mwangosi alisema hayo baada ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, kwenda kukagua shughuli zinaziofanywa na maofisa wa TRA na kuzungumza nao kuhusu mambo mbalimbali.

"Mpaka sasa kuna zaidi ya leseni 10,000 ambazo zimeshakamilika lakini wahusika wenyewe hawajajitokeza kuchukua leseni zao, na zipo ambazo tumeziteketeza kwa kuchoma moto, baada ya muda wake kuisha bila wahusika wenyewe kuchukua," alieleza.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya watu wanaoomba leseni katika mamlaka hiyo, wamekuwa wakilalamikia kucheleweshwa kwa leseni hizo wakidai kwamba wanaambiwa hakuna karatasi ngumu za kutoa leseni hizo.

Akizungumza baada ya kufanya ukaguzi chumba kwa chumba, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema mmlaka ya mapato nchini, ndiyo inaweza kuisaidia Wizara ya Viwanda katika kufikia malengo ya Tanzania ya viwanda kwa kuwaelimisha wananchi kufanya biashara halali.

Dk. Mghwira alisema jukumu la TRA si kuwekeza katika ukusanyaji wa kodi pekee bali pia ina jukumu kubwa la kuwaelimisha wananchi ili kuongeza wigo wa biashara kwa kufungua viwanda pamoja na kufanya biashara halali.

Pamoja na mambo mengine, Mkuu huyo wa mkoa alikitaka kitengo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mkoa huo, kufanya kazi na TRA upande wa forodha ili kuhakikisha wanawasaidia wafanyabiashara wanaofanya biashara za magendo kuachana na shughuli hizo.

**Mpaka sasa kuna zaidi ya leseni 10,000 ambazo zimeshakamilika lakini wahusika wenyewe hawajajitokeza kuchukua leseni zao, na zipo ambazo tumeziteketeza kwa kuchoma moto, baada ya muda wake kuisha bila wahusika wenyewe kuchukua,**



Ukurasa 19

**DC Mtatiro asukuma ndani mafataki 12**

## Wawili wapoteza maisha kwa vurugu Afrika Kusini



Ukurasa 17



Ukurasa 14


**Ndege kuzuiwa Afrika Kusini kulikoni?**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 11, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 20

**Vyanzo mtandaoni vyaanika ujasusi wa Uholanzi, vinu vya nyuklia**

# ROBERT MUGABE, 1924-2019

- Kama Gaddafi, aliichanganya dunia kwa kupendwa, kuchukiwa kwa kiwewe

**Na Anil Kija**

MPIGANAJI Robert Mugabe hatimaye amejisalimisha na kuaga dunia wakati viungo vikiwa vimedhoofu kwa muda, kwa miezi kadhaa akawa anatibiwa katika hospitali jijini Singapore.

Ni hospitali aliyokuwa amechagua na kuizoea, iwe ni kutokana na masuala ya kitaaluma au urafiki binafsi, kwani alikuwa rafiki mkubwa wa Jamhuri ya Watu wa China, ambayo ina uhusiano wa kijadi na Singapore, ila hawana itikadi moja.

Wakati anatibiwa mara kadhaa zilitangazwa taarifa potofu za kifo chake, kuanzia alipoondolewa rasmi madarakani na jeshi mwezi Novemba 2017, taarifa za kifo zikaanza Machi 2018 na kuendelea tu.

Hulka ya kuwa mpiganaji ndiyo inayoweza kujumuisha maisha na kazi ya hayati Mugabe, kwa sababu kwa vipindi virefu vya maisha yake alikuwa katika mapambano.

Kuna wakati kulikuwa na kipindi kirefu cha amani bila mapambano ya wazi, na wengi walitazamia kuwa hali ingeendelea hivyo lakini ilikuwa ni taswira danganyifu, kwani masuala ya msingi ya mapambano yalikuwa hayajatatuliwa bado.

INAENDELEA UK.16



Marehemu Robert Mugabe, Rais wa zamani wa Zimbabwe. **PICHA: MTANDAO**

**Kagame, Museveni kuyaheshimu makubaliano ya nchini Angola?** Ukurasa 18

# Ndege kuzuiwa Afrika Kusini kulikoni?



Rais John Magufuli (katikati), akisalimiana na mmoja wa marubani walioleta ndege mpya zilizonunuliwa na serikali kwa ajili ya Shirika la Ndege nchini (ATCL), nyuma yake ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Dk. Felician Kilahama**

KWELI kikulacho kinguoni mwako' ingawa ni usemi lakini kuna ukweli ndani yake.

Haiji akilini kwa Mtanzania anayefahamu historia kati ya Tanzania na Afrika Kusini ulivyo akaweza kuamini kilichotokea Johannesburg!

Tusemeje juu ya hilo, maana inabaki kuwa kitendawili kinachotakiwa kuteguliwa haraka iwezekanavyo.

Je, ni matokeo ya Ibilisi anayehangaika duniani kutaka kuleta mafarakano na kutokuelewana kinyume na mapenzi ya Mungu?.

Naamini kuwa Mungu wetu tunayemcha na kumwabudu ni mwema sana na mwenye upendo mwingi kwetu, hivyo ataendelea kuitakia mema nchi yetu.

Hata hivyo, ni wajibu wetu kumshukuru kwa kila jambo ikiwemo hili la Amri ya Mahakama Kuu ya Gauteng, Johannesburg kuizuia Ndege yetu isitoke na baadaye kuiachia baada ya hoja za msingi za kisheria zilizowasilishwa na Serikali yetu kwenye Mahakama hiyo.

Kwa mara ya kwanza nilisikia taarifa ya kukamatwa ndege yetu kupitia idhaa ya Kiswahili ya Radio Dutch-Welle (DW) ya Ujerumani saa 12 asubuhi, Agosti 26, 2019.

Kupitia taarifa ya habari nikasikia Ndege ya Tanzania imezuiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Oliva Tambo Jijini Johannesburg.

Kilichonishitua zaidi ni pale nilipokosikia kuwa imekataliwa kuondoka kwa sababu Taifa linadaiwa mamilioni ya fedha kutoka kwa

> Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015 kufanyika, Watanzania wengi tulipenda kuwepo mabadiliko ya uongozi maana hali ilikuwa tete kiasi cha kusema yatosha (enough is enough).

mtu ambaye mali zake zilitaifishwa miaka ya nyuma.

Kwamba Mahakama Kuu-Gauteng Jijini Johannesburg, iliamuru Ndege ya ATCL ikamatwe.

Vilevile, Agosti 27, 2019 gazeti moja liliandika: "Siri ya miaka 37 iliyoiponza ndege ya ATCL, Afrika Kusini".

Kusema kweli hii ni dalili ya aina fulani ya "figisufigisu" kutoka kwa baadhi ya watu wasioitakia mema Tanzania.

Kudaiwa siyo dhambi, lakini kwa nini ndege yetu ikamatwe kwa kisingizo cha deni? Cha kusikitisha zaidi ni kuibuka madai hayo mwaka 2019. Ingawa huwa tunasema kila kitu ni wakati lakini tujiulize deni lilisubiri Tanzania inunue ndege halafu itakapokwenda Afrika Kusini ikamatwe?

Kipindi cha miaka 37 siyo kifupi je, aliona hakuna kitu cha thamani cha kukamata ila sasa ndege zipo ikawa fursa kwenda mahakamani ili ndege izuiwe?

Sasa tusemeje juu ya hayo ni dalili kwamba wapo maadui ndani na nje ya Tanzania.

Hili la kuzuiwa ndege ya ATCL ni kiashiria kwamba tukae chonjo mambo siyo shwari hasa baada ya kuona kwamba Rais John Magufuli amedhamiria kuiinua Tanzania kiuchumi.

Lakini pia kuongeza fursa nyingi za ajira pamoja na kuboresha hali ya maisha kwa kuutokomeza umaskini.

Zaidi amekuwa akisema taifa letu siyo maskini ni tajiri, naamini wapo ambao hawapendi kusikia kauli kama hiyo.

Sasa ni mwaka wa nne kwa Serikali ya Awamu ya Tano lakini miradi inayotekelezwa inatia moyo na matumaini makubwa kwamba kwa kasi hii nchi itasonga mbele kiuchumi na kijamii.

Kuizuia ndege isifanye kilichokusudiwa siyo dalili njema kwa maendeleo ya uchumi wetu. Ni vyema kwamba juhudi za makusudi zilifanyika na hatimaye ndege yetu ikaachiwa.

Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015 kufanyika, Watanzania wengi tulipenda kuwepo mabadiliko ya uongozi maana hali ilikuwa tete kiasi cha kusema yatosha (enough is enough).

Hata marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere katika moja ya hotuba zake alisema:

"Watanzania wanahitaji mabadiliko na iwapo hawatayapata ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM)-watayatafuta nje ya CCM."

Vilevile aliamini kuwa mabadiliko ya kweli yatapatikana ndani ya CCM. Hivi ndivyo ilivyokuwa mwaka 2015 baada ya Dk. Magufuli kupendekezwa kuwa mgombea wa Urais kwa tiketi ya CCM.

Nithubutu kusema kuwa mwaka 2015 Wapinzani wa CCM walikuwa na fursa nzuri kuongoza Tanzania, shida ilianza pale waliposema wanaongeza nguvu kwa kubadilisha "gea-gear" angani.

Kumbe wenzao wa CCM wakabadilisha gea ardhini hivyo wakawa na mwendo kasi zaidi kwa kutumia "katapila" badala ya gari au ndege.

Kwa kufanya hivyo ukawa ni mwanzo kwa fikra za Baba wa Taifa, kwamba mabadiliko ya kweli yatapatikana ndani ya CCM, kuwa sahihi.

Kwa muda mfupi sana tumeshuhudia mengi yakifanyika kuiletea maendeleo endelevu nchi yetu. Rais Magufuli anasisitiza sana umuhimu wa uchumi wa viwanda na taifa kufikia kipato cha kati ifikapo 2025.

Ndiyo maana amejikita kujenga miundombinu muhimu ya barabara; reli mwendokasi (SGR); kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere ili kupata umeme wa uhakika kupitia maji ya Mto Rufiji (Stigler's gorge); kuimarisha umwagiliaji; kuongeza nguvu katika huduma za afya na elimu kwa mantiki ya kuwapo nguvukazi ya kutosha ili kuzalisha malighafi kwa matumizi ya viwanda lakini pia kupata wataalamu waliobobea wenye ujuzi stahiki.

Tulijitawala kukiwepo fikra za "ubeberu" yawezekana baada ya kuona juhudi hizo zitaifanya Tanzania isonge mbele hasa kwa kutumia zaidi rasilimali zilizopo; fikra kama hizo zikaibuka tena.

Hawakosi wenye mtazamo wa "tukose wote" hivyo tuwe macho huenda yakaibuka mengine zaidi.

Wapo ambao hawapendi tuwe kitu kimoja au waone kuna kasi kubwa ya kujiletea maendeleo endelevu.

Kutakuwapo na mabeberu na maadui ndani na nje ya nchi yetu. Watatamani mengine mabaya yotokee tukwame kiuchumi lakini Mungu atafanya kweli maana anajua fikra zetu na ukweli ulivyo ila mapenzi yake yatimizwe.

Naamini hatatuacha tuhangaike bali atatufanyia njia pasipo na njia na wabaya wetu wataaibika wakati Tanzania ikisonga mbele ipasavyo.

Na kwa kuwa kabla ya Uchaguzi Mkuu 2015 kulifanyika maombi ya nguvu tukimlilia Mwenyezi Mungu atuinulie Kiongozi Mkuu wa nchi mwenye dhamira ya kweli kuondoa dhuluma, rushwa, ufisadi/wizi wa mali za umma, dawa za kulevya, uzembe na hatimaye kurejesha nidhamu na heshima kwa taifa letu tusikate tamaa yatakwisha.

Nathubutu kusema kuwa maombi yetu Mungu aliyasikia akatuinulia Rais ambaye 2015 hakuwa mgombea mtarajiwa na sasa juhudi zake tunaziona.

Anakazana usiku na mchana ili Tanzania ifanikiwe kiuchumi na kijamii na kwa manufaa ya wengi siyo tu kwa watu wachache (elite).

Mimi napongeza sana juhudi zake na Wasaidizi wake katika Serikali ya Awamu ya Tano.

Jipeni moyo songa mbele wanaobeza na kuitakia mabaya Tanzania tumwachie Mwenyezi Mungu atashughulika nao.

Muhimu tuendelee kumwomba Mungu ambaye sikio lake siyo zito asiweze kutusikia.

Kwanza, tumshukuru kwa kutuinulia Rais Magufuli; pili, tuombe aendelee kutujalia amani na utulivu ndani ya mioyo yetu na kwa taifa letu.

Tatu, amjalie Rais wetu hekima na busara ili aiongoze Tanzania kwa faida yetu na Afrika kwa ujumla.

Kama ambavyo amekuwa akisisitiza uchumi wa viwanda na kujali maslahi ya wanyonge ambao wengi wameghubikwa na umaskini; muhimu Tanzania itumie rasilimali zilizopo: ardhi, madini, watu na maliasili zote kwa faida yetu wote.

***Mungu ibariki Tanzania na Watu wake.***

***Dk. Kilahama anapatikana kupitia***
***P.O. Box 79011, Dar-es-Salaam, Tanzania,***
***fkilahama@gmail.com; +255756007400; +255714250050;***

# Kuelekea Uchaguzi ngazi ya Serikali za Mitaa nchini

## • Vijana na wanawake msibaki nyuma kuwania uongozi

**Na Reubeni Lumbagala**



Wananchi wakipiga kura kuchagua viongozi wa serikali za mitaa mwaka 2014. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KIPENGA cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kimepulizwa tayari na uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Novemba 24 mwaka huu.

Kwenye uchaguzi huo, Watanzania wenye sifa ya kupiga kura watawachagua viongozi wa vijiji, vitongoji na mitaa watakaowaongoza kwa muda wa miaka mitano ijayo hadi mwaka 2024.

Akitangaza kufanyika kwa uchaguzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo, alizitaja nafasi zitakazogombewa.

Nafasi hizo ni pamoja na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo, Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa (Kundi Mchanganyiko la Wanaume na Wanawake) na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa (Kundi la Wanawake) katika Mamlaka za Miji.

Nafasi zingine ni; Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi la Mchanganyiko la Wanaume na Wanawake), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi la Wanawake) na Wenyeviti wa Vitongoji katika Mamlaka za Wilaya.

Vijana na wanawake ni makundi muhimu katika jamii ambayo wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa serikali za mitaa, ili kupata nafasi ya kushiriki moja kwa moja kuzitafutia ufumbuzi kero za wananchi katika maeneo wanayoishi.

Vijana wa kike na wa kiume ni vyema wakawa mstari wa mbele kuwania nafasi za uongozi, badala ya kubaki nyuma na kuwa wapigadebe wa wagombea wengine.

Vijana ni kundi linalokabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinapaswa kupatiwa ufumbuzi wa haraka.

Kutokana na hali hiyo, vijana wanatakiwa kuingia katika ulingo wa kisiasa kuwania nafasi hizo.

Pamoja na kwamba wana ndoto za kushika nafasi kubwa za uongozi kama vile udiwani, ubunge na hata urais, lakini ni vyema vijana wakaanza kuzichangamkia fursa za uongozi katika ngazi ya serikali za mitaa.

Hiyo itawawezesha kujijenga, kupata uzoefu na hatimaye kuja kushika nafasi zingine kubwa.

Vijana wakishika nafasi za uongozi katika vijiji, vitongoji na mitaa yao, watakuwa chachu ya kuzitafutia ufumbuzi kero za vijana na jamii yote kwa ujumla.

Kutokana na mahesabu yasiyowiana kati ya wanaume na wanawake kwenye ulingo wa siasa, wanawake wana kila sababu ya kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi.

Aidha, kuna nafasi nyingi maalum kwa wanawake za Wajumbe wa Kamati ya Mji na Halmashauri ya Kijiji.

Hivyo basi, kujitokeza kwa wingi kwa wanawake kutachochea kuongezeka kwa idadi ya wanawake katika siasa na pia wanawake watapata jukwaa (platform) la kusemea changamoto zao na za jamii na hivyo kupata ufumbuzi wake kwa ustawi na maendeleo ya maeneo yao.

> Vijana wakishika nafasi za uongozi katika vijiji, vitongoji na mitaa yao, watakuwa chachu ya kuzitafutia ufumbuzi kero za vijana na jamii yote kwa ujumla.

### CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI VIJANA NA WANAWAKE

Ziko za aina mbalimbali, lakini kubwa kwa ujumla ni pamoja na changamoto ya ajira. Vijana na wanawake wanakabiliwa na tatizo la ajira.

Viongozi wanayo nafasi ya kushirikiana na wananchi wao katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo.

Endapo vijana na wanawake watakuwa viongozi katika serikali za mitaa, watakuwa mstari wa mbele kupigania mikopo inayotolewa na Halmashauri zao ili kuwakopesha vijana na wanawake.

Hilo likifanyika, litatengeneza fursa za kujiajiri kwa kufanya shughuli za ujasiriamali na biashara, hatua ambayo itawasaidia vijana na wanawake kukuza vipato vyao na kushiriki moja kwa moja katika ujenzi wa uchumi wa nchi yao na maendeleo kwa ujumla wake.

Ipo vilevile changamoto ya huduma bora za kijamii. Mathalani, vijana wanahitaji elimu ili kuweza kujenga mustakabali wa maisha yao. Kama watapata fursa ya kuwa viongozi, watakuwa kichocheo kikubwa cha kupigania ujenzi wa shule za msingi na sekondari ili watoto na vijana wengi wapate elimu bora.

### MAJI

Ipo changamoto ya maji ambapo wanawake wamekuwa waathirika wakubwa kwani hutembea umbali mrefu kutafuta maji, hali inayohatarisha maisha yao na hata ndoa zao.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo.

Ni dhahiri viongozi wanawake katika serikali za mitaa watakuwa mstari wa mbele kupigania usambazaji wa maji kwa wananchi.

Vilevile, wanawake watapigania uboreshaji wa huduma za afya kwa kushiriki ujenzi wa zahanati, na uwepo wa dawa katika zahanati hizo ili wao na jamii yote kwa ujumla wapate huduma bora za afya.

Aidha, kuna changamoto ya ukatili wa kijinsia kwa vijana na wanawake katika jamii. Ukatili huu utapungua kama makundi yanayofanyiwa ukatili, ikiwa ni pamoja na vijana na wanawake, watakuwa viongozi katika serikali za mitaa.

Vilevile watakuwa watetezi wa watoto ambao pia ni waathirika wa ukatili wa kijinsia katika jamii.

Muda wa vijana na wanawake kuwa watazamaji katika nyadhifa za serikali za mitaa umepitwa na wakati . Wanapaswa kuwa mstari wa mbele kwenye uchaguzi huu, ili nao wawe sehemu ya ujenzi na maendeleo ya nchi yetu. Tafakari.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyo wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: (+255) 764 666349.***

# ROBERT MUGABE, 1924-2019

• Kama Gaddafi, aliichanganya dunia kwa kupendwa, kuchukiwa kwa kiwewe



Marehemu Robert Mugabe (kushoto) akiwa na mkewe Grace Mugabe enzi za uhai wake.

**INATOKA UK.13**

Ni kipindi cha miaka 10, au labda tuseme 20 kuanzia kupatikana kwa uhuru mwaka 1980 hadi mwisho wa karne, yaani Nelson Mandela alipoondoka madarakani Afrika Kusini 1999, Zimbabwe ikafumuka punde tu.

Mazingira ya amani yalitokana na kukubaliwa katika mkutano wa Lacanster House nchini Uingereza mwaka 1979 wa misingi ya Katiba ya Zimbabwe, ambako Wazungu nchini humo walipewa viti 20 kati ya 100 na hakuna mabadiliko ambayo yangetokea katika mfumo wa umiliki ardhi kwa muda wa miaka 10.

Hadi kufika mwaka 1990 muda huo ukawa umeisha kwa hiyo suala hilo lingeleta utata kama ufumbuzi muafaka kati ya Zimbabwe na Uingereza usingefikiwa.

Lakini Mugabe akalazimika kusimama wima asiguse kitu, kwani wakati huo Mandela ndiyo alikuwa ametolewa jela na yuko katika mazungumzo ya kuunda serikali ya wengi.

Ina maana Mugabe angeifumua Zimbabwe kubadili mfumo wa umiliki ardhi baada ya kipindi cha miaka 10 kikatiba kupita, angeingiza hitilafu katika majadiliano nchini Afrika Kusini, hivyo akatoa mchango wake wa kuzuia kutumia uhuru wa nchi hiyo hadi suala hilo nyeti limalizike kwanza.

> Na kimsingi ndicho kilichokubaliwa kwenye mkutano wa Lacanster mwaka 1979, lakini Uingereza ikaanza kutoa visingizio kwanini isitekeleze makubaliano hayo.

Na hata Mandela alipoingia madarakani 1994, ilibidi Mugabe aendelee 'kukanyaga mafiga' ili Mandela afaulu katika jitihada ya kujenga kuaminiana katika utawala mpya wa walio wengi.

Ni pale Mandela alipomaliza muhula wake mmoja aliojipangia na kustaafu, ndiyo sasa Mugabe akawa huru, akawaambia Waingereza ni muda sasa wa kumaliza suala la ardhi, watoe fedha ili Waafrika wanunue sehemu kubwa ya mashamba ya Wazungu.

Ndicho kilichofanyika Kenya wakati wa uhuru mwaka 1963 Desemba, kuwa Uingereza iliingiza fedha katika benki, ikatumika kuwakopesha Waafrika kwa riba ndogo wanunue mashamba ya Wazungu waliokuwa tayari kuondoka.

Na kimsingi ndicho kilichokubaliwa kwenye mkutano wa Lacanster mwaka 1979, lakini Uingereza ikaanza kutoa visingizio kwanini isitekeleze makubaliano hayo.

Katika akili ya watawala wa Uingereza, suala hilo limegeuka sura baada ya miaka 20, yaani imekuwa ni hali ya kawaida nchini humo ambayo wanatakiwa waizoee.

Na kama ni mikopo kununua mashamba, benki zipo huko.

Msimamo huo wa Waziri Mkuu Tony Blair ulimrudishia Mugabe roho ile ya uanaharakati na upiganaji. Kwa jumla ilikuwa imefifia, huku akijaribu kujenga taifa lisilo na ubaguzi au chuki za kikabila. Ila kuna tukio ambalo liliweka doa utawala wa Mugabe katika miaka ya awali, linaitwa Operesheni Gukurahundi.

Lilitokana na 'uvinjari madaraka' (Kiingereza, adventurism) kwa upande wa aliyekuwa kiongozi mwenza wa ZANU-Patriotic Front, mkongwe Joshua Nkomo ambaye alitaka kuwa Makamu wa Rais mwenye mamlaka makubwa, kama walivyotaka kina Dk. Riek Machar wa Sudan Kusini au Dk.Jonas Savimbi wa Angola.

Iliposhindikana kuwa na madaraka hayo inaelekea aliandaa uasi, zikapatikana silaha nyingi zimefichwa kwenye shamba moja ambako Nkomo anahusika, ila kwa vile hapakuwa na uchunguzi halisi ulio huru na kuthibitisha, huwezi kusema hapakuwa na 'false flag operation.' Ni kutegewa kitu ili vita vitangazwe.

Operesheni hiyo ilifanywa na jeshi la nchi hiyo lililosheheni wapiganaji wa chama cha ZANU cha Mugabe huku wapinzani wao wakiwa ni kundi la Nkomo la Patriotic Front, iliyokuwa inaitwa ZAPU awali.

Ilielezwa kuwa jeshi la Zimbabwe lilikuwa likishauriwa au kusimamiwa kwa mafunzo ya wahenyeshaji kutoka Korea Kaskazini, ambayo unaweza kusema ilipewa nafasi hiyo ili China isiingie kwa nguvu katika Afrika kijeshi, hali ambayo ingeweza kuleta matatizo kati ya Zimbabwe na nchi za Magharibi.

Watu wengi wa kabila la Ndebele (au Matebele) waliuawa, na maelfu wengine wakakimbia.

Suala hilo hata hivyo halikuwa linasikika katika siasa za Zimbabwe miaka ya baadaye hasa baada ya Mandela kutolewa kifungoni kwani hili la mashamba ya Wazungu lilichukua nafasi kubwa na ndiyo hasa limekuwa 'suala la maisha' kwa uongozi wa Mugabe.

Alipoona kuwa Uingereza haitatekeleza sehemu yake katika makubaliano ya Lacanster, Mugabe alijua hakuna njia nyingine ila Wazungu kunyang'anywa ardhi hiyo na Waafrika waipate bure au kwa malipo kidogo serikalini kwa sababu ni yao.

Ni hoja ambayo ilikuwa haina ubishi kwa mamilioni ya Waafrika, iwe ni Zimbabwe au kwingineko, Mugabe akapata sifa.

Ila hatua hiyo iliambatana na kuporomoka kwa uchumi wa Zimbabwe kwa vile mfumo wa amana za benki na kwa maana hiyo thamani ya fedha na upatikanaji wa fedha kuendesha shughuli za kilimo na viwanda kuendana na mahitaji yaliyopo, kulitegemea uwepo wa Wazungu na amana zao benki.

Kuondolewa kwa sehemu kubwa kulifanya Zimbabwe iwe ni nchi ya wakulima wa jembe la mkono, serikali inayohitaji gharama kubwa kuiendesha, na madini ya hapa na pale kusaidia kununua mafuta kutoka nje.

Siyo tena kilimo cha tumbaku na hata mazao ya chakula yalisuasua, au kuweka ng'ombe wa kisasa, waanze upya.

Unaweza kusema kuwa sababu ya Mugabe kuchukua hatua hiyo ni 'ulevi tu' wa siasa ya Ujamaa kwa jumla, kuwa alikuwa hajui matokeo yake, kama ambavyo nchi nyingi zilizofanya mapinduzi kuwaondoa 'wanyonyaji' au 'mabepari na makabaila' waliishia kuvuna mabua uchumi ukiporomoka.

Hatua ya Mugabe ilifanana na Jenerali Idi Amin ambaye hatua yake ya kuwafukuza Wahindi na kuchana hati zao za kusafiria mwaka 1972, kulileta mporomoko wa jumla wa uchumi wa nchi hiyo, kuparaganyisha sekta za biashara na fedha.

Na kuunda tabaka la walanguzi (Mafuta Mingi) lililotawala hadi akaanguka 1979.

> Ni hoja ambayo ilikuwa haina ubishi kwa mamilioni ya Waafrika, iwe ni Zimbabwe au kwingineko, Mugabe akapata sifa.

Unaweza kusema kuwa maisha ya Mugabe na uongozi wake yalikuwa kielelezo cha Uamsho wa kizalendo na kimapinduzi katika Afrika kwa kipindi cha kufikia uhuru, halafu mapambano ya jumla ya ukombozi, kung'oa ukoloni mkongwe au madhira yake katika suala la ardhi.

Licha ya tabu ambayo Zimbabwe ilipata, Mugabe aliendelea kuungwa mkono na watu wengi, hata kudiriki kufanya uchaguzi ambao licha ya vizuizi maridhawa kwa upinzani, ulienda vyema kiasi, ikaundwa serikali ya pamoja lakini Mugabe akatumia katiba na 'uamirijeshi mkuu' kuwabana wapinzani.

***Wakajivuruga, wakasahaulika....***



Mwalimu Julius Nyerere (kulia) akiwa na Mzee Robert Mugabe enzi za uhai wao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

## Wawili wapoteza maisha kwa vurugu Afrika Kusini



Raia wa Afrika Kusini, wakiwa na magongo tayari kuwashambulia Waafrika wenzao wanaowatuhumu kuchukua fursa zao za ajira nchini mwao. **PICHA: MTANDAO**

WATU wawili wamepoteza maisha kutokana na vurugu mpya zilizofanywa na magenge ya watu nchini Afrika Kusini.

Vurugu hizo zilianza baada ya hotuba iliyotolewa mjini Johannesburg na mwanasiasa mkongwe Mangosuthu Buthelezi, dhidi ya vitendo vya chuki kwa wageni.

Buthelezi alizomewa na kundi la watu Jumapili, ambapo vikosi vya usalama viliingilia kati.

Watu 10 wakiwamo wageni wawili, waliuawa mjini humo juma lililopita, baada ya makundi ya watu kuvamia biashara zinazomilikiwa na raia wa kigeni.

Vurumai hizo zimesababisha mvutano wa kidiplomasia na nchi nyingine za kiafrika, hasa Nigeria.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa amekemea vitendo vya vurumai za siku ya Jumapili, akisema mamlaka hazitaruhusu.

"Vurugu hizo na vitendo vya uvunjaji sheria zinahatarisha usalama wa mamilioni ya raia wa Afrika Kusini na raia wa kigeni nchini mwetu ambao wana haki kwa mujibu wa sheria kuishi na kufanya biashara kwa amani."

Siku ya Jumapili watu kadhaa wakiwa wamebeba marungu waliandamana mjini Johannesburg wakiimba: "Wageni ni lazima warudi walikotoka," kilieleza chombo cha habari cha Soweten.

Kundi hilo lilielekea kwenye bustani ya Jules jijini Johannesburg mahali ambapo Buthelezi, Kiongozi wa zamani wa upinzani wa chama cha Inkatha Freedom na waziri wa serikali ya umoja baada ya ubaguzi wa rangi alikuwa akitarajiwa kutoa hotuba kuhusu mashambulizi ya hivi karibuni.

Alisema alifika kama msuluhishi na kwamba amekuwa akijisikia vibaya kutokana na machafuko nchini mwake ambayo yameharibu sifa ya Afrika Kusini barani Afrika.

Hata hivyo, alizomewa wakati wote na video iliyochapishwa kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter ilionyesha makundi ya watu wakitoka nje ya mkutano wake.

Kisha watu walianza kushambulia magari na majengo, na kuchoma moto. Mkuu wa idara ya polisi jijini Johannesburg, David Tembe, alikieleza chombo cha habari cha Eyewitness.

"Nafikiri ni uhalifu kabisa kwa sababu baadhi ya maduka yaliyochomwa si mali ya raia wa kigeni, yanamilikiwa na raia wa Afrika Kusini," alinukuliwa.

Juma lililopita, polisi walisema kuwa waliwakamata watu zaidi ya 240 na fujo hizo zilipungua.

Mamlaka ziliwakamata watu 16 baada ya fujo za siku ya Jumapili kwa mujibu wa taarifa ya Rais wa nchi hiyo.

Machafuko yalianza juma moja lililopita baada ya madereva wa malori raia wa nchi hiyo kuanzisha mgomo wakipinga ajira zinazotolewa kwa raia wa kigeni.

Nchi hiyo imekuwa ikiwavutia wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali za Afrika kwa kuwa ni moja kati ya nchi zilizo na maendeleo makubwa ya kiuchumi.

Hata hivyo, kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa ajira nchini humo na baadhi ya watu wanahisi raia wa kigeni wanachukua ajira zao. **BBC**

# Kagame, Museveni kuyaheshimu makubaliano ya nchini Angola?



Rais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto), akipeana mkono na Rais Paul Kagame wa Rwanda baada ya kufikia makubaliano ya kumaliza uhasama kati yao. Katikati ni mpatanishi Rais wa Angola Joao Lourenco. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

MARAIS Paul Kagame wa Rwanda na Yoweri Museveni wa Uganda, walifikia hatua ya kutoa matamshi yenye vitisho, na hatua kali ikiwamo kufunga mipaka ya nchi mbili hizo kutokana na mgogoro uliokuwapo kati ya wawili hao.

Nchi hizo zimekuwa na mgogoro wa kidiplomasia kwa nyakati tofauti, lakini zaidi baada ya kuibuliwa madai kwamba Uganda ilikuwa inawakamata na kuwaweka ndani Wanyarwanda waliokuwa wanaingia nchini humo.

Hali hiyo ilikuwa ni sehemu ya historia ya migogoro ya mara kwa mara kwa nchi hizo, kama ilivyowahi kutokea katika miaka ya 1990 ziliponusurika kuingia kwenye vita kutokana na mapigano ya majeshi yao huko DRC.

Majeshi hayo yalikuwa yanashiriki katika mapigano ya kumuondoa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, wakati huo ikijulikana kama Zaire, Mobutu Sese Seko.

Mgogoro mwingine ni wa hivi karibuni ambapo Uganda iliishutumu Serikali ya Rais Kagame kwa kuzuia malori ya mizigo na magari mengine kutoka nchini mwake kuingia Rwanda.

"Utawala wa Rwanda uliyazuia maroli na magari mengine kutoka Uganda kuingia nchini humo," Msemaji wa Serikali ya Rais Museveni, Ofwono Opondo, akawaambia waandishi wa habari.

Kwa mujibu wa Opondo, maroli ya mizigo yanayofikia 129 kutoka Uganda yalikuwa 'yamekwama' kwenye mpaka wa Gatuna kwa wakati huo.

> Tumekubaliana mambo mbalimbali yatakayotekelezwa na nchi zetu mbili hizi, kwa sehemu kubwa ikimaanisha kuboresha usalama, biashara na uhusiano wa kisiasa.

Hata hivyo, serikali ya Rais Kagame kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Richard Sezibera, ilikanusha shutuma hizo na kufafanua kwamba magari hayo yalielekezwa kupitia mpaka wa Kagitumba uliopo Kaskazini mwa nchi hiyo ili kupisha ujenzi wa barabara yenye shughuli nyingi katika mpaka wa Gatuna.

Zipo tuhuma nyingi zilizotolewa kwa kila upande dhidi ya mwingine, kiasi cha kusababisha kukua kwa tofauti kati ya nchi hizo zilizo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Agosti 21, mwaka huu, marais hao waliowahi kukumbwa na migogoro ya kidiplomasia na majirani zao kwa nyakati tofauti, wakaingia katika historia mpya, wakijaribu kufunga mipaka ya uhasama wao kupitia makubaliano waliyowekeana saini jijini Luanda, Angola.

Walifikia makubaliano hayo katika mkutano wa pili huko Luanda mbele ya marais Joao Lourenco wa Angola, Felix Tshisekedi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Denis Sassou Nguesso wa Congo.

Mtaaluma wa sayansi ya siasa, John Mkorya, anasema makubaliano ya viongozi hao kama yatatekelezwa, yatasaidia kushusha joto la mzozo wa kidiplomasia lililokuwapo kati yao na kuathiri wananchi wa mataifa hayo.

Viongozi hao wawili wamekubaliana kutilia mkazo kutatua mzozo wowote baina ya mataifa yao kwa njia Amani, kwa mujibu wa Shirika la Habari la Angola (Angop).

**ASILI YA MGOGORO**

Mnamo Machi mwaka huu katika hotuba kwenye mkutano wa kitaifa, Kagame akaelezea kuwa chimbuko la mgogoro baina ya nchi yake na nchi ya Uganda ni la tangu miaka 20 iliyopita nchi ya Uganda ikitaka kuangusha utawala wake.

Kagame akasema mgogoro huo ulishika kasi hivi karibuni kufuatia wananchi

wa Rwanda wanaoingia nchini Uganda au kufanya kazi nchini humo kukamatwa na kuzuiliwa sehemu ambazo hazijulikani, kisha kufanyiwa vitendo vya mateso kwa madai kuwa ni mashushushu.

Lakini Uganda nayo mara kadhaa, imeishutumu Rwanda kuwatuma majasusi na kufanyia vitendo vya ujasusi kwenye ardhi yake. Kwa upande wake, utawala wa Rwanda umekuwa ukikanusha kama ilivyo kwa utawala wa Uganda.

Wakati swali likibaki kuwa, ikiwa Kagame na Museveni watatekeleza makubaliano ya Luanda kwa vitendo, wawili hao wanaonyesha hatua za awali za kushukuru hatua iliyofikiwa.

Museveni anamshukuru Rais Lourenco wa Angola, kwa kufuatilia utekelezaji wa mchakato uliofanikisha nchi mbili hizo kusaini makubaliano ya kuboresha uhusiano wa kisiasa na kidiploasia.

"Ninawashukuru marais Lourenco na Tshisekedi kwa kuja wao, kwamba tutashirikisha taarifa tulizonazo na kuhakikisha tunatoa tamko la pamoja na Rwanda," akasema Museveni.

Hata hivyo, Museveni akasema alishawasiliana na Kagame kutafuta suluhu ya mzozo uliokuwapo kati yao wakati Lourenco na Tshisekedi walipomwalika.

"Nilishawasiliana na Kagame kupitia njia zetu za mawasiliano, lakini suala hili limekuja kama uimarishaji wa kufikia lengo letu. Tunathibitisha namna tulivyokuwa wakuu wa Umoja wa Afrika," akasema Museveni.

Viongozi wa Angola and DR Congo ni wawezeshaji wa mpango wa kufikia suluhu kwa Kagame na Museveni kusaini makubaliano ya kuondoa mvutano uliokuwapo kati yao.

**MAKUBALIANO**

Makubaliano waliyoyafikia ni pamoja na kila upande, kuheshimu mamlaka ya taifa jingine na zile za nchi majirani zao.

Walikubaliana kutoshiriki vitendo vinavyochangia kudhorotesha utulivu ama kuchochea uhasama kwa taifa jingine ama mataifa jirani.

Pia walikubaliana kuondoa viashiria vyote vinavyoweza kuibua hisia hizo ikiwa ni pamoja na ufadhili, mafunzo ama kuingiza vikundi vyenye kuathiri utulivu kwa nchi husika.

Viongozi hao watatakiwa kuheshimu na kulinda haki na uhuru wa watu wa taifa jingine watakaoingia ama kupitia kwenye mipaka ya nchi zao kwa mujibu wa sheria za nchi husika.

Makubaliano hayo yakagusia pia suala la nchi hizo kurejesha shughuli za biashara na muingiliano wa watu mipakani, ili raia wapite na mizigo kusafirishwa.

Ili kutekeleza suluhu hiyo, Kagame na Museveni wakakubaliana kuanzisha kamati maalum ya muda itakayoongozwa na mawaziri wa mambo ya nje wa mataifa hayo na kuwajumuisha mawaziri wa mambo ya ndani, watawala na wakuu wa intelijensia watakaofanya ufuatiliaji.

Viongozi hao waliwahi kuwa marafiki wa karibu katika harakati tofauti za kutafuta fursa za kuyatawala mataifa yao, lakini mara kadhaa wamejikuta katika mizozo na migogoro inayohatarisha utulivu na uhusiano wa kiuchumi, hasa kwenye ukanda wa Afrika Mashariki.

Museveni anasema makubaliano hayo yatarejesha uhusiano mwema wa kisiasa na kiuchumi kati ya Uganda na Rwanda.

"Tumekubaliana mambo mbalimbali yatakayotekelezwa na nchi zetu mbili hizi, kwa sehemu kubwa ikimaanisha kuboresha usalama, biashara na uhusiano wa kisiasa. Uganda tupo tayari kabisa kutekeleza makubaliano haya," akasema.

Wakati Museveni akisema hayo, Kagame anabainisha, "Itachukua muda kiasi kwa nchi zetu hizi kuelewana kila mmoja, lakini ninafikiri tumetoka mbali."

Mpatanishi wa waliokuwa 'mahasimu wa kisiasa', Rais wa Angola, Lourenco akapongeza hatua hiyo yenye kutoa tafsiri kwamba Kagame na Museveni wapo tayari kusuluhisha mgogoro uliokuwepo.

Pamoja na utayari huo wa maneno, bado inaendelea kusubiriwa kuona ikiwa makubaliano ya Angola yataleta mageuzi ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo.

# Mkuu wa Wilaya Mtatiro asukuma ndani mafataki 12

## • Ni kukomesha mimba za wanafunzi Tunduru

**Na Sabato Kasika**



Mkuu wa wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro. **PICHA: SABATO KASIKA**

JULIUS Mtatiro ni miongoni mwa wakuu wapya wa wilaya walioteuliwa hivi karibuni na Rais John Magufuli na kupelekwa Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma.

Rais Magufuli alimteua Mtatiro Julai 14 mwaka huu ikiwa ni takribani mwaka mmoja tangu alipojiengua kutoka katika Chama cha Wananchi (CUF) na kujiunga Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwanasiasa huyo machachari aliyepitia nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya CUF kabla kujiunga CCM, alichukua nafasi iliyoachwa wazi na Juma Homera, aliyepandishwa cheo na kuwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi.

Mtatiro anasema mara baada ya kuteuliwa, aliahidi kwamba kipaumbele chake cha kwanza kitakuwa ni kushirikiana na wananchi na viongozi wenzake kusukuma mbele mipango na shughuli mbalimbali za maendeleo ya wilaya hiyo kwa ujumla.

Anasema, baada ya kufika kwenye kituo chake cha kazi alikutana na tatizo ambalo ameamua kuanza nalo kwa nguvu zote akishirikiana na wadau kuhakikisha linakoma.

Mkuu huyo wa wilaya anataja tatizo hilo kuwa ni mimba kwa wanafunzi linalosababisha wakatishe masomo na kushindwa kutimiza ndoto zao za baadaye walizojiwekea kwa ajili ya maisha yao.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili wiki hii Mtatiro anabainisha ukubwa wa tatizo hilo ulivyo katika wialaya yake na jinsi anavyokabiliana nalo kwa kushirikiana na wadau wakiwamo walimu, wazazi, madaktari na wanasheria.

**SWALI: Unasema tatizo la mimba kwa wanafunzi ni kubwa, hebu elezea ni kubwa kiasi gani?**

**JIBU:** Ni kweli tatizo ni kubwa hasa kwa wanafunzi wa sekondari, kwani Januari hadi Agosti mwaka huu zaidi ya wanafunzi 100 wa sekondari wamekatisha masomo kwa sababu ya kupachikwa mimba. Hili ndilo tatizo nililolikuta na nimeamua kuanza nalo ili kuhakikisha linakoma na kuwaacha wanafunzi wa kike wasome ili watimize ndoto zao.

Katika kipindi cha takribani miezi miwili tangu niteuliwe kushika nafasi hii, nimegundua kuna changamoto zinazoikabili Tunduru, lakini hili la mimba kwa wanafunzi si la kuchekea... kufanya hivyo ni kumwangamiza mtoto wa kike.

**SWALI: Katika ufuatiliaji wako, umegundua kuwa chanzo cha kuwapo kwa mimba hizo ni kipi, na umechukua hatua gani?**

**JIBU:** Vyanzo vya mimba hizo vinaweza kuwa vingi vikiwamo vya mazingira ya kusomea kutokuwa rafiki kwa wanafunzi, upungufu wa shule, vyumba madarasa, vyoo na huduma muhimu za kijamii kama maji na umeme... Lakini umbali wa shule na makazi wanayoishi wanafunzi, ambayo inaweza kusababisha kurubuniwa na waendesha bodaboda wakati wakitoka shule.

> Katika kipindi cha takribani miezi miwili tangu niteuliwe kushika nafasi hii, nimegundua kuna changamoto zinazoikabili Tunduru, lakini hili la mimba kwa wanafunzi si la kuchekea...

Pamoja na hayo yote, jamii nayo inachangia sana kwa kuona tatizo la mimba kama jambo la kawaida. Imefikia wakati baadhi ya wazazi kukubali kupewa chochote na wale wanaowapa watoto wao mimba ili mambo yaishe na wengine kuruhusu watoto wao waolewe kimya kimya kana kwamba ni jambo la kawaida. Vilevile baadhi ya wazazi na wanafunzi wenyewe kutoona umuhimu wa elimu.

Hayo yote ni sababu kuu ya kuwapo kwa mimba hizo. Kuhusu hatua nilizochukua ni kwamba tayari mafataki 12 wako gerezani. Aidha, kuna wasichana watatu nao wako gerezani kwa tuhuma za kutoa mimba. Ninafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na walimu, wazazi, wanasheria na madaktari na vyombo vya dola, kwani mbali na kuwakamata watuhumiwa, tumekuwa pia tukielimisha jamii madhara ya mimba hizo, umuhimu wa elimu, madhara ya mimba za utotoni na hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya wahusika. na pia kukamatwa kwa wahusika ili kuhakikisha tatizo hilo linakuwa historia.

**SWALI: Mwitikio wa wananchi ukoje kwenye kampeni hizo za kutokomeza mimba Tunduru?**

**JIBU:** Kwa sababu tunakamata na pia tunawaelimisha watambue umuhimu wa elimu, mwitikio wao na wapo ambao wametoa ushirikiano hadi kufanikiwa kuwakamata mafataki 12, hivyo ninaweza kusema kwamba tunakwenda vizuri katika vita hii ya kutokomeza mimba kwa wanafunzi na hatimaye kama nilivyosema, mwisho wa siku tatizo la mimba litakuwa historia Tunduru. Lengo lango la kuambatana na wadau hao wote ni kama nilivyoeleza. Mimi Nimeletwa Tunduru kumsaidia rais, hivyo sitarajii kumwangusha katika hili, nitapambana nalo hadi kuhakikisha linakwisha. Ndio maana ninatembea na timu kubwa ya wadau ambao kwa kweli wananipa ushirikiano mkubwa katika vita hii ambayo tunamwangamiza mtoto wa kike.

**SWALI: Mbali na njia hizo unazotumia kuna nyingine zaidi kwa ajili ya kufanikisha vita hiyo ya kuokoa watoto wa kike?**

**JIBU:** Njia nyingine ni kuwawekea mipaka wenyeji wa Tunduru kuhusu mambo ya mila hasa jando na unyago, kwani navyo vina mchango kwenye mimba hizi. Nimeelekeza mambo ya jando na unyago yaendelee kufanyika, lakini watoto wa kike wasifundishwe mambo ya kikubwa, kwani mwisho wa siku wanakwenda kufanya majaribio na kujikuta wakipata mimba. Hivyo sikukuu za jando na unyago zinafuatiliwa kwa karibu sana ili kuhakikisha watoto wanafundishwa maadili mema, siyo kuelekezwa kufanya mambo ya ovyo. Tumechukua hatua hizi kwa lengo zuri tu la kuzuia mimba. Hivyo jamii yote ya wana Tunduru iendelee kutuunga mkono kwa ajili kuandaa kizazi chenye kuzingatia maadili mema.

**SWALI: Kuna changamoto zozote ambazo unakumbana nazo katika kampeni hizi za kutokomeza mimba kwa wanafunzi Tunduru?**

**JIBU:** Ndugu yangu, hakuna shughuli ambayo inaweza kuwa ya mteremko, kila shughuli ina changamoto zake, hivyo hata katika vita hii changamoto zipo, lakini tunaendelea kukabiliana nazo. Kwa mfano wapo baadhi ya wazazi ambao bado ni wagumu kuelewa, wanawaficha watu waliowapa mimba watoto wao.

Yaani kama wazazi wamehusika katika hilo, wakijua kwamba serikali inakwenda kwenye vijiji vyao, wanakimbia kwenda kusikojulikana. Sisi kampeni hii tumeanzia ngazi ya chini kabisa kwenye vijiji, ambako huwa ninakwenda na timu yangu na kukutana na mambo mengi ya ajabu yakiwamo hayo ya baadhi ya wazazi kukimbia. Hata hivyo, nina uhakika tatizo hili la mimba litafika mwisho.

Ninataka dhana inayosema "Ukimuelimisha mtoto wa kike utakuwa umeelimisha taifa," ifanye kazi. Sikubaliani na mtindo wa kuwatumia watoto wa kike na kuwaharibia malengo yao ya baadaye.

# Vyanzo mtandaoni vyaanika ujasusi wa Uholanzi, vinu vya nyuklia Iran



Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

TAARIFA iliyovujishwa na Yahoo News, kijarida cha mtandaoni zinasema kuwa kipenyezi cha siri cha Uholanzi kiliwezesha shambulizi kwa virusi vya kompyuta la Stuxnet dhidi ya mfumo wa urutubishaji wa madini ya kufua nguvu za atomiki wa Iran.

Taarifa hiyo ilisema kuwa nchi ya Uholanzi ilikuwa na nafasi maalum ya kupata nyaraka nyeti kuhusu mpango wa Iran wa kununua vifaa vya mpango wake wa nyuklia kutoka Ulaya na hivyo ikawezesha mipango ya Marekani na Israel kuuhujumu mpango huo.

Uholanzi ilipata nafasi ya kuangalia kwa kina mpango wa nguvu za nyuklia na vinu husika, hivyo Uholanzi ikaingiza jasusi katika kazi hiyo, aliye raia wa Iran.

Jasusi huyo alifanya kazi ya kuingiza virusi vya Stuxnet katika vinu vya nyuklia vya Iran huko Natantz kwa mujibu wa Yahoo, ikiainisha kuwa imepata taarifa hizo kutoka vyanzo vya nchi za nje.

Maofisa wa Shirika la Ujasusi la Israel, Mossad au majasusi wa amani wa shirika hilo au wale wa Shirika la ujasusi la CIA nchini Marekani, waliosemekana walihusika na operesheni hizo walikubali kuzungumzia suala hilo, kwa mujibu wa gazeti la kila siku la Israel, Jerusalem Post.

Inasemekana kuwa virusi vya Stuxnet vilivuruga vituo 2,000 vya mitambo hiyo ya Iran, hali ambayo ilizuia kuendeleza mipango ya urutubishaji wa uranium kwa takriban miaka miwili.

> Taarifa zinasema kuwa mtandao wa kuhujumu mitambo ya urutubishaji ilihusisha kundi la nchi za magharibi, kuwa wahusika wakuu walikuwa Marekani na Israel...

Taarifa hiyo ilisema kuwa muda huu ulionunuliwa kwa mizunguko hasi ya kuvurugwa kwa uendeshaji wa mpango wa urutubishaji katika kipindi cha 2008 hadi 2010 iliongeza shinikizo na nafasi ya kuisukuma Iran itafute suluhu kuhusu suala hilo.

Wanasema hali hiyo ilichangia kwa kiasi kikubwa kuweka mazingira ya changamoto kwa utawala wa Iran, hasa suala la kuwa na matumaini ya kufikia malengo ya urutubishaji uranium na kutengeneza silaha za nyuklia kwa gharama ambazo Iran inaweza kubeba.

Hali hiyo ilifikia mkataba wa kimataifa wa mwaka 2015 ambao kimsingi ulifikiwa kati ya Iran na Marekani, na nchi tano nyingine kubwa zikiwa shahidi.

Imechukua miaka kadhaa hadi ikafahamika kwa uchunguzi wa kina wa matatizo ya shughuli hiyo ya urutubishaji, zikiwamo taarifa ambazo Iran inatoa kwa wakaguzi wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) kuwa hujuma ya kina ilitokea.

Ilianza kufahamika ilikuwa ya namna gani na ilipangwa vipi, ndiyo wachunguzi wa Iran wakaanza kufuatilia kilichotokea wakati wanatafuta kununua vifaa muhimu kutoka Umoja wa Ulaya (EU), pamoja na kupata wataalamu wa kuvifunga na kuviendesha au kujenga uwezo wa kuvisimamia. Ndiyo hujuma ikajionyesha.

Taarifa zinasema kuwa injinia raia wa Iran aliajiriwa kwa shughuli hiyo na shirika la ujasusi la Uholanzi, AIVD, na suala hilo limethibitishwa na vyanzo vinne vya kijasusi vilivyofuatilia suala hilo kwa kina.

Injinia huyo aliwapatia waajiri wake data muhimu zilizowawezesha waunda virusi wa Marekani kujenga kirusi ambacho kinalenga mifumo ya urutubishaji ya Natanz.

Baada ya Marekani kukamilisha uundwaji wa kirusi hicho, wadadisi wanasema kiliwekwa katika 'flash' ya kupenyeza katika kompyuta kwani mfumo wa urutubishaji usingeweza kuguswa kupitia intaneti.

Bado wachunguzi walikuwa wanajiuliza kama injinia huyo aliweka mwenyewe 'flash' hiyo katika mfumo wa kompyuta wa mitambo ya urutubishaji na mtandao wa vinu eneo la Natanz, au kama alimpa mtu mwingine 'flash' hiyo na wakati anaitumia kukawa na hitilafu, au kirusi kikapenya.

Taarifa zinasema kuwa mtandao wa kuhujumu mitambo ya urutubishaji ilihusisha kundi la nchi za magharibi, kuwa wahusika wakuu walikuwa Marekani na Israel, lakini pia Uholanzi na Ujerumani zilihusika.

Pia inasemekana kuwa mashirika ya ujasusi ya Ufaransa na kwa kiwango fulani Uingereza yanaaminika yalishiriki pia katika mpango huo, kwa njia tofauti.

Ingawa Uholanzi ndiyo iliyomtafuta injinia jasusi kuingiza kirusi katika mfumo wa kompyuta wa vinu vya urutubishaji, ilifanya hivyo kwa msukumo wa CIA na Mossad.

Taarifa hizo zinaeleza kuwa Ujerumani ilitoa vielelezo kadhaa vya kiufundi na utaalamu kuhusu mifumo ya uendeshaji mitambo iliyotengenezwa na kampuni yake ya Siemens, iliyotumika Iran kudhibiti uzungushaji mitambo ya urutubishaji.

Ufaransa pia ilitoa mchango katika upelelezi wa nchi za Magharibi na hasa Marekani kuhusu mitambo ya Iran, ila Uholanzi ilikuwa na nafasi ya kipekee kwa hali hiyo.

Taarifa zinasema kuwa vinu vya Natantz vilijengwa kwa mfumo wa michoro iliyoibwa kutoka kampuni ya Uholanzi na mwanasayansi wa Pakistan, Abulkadir Khan, ambaye aliitumia kuunda mitambo ya nyuklia ya Pakistan, na pia ili kuzisaidia Iran na Libya.

Katika miaka mingi ya juhudi za majadiliano iliyofuata, CIA na Mossad ziliwavuta Waholanzi na injinia wao kushirikiana na kuwa mtu huyo awe ndiye kiungo wao kwa mitambo ya Natantz wakati wanajenga kirusi hicho ambacho kingeingia katika historia.

Wadadisi wanasema kuwa mizunguko iliyofuata baadaye ya mashambulizi dhidi ya mfumo wa urutubishaji Iran haikuhitaji injinia huyo kuwapo hapo bado.

Kuwapo kwake katika hatua za mwanzo na undani wa siri za kiufundi wa mitambo na mifumo ya mawasiliano ya kompyuta inayoendesha mitambo hiyo ambayo tayari alikuwa amezipatia CIA na Mossad vilitosha kuwezesha shughuli za hujuma kuendelea bila yeye kuwepo, baadaye.

Pia wadadisi wanasema kuwa kutokuwapo kwa injinia huyo mahali hapo katika hatua za baadaye kuliwapatia nafasi wahujumu wa CIA na Mossad kusukuma virusi kwa nguvu zaidi kuliko awali.

Ni kwa sababu hapakuwa tena na suala la kuhofia kuwa mtu wao anaweza kugundulika, auawe.

Alipoulizwa kuhusu tofauti za hisia zilizojitokeza kati ya CIA na Mossad katika operesheni hiyo, mshirika wa zamani wa Mossad alisema kuwa wale wanaopinga Israel kuwa inatumia nguvu na shari kupita kiasi katika masuala hayo hawako hatarini kwa kiasi kikubwa na mpango wa nyuklia wa Iran.

Wako pia wanaodhani kuwa kutokuwapo kwa injinia huyo mwajiriwa wa Uholanzi katika eneo la mitambo siyo tu kulizidisha mashambulizi kwa kutumia kirusi Stuxnet, lakini pia kulichangia kugunduliwa kwa mashambulizi hayo.

Sababu ni kuwa endapo kuna mtu anayetoa kirusi katika eneo husika, inakuwa vigumu zaidi kugundua uwepo wa hujuma kuliko kirusi kikiingia katika mifumo ya uendeshaji kutoka nje, ila hawasemi kuwa angeendelea kuwepo tu.

Kuna eneo jingine la kushangaza kuhusu injinia huyo alivyoingia katika upana wa kitaalamu wa ushauri na uelekezi kuhusu uendeshaji wa mitambo, kuwa alishindwa kuingilia mfumo wa Natantz akitumia kampuni moja hewa.

Alifaulu kwa kutumia kampuni nyingine hewa kushiriki katika mtandao wa wataalamu wanaotumiwa na Uholanzi kwa ajili ya kazi hiyo ya Iran, akielekezwa na Mossad.

Haikueleweka pia ni vipi watoa taarifa walijitolea kusema hivyo sasa.



## HABARI MBEYA

# Wanahabari wapewa somo rushwa ya ngono

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAANDISHI wa habari wanawake mkoani Mbeya, wameshauriwa kuwa jasiri, kujitambua na kujiamini katika kutimiza majukumu yao ya kihabari kwani wana uwezo mkubwa badala ya kutoa rushwa ya ngono ili kupata fursa mbalimbali zinazotolewa.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya, Festo Sikagonamo, wakati wa mafunzo ya masuala ya jinsia na usalama mahali pa kazi yaliyoandaliwa na Chama cha Wafanyakazi Waandishi wa Habari Tanzania (Jowuta) yaliyofanyika jijini Mbeya.

Sikagonamo alisema wanahabari wanawake nchini wanakabiliwa na vikwazo vingi katika kutimiza majukumu yao vikiwamo vitendo vya rushwa na mfumo dume.

Alisema vitendo hivyo vimesababisha wanawake kushindwa kutimiza majukumu yao ipasavyo kwa sababu kutokana na mazingira magumu baadhi yao hulazimika kutumia miili yao kupata fursa.

"Zipo changamoto wanazokabiliana nazo wanahabari wanawake na kubwa zaidi ni rushwa ya ngono kazini baadhi ya waajiri na wahariri hutumia nafasi zao kuwataka kimapenzi. Wanaokataa wanafukuzwa kazi au kujenga uadui nawaomba mjiamini muwe majasiri mnaweza kufanya mambo makubwa bila kutoa rushwa," alisema Sikagonamo.

Aliongeza kuwa mwanahabari wa kike anapaswa kujiamini na kuwa jasiri wa kukataa rushwa ya ngono kwa kiongozi yeyote ili ampatie kazi au habari yake itoke badala yake ajiamini kwa sababu anaweza kusimama kwa miguu yake mwenyewe kulingana na ubora wa kazi yake.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Wanahabari Tanzania Jowuta, Saphia Ngalapi, alisema lengo la kuanzisha mafunzo hayo kwa wanawake nchini ni kuwajengea uwezo ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Wanawake ndiyo waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili kutokana na mazingira na maumbile yao kwa kutambua changamoto hizo waliamua kutoa mafunzo hayo ili kujenga uelewa ili watambue namna ya kukabiliana navyo.

Aidha, elimu ya usalama mahali pa kazi ni muhimu kwa waandishi wa habari wanawake kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sababu wataweza kukabiliana na changamoto ikiwamo vipigo na kunyang'anywa vifaa vya kazi.

Baadhi ya washiriki katika mafunzo hayo akiwamo Rukia Chasanika, alisema yamemwongezea uelewa wa namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati wa kutimiza majukumu yake.

Alisema mwanahabari wa kike anaweza kusimama kwa miguu yake kwa sababu anauwezo wa kuandika habari kuliko kutumia mwili wake kusaidiwa habari au kupata fursa.

# Wakala TFS waonya ujio wa jangwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, umetahadharisha wananchi kuacha kukata miti ovyo ili kuepusha jangwa.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na Meneja Msaidizi wa TFS, kanda hiyo, Innocent Lupembe, wakati wa mahojiano maalum na Nipashe kuhusu namna ambavyo wanakabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira hasa msimu huu wa kiangazi.

Alisema ukataji miti na uchomaji misitu kwenye hifadhi za misitu vimekuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira na ndiyo unaosababisha mabadiliko ya tabianchi.

Alisema misitu ikitunzwa na kuhifadhiwa katika mazingira yanayolindwa italeta manufaa katika jamii lakini pia itakuwa urithi kwa vizazi vijavyo.

"Jukumu la kutunza na kuhifadhi misitu sio la TFS pekee yake bali kila mwananchi anapaswa kulinda. Hakikisheni hakuna shughuli zozote za uvunaji, ukataji na uchomaji misitu zinafanyika."

Alisema na kuwaambia watoe taarifa kwenye mamlaka kwa yeyote atakayekata miti ovyo ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Lupembe, alisema katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira wa Wakala wa Huduma za Misitu Kanda ya Mbeya kwa kushirikiana na wadau wengine wameanzisha kampeni ya upandaji miti ambayo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji kama vile mikuyu, miembe pori, migunga mipori.

Aliongeza kuwa sera ya misitu inahimiza ushirikishwaji wa wananchi katika kutunza na kuhifadhi misitu kwa faida ya sasa na ya baadaye na kuongeza kuwa sheria namba 14 ya mwaka 2002 inatoa mwongozo na taratibu kwa mwananchi kufuata anapohitaji kuvuna misitu.

Chifu wa Jiji la Mbeya, Rocket Mwashinga, aliwaomba TFS kuwaachia jukumu la kulinda misitu kwa sababu ni miongoni mwa majukumu waliyopewa tangu enzi.



Binti mchuuzi wa korosho akizinadi kwa abiria katika Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI.**

# Mbeya waamshwa kupinga ukatili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKAZI wa Mbeya wameonywa wasinyamazie ukatili wa kijinsia badala yake watoe taarifa kila vitendo hivyo vinapotokea.

Wamekumbushwa kuripoti matukio ya ukatili dhidi ya watoto na wanawake ili hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo kwenye jamii.

Meneja Programu wa Shirika la kiraia linalojihusisha na utoaji wa elimu na msaada wa kisheria (Mbepace), Laiki Ndagile, alitoa rai hiyo jana.

Alisema kuwa watoto na wanawake wanafanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo vipigo visivyo vya kiutu na ubakaji.

Alisema licha ya wanawake na watoto kuwa waathirika wa vitendo vya ukatili jamii na watendewa wamekuwa waoga kuripoti vitendo hivyo kwenye vyombo vya sheria kwa sababu wanaofanya vitendo hivyo ni ndugu wa karibu.

"Kumekuwa na woga kwa baadhi ya familia ndugu zao wamefanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kubakwa au kulawitiwa wakiogopa kuharibu uhusiano dhidi ya watendewa na kuficha aibu jambo ambalo ni kinyume na haki za binadamu, nawaasa jamii tubadilike tusikubali kuvumilia," alionya Ndagile.

Aliongeza kuwa Shirika la Mbepace limekuwa likitoa elimu ya msaada wa kisheria na kuwajengea uwezo maofisa watendaji wenyeviti wa vijiji, walimu na wananchi kwenye wilaya za Kyela, Rungwe na Mbeya.

Alisema elimu hiyo imesaidia kupunguza vitendo vya ukatili, ambapo katika kipindi cha mwaka 2017/2018, jumla ya kesi 528 ziliripotiwa kwenye shirika hilo.

"Tumejipanga kuzijengea uwezo taasisi za elimu hususani wanafunzi na kamati za wazazi ili washiriki kikamilifu kwenye ulinzi na haki za watoto kwenye wilaya tunazofanya nazo kazi," alisema Ndagile.

Mmoja wa wasaidizi wa kisheria kutoka Wilaya ya Kyela, Tatu Hussein, alisema wanafanya kazi kwenye mazingira magumu kwa sababu ya kukosa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa vijiji wanapohitaji kutoa elimu.

Alisema baadhi ya viongozi huwachukulia wasaidizi wa kisheria kama adui kwa kuhofiwa kuingiliwa majukumu yao hivyo aliomba jamii kutambua umuhimu wao na kuielimisha jamii kuhusiana na masuala mbalimbali ya sheria.





# Walimu wezi wa mitihani waonywa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI leo wanafunzi wa darasa la saba wakitarajia kuanza mtihani wao wa mwisho wa kuhitimu elimu ya msingi, walimu wametakiwa kuwa waaminifu katika usimamizi ili kuondokana na udanganyifu (uvujishaji) wa mtihani.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu nchini (CWT), Mwalimu Deus Seif, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mtihani wa darasa la saba.

Alisema walimu wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mtihani huo unafanyika katika hali ya uaminifu wa hali ya juu ili wanafunzi kila mmoja afaulu kutokana na uwezo wake na siyo njia ya udanganyifu.

"Walimu tunatakiwa kufanya uaminifu wetu kwa asilimia kubwa sana ili kuzuia vitendo vyote vya udanganyifu ambavyo vitafanyika katika mtihani huu unaoanza nchini kote kesho (leo)," alisema Seif.

Alisema walimu wanatakiwa kuwa waaminifu ili kurejesha imani iliyokuwapo ya kusimamia bila ya kuwapo na mgambo wala Jeshi la Polisi.

"Natamani sana hali ya usimamizi wa mitihani irudi kama ilivyo kuwa zamani, uaminifu ulikuwa katika hali ya juu sana walimu tulisimamia mitihani sisi wenyewe, lakini hivi sasa tumepewa mgambo hali ikiendelea hivi siku moja tutalindwa na vifaru vya kivita," alisema.

Alisema pamoja na kuwa CWT ni kwa ajili ya kuwatetea walimu, lakini kwa yule ambaye atashiriki katika vitendo vya udaganyifu atakumbana na mkono wa sheria hivyo ni lazima wakatimize wajibu wao.

"CWT ni kwa ajili ya kuwatetea walimu, lakini ili kuondoa adha ya kutumia gharama katika kuwatetea watakao jiingiza katika vitendo vya udanganyifu wa mitihani, ipo haja sasa kutimiza wajibu ili kukisaidia chama chetu kuondokana na usumbufu," alisema.

Alizitaka shule binafsi kuacha tabia ya kununua mitihani na kuwapatia majibu wanafunzi wao kwa kuwa hali hiyo inashusha hadhi yao.

Katibu mkuu huyo alizitaka mamlaka husika za serikali ambazo zinahusika na mtihani huo kutimiza majukumu yake ili kuondoa usumbufu utajitokeza kwa walimu.

"Ni imani yangu kuwa serikali imejipanga na yale malalamiko ya walimu pia hayatakuwapo wakati huu kama ambavyo imekuwa kipindi kilichopita, Tamisemi pamoja na Baraza la Mitihani najua wamejipanga kuwezesha mtihani huu muhimu wa darasa la saba," alisema Seif.



Wajane kutoka jumuiya ya kikristo Tanzania na nchi jirani ya Kenya, Zambia, Uganda, Malawi na Congo DRC, wakimsikiliza Askofu wa Kanisa la Mennonete Dayosisi ya Kati, Amos Muhagachi (hayupo pichani), wakati akifungua kongamano la tisa la kitaifa la kuwawezesha wajane, lililofanyika Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Mabalozi 20 wa watoto wachaguliwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

JUMLA ya mabalozi 20 wa watoto wamechaguliwa kutoka Wilaya ya Chamwino mkoani hapa na watakuwa na jukumu la kusaidia watoto kufikia mifumo ya ulinzi na kusaidia uharakishaji wa rufani za kesi za ukatili dhidi ya watoto.

Hayo yalibainika juzi wakati wa kikao cha majadiliano katika mradi wa Sauti Yangu unaotekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la Woman Wake Up (Wowap), ambalo hujishughulisha na ushawishi na utetezi hasa wanawake na watoto kilichofanyika wilayani hapa.

Akizungumza kwenye kikao cha majadiliano, Mratibu wa Wowap, Nasra Suleiman, alisema jumla ya mabalozi 20 wa kutetea haki za watoto kutoka Wilaya ya Chamwino, wamechaguliwa kwa lengo la kuwasaidia kufikia uharakishwaji wa rufani za kesi za ukatili dhidi ya watoto.

Alisema mabalozi ni mchanganyiko wa jinsi na wanatoka katika vijiji vitano vya kata ya Manchali iliyopo wilayani hapo.

Alivitaja vijiji hivyo wanapotoka mabalozi hao kuwa Manchali A, Manchali B, Chalinze, Wilunze na Bwawani.

Hata hivyo, Suleiman alisema watasaidiana na watendaji pamoja na wanajamii ambao wako huko kuanzia ngazi ya vitongoji hadi wilaya kwa ajili ya kujitolea kuwa wawakilishi wa watoto katika utetezi wa haki zao.

Alisema mabalozi hao watakuwa na majukumu mbalimbali ikiwamo kuwa daraja la kusaidia watoto kufikia mifumo ya ulinzi pamoja na kusaidia uharakishaji wa rufani za kesi za ukatili dhidi ya watoto.

Pia kuhamasisha watoto kutekeleza masuala na majukumu yanayohusiana na watoto kufikia malengo ya mradi, kutoa elimu kwa wasimamizi wa ulinzi wa mtoto kuhusu masuala yote yanayohusu haki za watoto.

Pia watakuwa na jukumu la kuhimiza uwajibikaji wa watendaji na jamii katika ulinzi wa mtoto sehemu wanazohudumu na kuandaa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili kwa watoto.

Aliongeza kuwa mradi wa Sauti Yangu ulianzishwa kutokana na maamuzi ya Umoja wa Mataifa ya kutokomeza ukatili dhidi ya watoto.

Alisema watoto wamekuwa wakifanyiwa ukatili katika mazingira mbalimbali ikiwamo ndani ya familia na mazingira ya nyumbani.

Ukatili mwingine umekuwa ukifanyika shuleni na katika mazingira ya kutolea elimu na taasisi ya malezi na mahakamani.

"Sauti yangu imeanzishwa kwa imani kwamba kupunguza ukatili dhidi ya watoto ni jambo linalowezekana kwa kiasi fulani hususani kwa kuwashinikiza viongozi wawajibike katika kutimiza wajibu wa jukumu lao la kuwalinda watoto," alisema.

Naye mmoja wa mabalozi hao, Burton Bwanamzuri ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Manchali B, alisema baadhi ya vitendo vya ukatili vimekuwa haviripotiwi kwa hofu ya kuharibu undugu au ujirani.

Kwa uapande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya ya Chamwino, Jane Chalamila, aliitaka jamii kuwa karibu na watoto ili waweze kutoa taarifa za ukatili wanaofanyiwa.

# Serikali yaonya mila zinazonyanyasa wajane

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, amesema mila na dini zisizo na hitilafu haziwezi kuruhusu wajane kunyanyaswa katika jamii.

Dk. Jingu aliyasema hayo jijini Dodoma kwenye kongamano la tisa la wajane lilioandaliwa na Taasisi ya 'Amazing Grace' la kuwajengea uwezo wajane ili waweze kupambana na changamoto mbalimbali katika jamii.

Alisema jamii ina wajibu wa kumlinda mjane na vitendo vyote vya unyanyasaji dhidi yake kwa kuwa hata vitabu vya dini vimeipa jamii jukumu hilo la kuwasaidia na kuwalinda wajane dhidi ya unyanyasaji wowote.

Dk. Jingu alifafanua kuwa hakuna mila wala dini zilizo nzuri zinazoruhusu wajane kunyanyaswa, kunyang'anywa nyumba zao na kudhulumiwa haki zao za msingi kama ardhi, nyumba, magari na mali nyingine na hata wakati mwingine kunyang'anywa watoto.

"Hakuna mila inayosema mjane apokonywe vitu alivyochuma na mwenzi wake hiyo dhana potofu iliojengeka machoni mwa jamii," alisema Dk. Jingu.

Alisema kuwa wajane ni kundi maalum katika jamii ambalo serikali, jamii na mtu mmoja mmoja tuna wajibu wa kuwalinda na hivyo serikali imejizatiti katika kuwasaidia wajane kutatua changamoto zinazowakabili.

Dk. Jingu aliainisha mambo yanayopaswa kuwasaidia ni utoaji wa elimu bure na watoto wengi ambao ni yatima kutoka familia za wajane wamepata fursa ya elimu ya msingi, sekondari na hata kufikia vyuo vikuu, uwapo wa mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi inayosaidia kuwapa wajane mikopo inayowawezesha kujikwamua.

"Hakuna mila wala dini inayoruhusu wajane wanyanyaswe ila kama zipo basi zitakuwa na hitilafu na hazifai katika jamii hivyo zinapaswa kuangaliwa," alisema Dk. Jingu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Amazing Grace, Paulo Mwanga, alitoa wito kwa jamii kuacha kuwafanyia wajane vitendo vya kikatili vya uonevu ili waweze kuishi kwa kuwa mama mjane akipoteza amani jamii nzima inakosa.

"Na tutakuwa na familia legelege kiuchumi, kijamii na kiutamaduni maana wajane ni sehemu ya jamii ambayo ni nguvu kazi ya jamii na wanatakiwa kutendewa haki ili kujenga taifa imara," alisema.

Kwa upande wake Beatrice Muinuka kutoka Mkoa wa Mbeya, ambaye ni mjane alisema kongamano hilo limewasaidia kutambua haki zao kama wajane na wanaishukuru serikali kwa hatua mbalimbali ikiwamo fursa katika maeneo yao ya kupata mikopo itakayowawezesha kujikwamua kiuchumi na kuendesha maisha yao.



HABARI ZANZIBAR

# Ikulu Zanzibar kusomesha zaidi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar, itaongeza nafasi za masomo kwa wanafunzi bora wa kidato cha sita wanaodhaminiwa na serikali.

Mwaka jana ilitoa nafasi 30 na kwamba mwaka huu zimeongezwa hadi 60 na wanufaika ni wanafunzi bora wa kidato cha sita wenye viwango vya juu vya ufaulu.

Akizungumza Ikulu katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi bora wa kidato cha nne na cha sita waliofanya vizuri katika mitihani ya taifa, Rais wa Zanzibar Ali Mohamed Shein, alisema idadi hiyo aliyoiongeza mwaka huu ni mara mbili ya nafasi za ufadhili wa masomo ambazo alizitoa mwaka jana kwa wanafunzi bora wa kidato cha sita.

Dk. Shein alieleza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na utaratibu wa kuwapa udhamini wanafunzi bora wenye viwango vya juu vya kufaulu kwa masomo ya sayansi na sanaa.

Alisema kuwa mwaka huu ameongeza nafasi hadi kufikia 60 badala ya 30 za mwaka jana kwani aliahidi kuendeleza utaratibu huo ili kupata wataalamu wa fani mbali mbali watakaoendelea na masomo yao ndani na nje ya nchi.

Rais Shein alisema: "Pia natoa pongezi kwa wanafunzi 187 waliofaulu kwa daraja la kwanza katika mtihani wa kidato cha nne mwaka jana pamoja na shule bora 10 ambazo ufaulu wa mwaka jana ulikuwa ni wanafunzi 135."

Aidha, aliwapongeza wanafunzi wote 188 wa kidato cha sita hasa vijana wanne waliofaulu kwa alama nne kila mmoja na kuonyesha uwezo mkubwa walionao.

Dk. Shein alieleza kuwa kwa mara nyingine tena wanafunzi wa kike wameonyesha uwezo mkubwa wa kufanya vyema katika mitihani ya taifa na hasa kwa masomo ya sayansi na kuwapongeza wanafunzi hao.

"Wazee walisema mcheza kwao, hutunzwa na chanda chema, huvikwa pete. Kauli zote hizo za wazee wetu zinasibu kwenu. Kwa hivyo, tumeamua kuwaandalia hafla hii kwa ajili ya kuwaenzi kwa sababu mmecheza vyema kwa ajili yenu na kwa ajili ya nchi yenu," alisema Dk. Shein.

Kadhalika aliwataka walimu wasiozingatia vyema majukumu yao na kuyakiuka maadili ya ualimu wajirekebishe kwani kazi hiyo ni ya watu wenye heshima kubwa katika jamii.

Aidha, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alieleza mafanikio yaliopatikana katika sekta ya elimu na kutumia fursa hiyo kutoa pongezi za pekee kwa Rais Dk. Shein kwa juhudi zake za makusudi za kuimarisha sekta ya elimu hapa nchini.

Waziri Pembe alieleza kuwa Rais Shein anaendeleza nyayo za waasisi wa taifa Mzee Abeid Karume pamoja na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere za kuimarisha sekta ya elimu na kukuza sekta zote za maendeleo kwa watu wote.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara Dk. Idrisa Muslim Hijja alieleza kuwa mafanikio yote yaliopatikana katika sekta ya elimu ni juhudi za Rais Dk. Shein katika kuhakikisha anaweka mazingira bora kwenye sekta ya elimu.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akitoa hotuba ya uzinduzi wa mpango shirikishi wa kutokomeza kipindupindu Zanzibar katika hafla iliyofanyika Vuga Mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wapewa maagizo maalumu kisiasa

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amewahimiza wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi.

Aidha, amewaonya kuacha tabia ya kuwapigia kampeni wanaume kwa ajili ya kugombea nafasi hizo bali nao wajitose na kujipigia debe.

Mgeni alisema hayo kwenye viwanja vya Mzalendo huko Magomeni wakati wa mkutano wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwakani.

Alisema bado ushiriki wa wanawake katika uongozi na kwenye vyombo vya kutunga sheria kama Bunge na baraza ni mdogo sana hata katika majimbo ya uchaguzi.

Alisema katika majimbo ya uchaguzi 55 ni wanawake watano pekee waliogombea nafasi ya uwakilishi Zanzibar.

Aidha, kwa upande wa nafasi ya ubunge, ni wanawake watatu walioshinda na kuongoza majimbo ya uchaguzi kwa upande wa Zanzibar.

"Bado uwakilishi wa wanawake katika kugombea nafasi za uongozi ni mdogo sana ambapo nafasi zote tumekuwa tukiwaachia wanaume," alisema Juma.

Alisema yapo mafanikio makubwa katika Baraza la Wawakilishi ambapo baadhi ya kamati za baraza hilo zinaongozwa na wanawake kwa mafanikio makubwa.

"Tunazo kamati tatu za Baraza la Wawakilishi zinazoshikiliwa na wanawake ambao wameonyesha uwazi na ujasiri mkubwa katika kufuatilia mambo mbalimbali katika wizara na taasisi zake," alisema Juma.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA), Profesa Issa Haji Ziddy, aliwataka wanawake kuwa mstari wa mbele kugombea nafasi za uongozi na hakuna vikwazo kwa dini ya Kiislamu kuwazuia wanawake kuwa viongozi.

Alisema hata katika zama za mitume walikuwapo wanawake mashujaa ambao wametajwa kuwa ni watukufu kutokana na kazi kubwa katika kuipigania dini na masuala ya maendeleo.

Aliwataka baadhi ya watu kuacha kuzitumia vibaya aya za Qu'ran kwa kuzitafsiri kwa malengo na madhumuni yao.

"Ipo Suratul Nisaa aya ya 34 ambayo inatafsiriwa wanaume ni viongozi wa wanawake, wakati tafsiri sahihi ni wanaume ni wasimamizi wa wanawake," alisema Profesa Ziddy.

Baadhi ya wanawake walikiri kuwapo kwa vikwazo na vitisho dhidi ya waume zao wakati wanapoonyesha nia ya kutaka kushiriki katika uongozi ikiwamo tishio la talaka.

"Wanaume wengi wanatumia silaha ya talaka kama vitisho na vikwazo katika kushiriki harakati za kisiasa," alisema Ziddy.

# Utoroshaji maliasili kiholela wapata dawa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuwapo kwa kanuni bora za sheria za wanyama na miti asilia kutasaidia kupunguza usafirishaji haramu wa rasilimali hizo nje.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, wakati aliposhiriki mkutano wa kuweka kanuni za sheria kuhusu udhibiti wa usafirishaji wa wanyama asilia na miti nje ya nchi.

Alisema lengo la kuweka kanuni hizo si kuzuia moja kwa moja biashara ya aina hiyo, lakini ni kuweka mwongozo utakaosaidia udhibiti wake.

Alieleza kuwa sheria na kanuni kama hizo zipo kwa upande wa Tanzania Bara ambazo zimesaidia kudhibiti wanyama wakiwamo walio katika hatari ya kutoweka.

"Kanuni za udhibiti wa wanyama pamoja na miti ni muhimu ili kuona rasilimali hizo zinalindwa kwa mujibu wa sheria na kuepuka kutoweka ," alisema Mjawiri.

Mkurugenzi wa Idara ya Maliasili na Mali Zisizorejesheka, Soud Mohamed, alisema katika siku za hivi karibuni kumejitokeza matukio mbalimbali ya kutaka kusafirisha miti maarufu nje ya nchi.

Aliitaja miti ambayo ilikuwa ikitaka kutoroshwa kuwa ni mibuyu iliyokusudiwa kupelekwa nje ya nchi kwa matumizi mbalimbali.

"Tumezuia usafirishaji wa mibuyu kwa sababu ya hofu ya kutoweka kwa miti hiyo hadi hapo uchunguzi zaidi utakapofanyika," alisema Mjawiri.

Alisema udhibiti wa miti na wanyama unafanyika kwa mujibu wa sheria Namba 10 ya mwaka 1996 ambayo mikakati yake ni kulinda rasilimali za taifa kiholela.

Baadhi ya wanyama wanaochukuliwa na kusafirishwa kinyume na sheria ni pamoja na kobe na kima punju ambao hawapatikani kokote duniani isipokuwa Zanzibar.

# Kituo kuwezesha wananchi ufugaji wa asali kibiashara

**Na Idda Mushi,** MVOMERO

BALOZI wa Ubeljiji nchini, Petter Van Acker, amezindua kituo cha ukusanyaji wa asali katika kijiji cha Madizini, Turiani wilayani Mvomero mkoani Morogoro kinacholenga kuwasaidia wananchi kufuga nyuki kitaalamu na kibiashara.

Kadhalika lengo lake ni kutunza mazingira yanayowazunguka .

Balozi huyo alizindua kituo hicho kilichojengwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha AFD Aden Leuven cha Ubeljiji, waliokusanya michango ya wadau na kusimamia ujenzi wake kwa uratibu wa mwenyeji wao, Chuo Kikuu cha Mzumbe kupitia mradi wa Vliruous unaofadhiliwa na nchi hiyo katika utekelezaji wake wa awamu ya nne, huku serikali ya kijiji cha Madizini kilipojengwa kituo hicho, ikitoa eneo la hekari moja kuwezesha kujengwa kituo hicho.

Kiongozi huyo aliwahimiza wananchi wa Mvomero hususani wafugaji nyuki, kukitumia kwa kufanya mabadiliko ya kuondokana na umaskini kwa kuongeza uzalishaji wa asali kutoka lita 300 wanazozalisha kufikisha tani 10 kwa mwaka.

Mkuu wa kitivo cha Biashara cha Chuo Kikuu Mzumbe na kiongozi wa mradi namba nne wa kukuza maendeleo ya ujasiriamali kupitia shughuli jumuishi za kijamii, Dk. Hawa Tundui, alisema nia ya mradi huo ni kisaidia jamii kupitia njia za kitaaluma kuboresha shughuli za kibiashara na kuchangia maendeleo ya taifa kwa kuboresha mnyororo wa thamani wa uchumi wa wananchi wa vijijini.

Alisema lengo ni kuangazia zaidi rasilimali za misitu, na kwamba kituo hicho kitaendeshwa na ushirika wa wafuga nyuki wa Mvomero kwa kushirikiana na washirika wengine kuhakikisha kinaleta tija kwa wananchi kama inavyokusudiwa.

Mratibu wa Mradi huo, Prof. Arbogast Msambila, alisema uwapo wa kituo hicho ni matokeo ya utafiti uliolenga kuunganisha na shughuli za kijamii kwa kuwahusisha wananchi katika mazingira yao na kwamba wamelenga kukusanya asali, kudhibiti ubora na kutafuta masoko ya pamoja.

Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Dk. Eliza Mwakasangula, alisema kituo hicho ni njia ya kuwashirikisha wanajamii kivitendo kuelekea uchumi wa kati wa viwanda kwani asali ni malighafi inayohitajika sana katika ukuaji wa viwanda.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akipita jirani ya shimo kubwa lililopo katika Barabara ya Mtaa wa Libya, jijini humo jana, ambalo ni hatari kwa waenda kwa miguu na vyombo vya moto. **PICHA: JOHN BADI**.

# Upelelezi anayedaiwa kuua mke kwa kumchoma wanukia

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya mauaji inayomkabili Khamis Luwongo maarufu Meshack (38), umedai kuwa upelelezi wa kesi hiyo uko kwenye hatua za mwisho kukamilika na kwamba wanatarajia kuwasilisha nyaraka zinazohusu kesi hiyo.

Meshack anakabiliwa na tuhuma za kumuua mkewe wake kwa kumchoma moto Naomi Marijani.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai upelelezi umefikia hatua ya mwisho kukamilika na wanatarajia kuwasilisha nyaraka muhimu za kesi hiyo kwa ajili ya kuihamishia Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Mshtakiwa aliomba Mahakama kuamuru upande wa Jamhuri umpatie hati ya mashtaka.

Hakimu alikubali ombi lake na aliipanga kesi hiyo kutajwa Septemba 24, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, mshtakiwa anatuhumiwa kwa kosa moja la mauaji kinyume cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu namba 196 sura 16 kama kilichofanyiwa marejeo mwaka 2000.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba 4 ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwongo ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimuua Naomi Marijani.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji mpaka upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu.

# Zaidi ya 800 waelimishwa majukumu mapya ya TBS

**Na Mwandishi Wetu,** KILOLO

ZAIDI ya wanawake na vijana 800 katika Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, wameelimishwa jinsi Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linavyotekeleza majukumu mapya ambayo awali yalikuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

Wananchi hao walipatiwa elimu hiyo kupitia kongamano la siku mbili lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na wilaya na kudhaminiwa na TBS. Kongamano hilo la siku mbili lilianza Septemba 4 na kumalizika Septemba 5, mwaka huu.

Akitoa elimu kwa washiriki wa kongamano hilo kuhusiana na mabadiliko hayo, Ofisa Uhusiano wa TBS, Neema Mtemvu, alisema TBS inatekeleza majukumu hayo kufuatia mabadiliko ya sheria ya fedha ya mwaka 2019 ambayo yameleta mabadiliko katika sheria ya viwango Na: 2 ya mwaka 2009.

Kutokana na mabadiliko hayo, Mtemvu alisema majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi yanafanywa na TBS.

Alitaja huduma zinazotolewa na shirika hilo ni pamoja na usajili wa jengo, kusimamia masuala ya usalama na ubora wa chakula na vipodozi na upimaji wa bidhaa za vyakula na vipodozi kwa lengo la kudhibiti ubora.

Wakati huo huo, maofisa wa shirika hilo walitoa elimu ya viwango kwa washiriki wa kongamano hilo miongoni mwao wakiwa ni wajasiriamali.

Akizungumza wakati wa kutoa mafunzo hayo kupitia kongamano hilo, Mtemvu, alitoa wito kwa wajasiriamali kutumia fursa ya huduma ya bure ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ambayo inatolewa na shirika hilo, ili kuwainua wajasiriamali na hatimaye kuweza kushindana na kuuza bidhaa zao katika masoko ya ndani na nje ya nchi bila vikwazo vya kibiashara.

Alisema kinachotakiwa ni mjasiriamali kupata barua ya utambulisho kutoka Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) na akipeleka TBS mchakato wa kumthibitishia ubora bidhaa zake unaanza mara moja.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ali Hapi, alitoa wito kwa wajasiriamali kujiajiri na hatimaye kuwa wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda vikubwa, hivyo kusaidia kutoa ajira kwa Watanzania.

Hapi alifafanua kwamba serikali peke yake haiwezi kuajiri wananchi wote, hivyo alitoa wito kwa washiriki wa kongamano hilo kuchangamkia fursa za kujiajiri.

## HABARI KIMATAIFA

# Waliohusika na mauaji ya jasusi kukamatwa

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MAHAKAMA ya Afrika Kusini imetoa waranti za kukamatwa kwa wahusika wakuu wa mauaji ya aliyekuwa mkuu wa Idara ya Ujasusi nchini Rwanda, Patrick Karegeya.

Ismael Gafaranga na Alex Sugira wanashukiwa na mahakama nchini Afrika Kusini kushiriki katika mauaji ya Mkuu wa zamani wa idara ya ujasusi nchini Rwanda mwaka 2014.

Karegeya aliuawa baada ya kudaiwa uhusiano na Rais Paul Kagame kuwa mbaya.

Waranti hizo zinatolewa dhidi yao baada ya miaka mitano ya kesi hiyo mahakamani.

Januari 1, 2014, Patrick Karegeya alikutwa amefariki dunia kwenye chumba chake cha hoteli mjini Johannesburg.

Tangu mwanzo wa uchunguzi, mahakama nchini Afrika Kusini ilitambua haraka watuhumiwa wanne ambao wana uhusiano na serikali ya Rais Paul Kagame.

Ili kuepusha mzozo wa kidiplomasia kati ya nchi hizi mbili, ofisi ya mwendesha mashtaka ilikataa kuendelea na mashtaka dhidi ya watuhumiwa hao na hivyo kesi hiyo kusitishwa.

Kwa upande wa David Batenga, mpwa wa Patrick Karegeya, kutolewa kwa waranti hiyo amesema ni ushindi wa kwanza.

"Tumesubiri muda mrefu sana. Tutaendelea kupambana ili wauaji warejeshwe kutoka katika nchi yetu. Hatutochoka na kwa bahati nzuri tunaishi katika nchi yenye sheria. Sio Rwanda. Kwa hivyo baadhi ya vizingiti vitachelewesha mahakama kufanya kazi yake, lakini tunajua kuwa haraka sana au baadaye, ukweli utajulikana na tutatendewa haki," alisema Batenga.

Gihanna Kennedy, mmoja wa mawakili wa familia, alisema anaimani kuwa mahakama itatekeleza majukumu yake, lakini haamini kuwa washukiwa watarejeshwa nchini Afrika kusini.

"Kwa kweli tunajua kuwa serikali ya Rwanda haitokubali kuwasafirisha wanajeshi waje kwenda katika kesi katika nchi ya kigeni. Hata hivyo Afrika Kusini inaweza kuomba polisi ya kimataifa, Interpol, kuwakamata watu hao. Huu ni ujumbe muhimu, uliotumwa na mahakama huru ya nchi huru," alisema mmoja wa mawakili wa familia ya Patrick Karegeya.

Karegeya alikuwa Mkuu wa zamani wa ujasusi nchini Rwanda na alikutwa amenyongwa katika hoteli moja mjini Johannesburg, Afrika Kusini.

Karegeya alikuwa mshirika wa karibu sana wa Kagame kabla ya kutofautiana naye. **RFI**

# Mwili wa Mugabe kuagwa maeneo matatu tofauti

**HARARE,** Zimbabwe

WAZIRI wa Habari wa Zimbabwe, Monica Mutsvangwa, amesema mwili wa Rais wa zamani wa taifa hilo, Robert Mugabe utalazwa katika sehemu tatu tofauti mjini Harare kwa ajili ya kupewa heshima ya kitaifa kabla ya kuzikwa siku ya Jumapili.

Mugabe, kiongozi wa zamani wa Zimbabwe aliyeiongoza nchi hiyo kwa miaka 37, alifariki Ijumaa katika hospitali moja nchini Singapore alikokuwa akipata matibabu.

**Mugabe, kiongozi wa zamani wa Zimbabwe aliyeiongoza nchi hiyo kwa miaka 37.**



Alikuwa na umri wa miaka 95. Mutsvangwa alieleza kuwa mwili wa muasisi wa taifa hilo utalazwa katika Uwanja wa michezo wa Rufaro uliopo mjini Harare siku ya Alhamisi na Ijumaa kwenye Uwanja wa michezo wa kitaifa, na siku ya Jumamosi mwili wa kiongozi huyo utalazwa katika Ikulu.

Hata hivyo, waziri huyo wa habari alifahamisha tu kwamba marehemu Mugabe atazikwa siku ya Jumapili lakini hakutaja mahala ambapo maziko yatafanyika hali ambayo inaudhihirisha uvumi kwamba kuna hali ya kutokukubaliana kati ya familia ya Mugabe na serikali juu ya mahala atakapozikwa Rais huyo wa zamani wa Zimbabwe. **DW**



Rasi wa Kenya, Uhuru Kenyatta (kulia), akiwa na Makamu wake William Ruto. **PICHA: AFP**

# Mpasuko wanukia chama cha Jubilee

**NAIROBI,** Kenya

WABUNGE wanaomuunga mkono Makamu wa Rais wa Kenya, William Ruto, wanamtaka Rais Uhuru Kenyatta kujitokeza hadharani na kuelezea jinsi wanavyodhulumiwa na vyombo vya dola.

Hayo yanajiri ikiwa imepita siku moja tu baada ya mbunge mmoja kutiwa nguvuni kwa kuzuia hafla ya mchango kanisani katika jimbo lake la uchaguzi analoliwakilisha bungeni.

Wabunge hao wanadai kuwa hizo ni njama za kuwanyamazisha wasiiunge mkono azma ya Ruto kuwania kiti cha urais katika uchaguzi mkuu ujao.

Kimya cha Rais Kenyatta kuhusu matukio yanayokizonga chama tawala cha Jubilee, kinatishia kukipasua na kukisambaratisha chama hicho huku salamu za heri kati yake na kinara wa upinzani Raila Odinga zikileta shari na utengano ndani ya chama badala ya umoja.

Kutiwa nguvuni kwa mbunge wa Jubilee, Ndindi Njoro, baada ya kuvamia hafla ya mchango wa pesa kanisani, uliokuwa ukiongozwa na kundi la Kieleweke siku ya Jumapili, kumeongeza mianya kwenye chama hicho.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema hakitaishi kuona uchaguzi mwingine mkuu, iwapo misuguano itaendelea kushuhudiwa.

Mpasuko wa chama hicho unashuhudiwa katika ngome ya kisiasa ya Rais Uhuru ya Mlima Kenya ambapo pameibuka makundi mawili ya Tangatanga na Kieleweke. Njoro anaegemea upande wa Kieleweke unaomuunga mkono Naibu Rais William Ruto.

Viongozi hao wanaonya kuwa, kimya cha Rais Kenyatta kinathibitisha kuwa ameagiza vyombo vya dola kuwanyamazisha na kuwatisha wanaomuunga mkono Ruto.

Aidha wanataka Rais Kenyatta aelezee msimamo wake kuhusu nani anayemuunga mkono kati ya Raila na Ruto.

Mbunge wa Kandara, Alice Wahome alinukuliwa akidai kuwa baadhi ya wafanyabiashara wenye ushawishi kutoka eneo la Mlima Kenya wamekuwa wakifanya mikutano na vyombo vya dola kujadili jinsi ya kumzuia Ruto kumrithi Rais Kenyatta.

Ndindi Nyoro alifikishwa mahakamani jana na aliachiwa bila ya kushtakiwa. Alipokamatwa huko Murang'a, ghasia zilishuhudiwa kwa muda kabla ya hali kurejea kawaida usiku wa kuamkia jana.

Mapema mwaka huu, wabunge wanaoegemea upande wa Ruto wakiwamo Gavana wa Kiambu, Ferdinand Waititu na Mbunge wa Kikuyu, Kimani Ichung'wa, wote kutoka eneo la Mlima Kenya walinyang'anywa walinzi wao kwa njia ya kutatanisha na kisha baadaye wakarejeshewa. **DW**

# Askari sita kortini kwa tuhuma wizi wa mafuta

Na Hellen Mwango

ASKARI sita wakiwamo polisi watano na mmoja wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi.

Sambamba na tuhuma hizo, askari hao pia wanakabiliwa na mashtaka matatu yakiwamo ya wizi wa mafuta ya ndege lita 2,180 na utakatishaji wa zaidi ya Sh. milioni nne.

Washtakiwa hao ni Koplo Shwahiba (38), Sajenti wa JWTZ, Ally Chibwana (47), Konstebo Elidaima Paranjo (38), Konstebo Simon (28), Konstebo Dickson na Konstebo Hamza.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Victoria Mwaikambo.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Faraji Nguka na Saada Mohammed, ulidai kuwa washtakiwa wote kwa pamoja wakiwa watumishi wa umma walikiuka maadili ya kazi zao na kupanga genge la uhalifu ikiwamo kuiba lita 2,180 za mafuta ya ndege (Jet A-1/Ik) yenye thamani ya Sh. 4,647,760.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kuwa Julai 30, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, askari hao waliiba lita 2,180 za mafuta ya ndege (Jet A-1/Ik) yenye thamani ya Sh. 4,647,760 mali ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa siku na mahali pa tukio la pili, washtakiwa wote kwa pamoja waliiba mafuta hayo na kutakatisha Sh. milioni 4.6 wakati wakijua kuwa fedha hizo ni zao la kosa tangulizi la wizi kinyume cha sheria.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na kwamba baada ya upelelezi itahamishiwa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu kama Mafisadi au Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) atakapotoa kibali cha kusikilizwa na mahakama hiyo.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa Septemba 24, mwaka huu.



Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, akiongea na wahariri toka vyombo mbalimbali vya habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuelimisha wananchi kuhusu kazi zinazofanywa na wakala huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wafungwa miaka 60 kwa ujangili

Na Jumbe Ismailly, MANYONI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida imewahukumu wakazi wawili wa Tarafa ya Itigi,wilayani Manyoni adhabu ya kutumikia kifungo cha jumla ya miaka 60 jela baada ya kuwatia hatiani kwa makosa ya kumiliki nyara za serikali pamoja na kujihusisha na biashara ya nyara.

Waliohukumiwa ni Fale Shija, Migungumalo, mkazi wa Kijiji cha Mitundu na Mashaka Abdala Sudi, mkazi wa Kijiji cha Kalekwa ambao kila mmoja anatumikia adhabu ya kifungo cha miaka 15 kwa kila kosa.

Wakili wa serikali, Petrida Muta, alidai washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka mawili ya kumiliki nyara za serikali na kufanya biashara ya nyara za serikali.

Alidai katika shtaka la kwanza Septemba 22, mwaka 2017 saa 10:40 jioni kwenye maeneo ya Kijiji cha Mtakuja barabara ya kuelekea Mji Ndogo wa Itigi, wilayani Manyoni washtakiwa walikutwa wakimiliki vipande tisa vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilogramu 6.5, baada ya kuuawa tembo watano vyenye thamani ya Sh. 168,675,000 mali ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muta alidai katika shitaka la pili Septemba, 22, 2017 saa 10:40 jioni kwenye maeneo ya Kijiji cha Mtakuja, wilayani Manyoni barabara ya kuelekea mji mdogo wa Itigi, washitakiwa walikutwa wakijihusisha na biashara ya kuuza vipande tisa vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilogramu 6.5, vilivyopatikana baada ya kuwekwa mtego kisha kufanikiwa kuwatia mbaroni.

Kesi ya uhujumu uchumi iliyosajiliwa na kupewa namba 53/2017 ilifuguliwa mwaka 2017 ambapo kabla ya hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Manyoni hajatoa hukumu, wakili wa serikali aliiomba Mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa washtakiwa hao.

Kwa mujibu wa wakili huyo, makosa yaliyofanywa na washtakiwa hao yamesababisha kuwapo kwa mauaji mengi ya tembo katika kipindi cha miaka ya nyuma, hivyo kupelekea kupungua kwa wanyanahao, na kwamba tembo wanapopungua hata pato la taifa nalo hupungua.

Muta aliiomba Mahakama hiyo itoe adhabu kwa kuzingatia sheria ili liwe fundisho kwa watu wengine wanaojihusisha na vitendo vya ujangili katika hifadhi za Taifa.

Katika utetezi wake mshtakiwa wa kwanza aliiomba Mahakama hiyo kutompa adhabu kali kwa kuwa alishakaa mahabusu kwa kipindi kirefu, ana mke, watoto na wazazi wanaomtegemea, hivyo anaomba apunguziwe adhabu.

Mshtakiwa wa pili, Mashaka Abdala Sudi hakuwa na utetezi wowote zaidi ya kukana kutenda makosa hayo.

Akitoa hukumu, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Manyoni, Stella Thomasi Kiama, alisema washtakiwa hao wametiwa hatiani kwa makosa yote mawili, hivyo kuwahukumu kifungo cha jumla ya miaka 60 jela, ambapo kila mmoja amehukumia adhabu ya kifungo cha miaka 15 jela kwa kila shtaka.

## Wafanyabiashara 10 wa madini kizimbani

INATOKA UK.5

ambazo walizipata kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa Clever.

Watuhumiwa hawakutakiwa kujibu lolote kwa vile mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Namkambe alidai haujakamilika na aliwasilisha maombi ya kutaka baada ya kuahilishwa kesi hiyo, Solomon achukuliwe na Jeshi la Polisi kwa ajili ya upelelezi.

Maombi hayo yalisababisha mvutano na wakili wa utetezi Baraka ambaye alidai mteja wake alikamatwa tangu Septemba Mosi, mwaka huu na kusafirishwa hadi Dar es Salaam kwa mahojiano, na muda wote huo alikuwa mikononi mwa polisi, hivyo ni vema apelekwe gerezani na kama watamuhitaji kwa upelelezi wamfuate huko.

Hata hivyo Namkambe alidai ombi lake ni sahihi kwa vile hata kama ni kumfuata huko ni lazima mahakama itoe idhini, hivyo ni busara aruhusiwe kwenda polisi ili kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo kuepuka malalamiko yanayoweza kujitokeza baadaye kuhusu upelelezi kuchelewa kukamilika.

Hakimu Denis Luwongo aliamuru kuruhusu mshtakiwa kuchukuliwa na polisi kwa ajili ya upelelezi na kuahilisha kesi hiyo hadi Septemba 23, mwaka huu.

Kesi ya tatu ambayo ilisomwa mbele ya Hakimu Mkazi Hapness Chuwa iliwahusu watuhumiwa wawili, Everine Bahati na Tyson Jeremiah ambao wamesomewa makosa matatu.

Namkambe alidai katika kosa la kwanza watuhumiwa walikamatwa na dhahabu gramu 33.21 yenye thamani ya Sh. milioni 3 bila kuwa na kibali.

Katika kosa la pili, wanadaiwa kujipatia fedha kwa udanganyifu kwa kuuza madini hayo bila kuwa na kibali.

Wakili Namkambe alidai katika kosa la tatu ni utakatishaji wa fedha Sh. milioni 3 ambazo walijipatia kwa njia ya udanganyifu.

Katika kesi nyingine wafanyabiashara watano wa madini walipandishwa kizimbani chini ya kiapo cha faragha kilichosainiwa na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa (RCO) Mbeya, ambapo serikali imeomba watu hao wawekwe chini ya uangalizi maalum ili wawe na mwenendo mzuri.

Namkambe alidai ombi hilo linatokana na watuhumiwa kufanya makosa mengi ya mara kwa mara.

Baada ya kusomwa kwa maombi hayo, watuhumiwa wote hawakuwa na pingamizi na badala yake wakaomba walegezewe masharti ya dhamana na ndipo hakimu akawaweka chini ya uangalizi kwa kipindi cha miezi 12, ambapo watatakiwa kuripoti kwa wakuu wa polisi wa wilaya mara moja kila mwezi.

Hata hivyo watuhumiwa hao walitakiwa kila mmoja kuwa na mdhamini mmoja atakayesaini bondi ya Sh. milioni 10 ili wapewe dhamana.

Hata hivyo wawili ndio waliotimiza masharti ya dhamana na kuachiwa huru na watatu wamerejeshwa rumande hadi Ijumaa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

REHANI IBRAHIM MADRAI
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Corolla T 444 ANF yenye Chassis namba AE1008019552 na Injini namba, 5AB342630. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi.
MS/TR/RB/1509/2019.

215413902

## KUPOTEA KWA VYETI



Magreth John Kiyabo anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0534-0069 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari St. Anthony's, Cheti cha Kidato cha sita chenye index namba S0204-0633 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Jangwani na Cheti cha Kuzaliwa chenye namba 0006886.

Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: DAR/KIJ/RB/288462/2019

115413402

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI

(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)

Katika Mahakama ya Mwanzo: MJINI - TANGA
Usimamizi wa Mirathi No. 128/2019
Ombi la SULEIMAN AHMED SAID kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **AHMED SAID ALLY**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/09/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 9/9/2019

115412802

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA
MISC CIVIL APPLIC/CASE NO. 33 OF 2019
ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION..........PLAINTIFF
APPLICANT
VERSUS
HAPPINESS KILEO &
OTHERS..................DEFENDANT/RESPONDENT

**NOTICE OF MENTION**

TO: BENSON LYIMO
TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 18 day of SEPTEMBER, 2019 at 8:30 am o'clock in the forenoon. You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE** that in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 05 day of **SEPTEMBER, 2019.**

115412702

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA
MISC CIVIL APPLIC/CASE NO. 33 OF 2019
ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION..........PLAINTIFF
APPLICANT
VERSUS
HAPPINESS KILEO &
OTHERS..................DEFENDANT/RESPONDENT

**NOTICE OF MENTION**

TO: ROBERT SIMON URASSA
TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the 18 day of SEPTEMBER, 2019 at 8:30 am o'clock in the forenoon. You may appear in person or by Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
TAKE FURTHER NOTICE that in default of your appearance on that day time before mention or hearing the Court may proceed in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 05 day of SEPTEMBER, 2019.

115412702

## KUPOTEA KWA CHETI



LIDIA OBERD KUCHAGA ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NO-S0951-0015 KILICHOTOLEWA NA MLOWA BARABARANI SECONDARI MWAKA 2014.

YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. PIA AMEPOTELEWA NA CHETI CHA KUZALIWA. TAARIFA YA POLISI: DOD/DOD/RB/135754/2019.

115413502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FASTJET AIRLINES LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 543 DMX TOYOTA TOWNACE NOAH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/OST/RB/283078/2019.**

115412502

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11
(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)

**Katika Mahakama ya Mwanzo MBALAMO**

**Usimamizi wa mirathi 57/2019**

**Ombi la YVONNE FRANCIS MBAULA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu GERALD SERAFINI BALUA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 20/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 3/09/2019

115412602

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA
SHAURI NA. 168 LA 2019
MASHAKA SAMSON.................MUOMBAJI
DHIDI YA

1. OBED ENOCK
2. ALLY FRANCIS MAKOS ...........WADAIWA

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: OBED ENOCK**

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 16/10/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Tanzania, kitengo cha Biashara.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 03/09/2019.

115412002

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA
SHAURI NA. 508 LA 2018
THOMAS CHUBWA KAPESA.........MUOMBAJI
DHIDI YA

1. NKYA COMPANY LIMITED
2. ACCESS BANK TANZANIA LTD .......WADAIWA

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: NKYA COMPANY LIMITED**

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 20/09/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 27/08/2019.

115412102

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA
SHAURI NA. 39 LA 2019
JOSHUA MADAHA.......................MUOMBAJI
DHIDI YA

1. CRDB BANK PLC
2. MEM AUCTIONEERS AND ...........WADAIWA GENERAL BROKERS
3. HANIFA HUSSEIN ABEID


**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: HANIFA HUSSEIN ABEID**

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 25/09/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Tanzania, kitengo cha Biashara.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 29/07/2019.

115411902

## KUPOTEA KWA CHETI



**ATHANAS EDWARD KUSENHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0138-0053** kilichotolewa na MPWAPWA SEKONDARI November, 2002. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **LIN/LIN/RB/269605/2019.**

115411802


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# CARROLL KUIKOSA LIVER

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Newcastle, Andy Carroll, ataukosa mchezo dhidi ya Liverpool Jumamosi hii wakati akiendelea kujiuguza kutokana na kufanyiwa operesheni ya 'enka'.

Nyota huyo alikuwa na matumaini ya kucheza kwenye mchezo huo baada ya kusajiliwa akiwa mchezaji huru katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili la England.

Lakini tangu kutua klabuni hapo bado hajaweza kufanya mazoezi na kikosi cha kwanza na kwa vyovyote hatakuwapo kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, klabu ambayo ajiunga nao akitokea Newcastle kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 35 mwaka 2011.

Carroll amekuwa akifanya mazoezi ya daktari wa mazoezi wa klabu hiyo, licha ya kwamba kocha, Steve Bruce anaamini kuwa atarudi uwanjani haraka.

"Sidhani kama ataweza kucheza kwenye mchezo wa Jumamosi, kwani bado anaendelea kujiuguza," alisema kocha Bruce.

Hata hivyo, kuna uwezekano Carroll atakuwa kwenye mchezo dhidi ya Leicester mwishoni mwa mwezi huu.

# Sarri alizuia uhamisho wa Costa

**TURIN,** Italia

KLABU ya Manchester United ilikuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili Douglas Costa, lakini kocha wa Juventus, Maurizio Sarri alikataa kumuuza kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Winga huyo wa kimataifa wa Brazil, Costa, alipata majeruhi msimu uliopita na hivyo kumfanya kukosa mechi nyingi za kucheza, na United ilionekana kutaka kutumia mwanya huo kwa ajili ya kumsajili ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Hata hivyo, Sarri ambaye alihamia pale Turin kipindi cha majira ya joto kutoka Chelsea baada ta kuchukua nafasi ya Massimiliano Allegri – alizuia uhamisho huo.

Giovanni Branchini aliyempeleka Costa Juventus ameliambia gazeti la Daily Mail: "Kiukweli Allegri na Sarri hawakuwahi kufikiria kumuachia aondoke.

"Manchester United walikuwa wamejidhatiti kutaka kumsajili, klabu hiyo mara zote ilikuwa inataka kumsajili nyota huyo wa Brazil.

"Haikuwa klabu moja pekee iliyokuwa inataka kumsajili Douglas Costa."


Costa sasa amepona majeruhi yake na ameanza vizuri msimu huu chini ya kocha Sarri kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati Juventus ikitafuta kubeba taji lake la tisa mfululizo la ligi kuu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ametoa pasi za mwisho mbili za mabao msimu huu, wakati Juventus ikiwa na mwanzo mzuri kwenye ligi hiyo.

Branchini aliongeza: "Alikuwa na matatizo ya majeruhi mara kwa mara, msimu uliopita alikuwa anaumia mara kwa mara. Lakini alitaka kupona haraka na ameweza kurudi uwanjani.

"Juventus hakuwa na mpango kabisa wa kumuuza, licha ya kwamba, Man United walimtaka kwa udi na uvumba."



# *Xhaka: Bado sijapona nacheza na maumivu*

**GENEVA,** Uswisi

GRANIT Xhaka amebainisha kwamba ameanza msimu huu akicheza huku akiwa na maumivu ya kisigino, wakati nahodha huyo wa Uswisi akiwa sehemu ya kikosi cha nchi yake kilichioibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Gibraltar.

Kiungo huyo wa Arsenal amekuwa akishutumiwa na mashabiki wa washikabundi hao kutoka na kiwango hake msimu huu, lakini mchezaji huyo mwenye umri w amiaka 26 amebainisha kwamba bado hajapona na kuwa fiti.

Akizungumza baada ya mchezo wa ushindi wa Jumapili, ambapo alitolewa dakika ya 74, alisema: "Nimekuwa na maumivu ya kisigino kwa zaidi ya wiki kadhaa sasa. Huwa najisikia maumivu nikiwa mchezoni.

"Inaniumiza, lakini naamini kuna wakati itakuwa poa."

Xhaka ameshindwa kuwashawishi mashabiki wa Arsenal ambao wamekuwa kimtaka kocha Unai Emery kutomchezesha kwenye safu ya kiungo.

Pia Xhaka alishutumiwa kwa kiwango kibovu na kusababisha penalti, wakati Arsenal ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Tottenham Jumapili iliyopita.

# Nabil aelezea kutosajiliwa Liverpool

**PARIS,** Ufaransa

NABIL Fekir amesissitiza kwamba, madai ya uhamisho wake kukwama kwenda Liverpool kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2018 kwa sababu kutofuzu vipimo vya afya 'yalikuwa ya uongo' na kwamba goti lake lilikuwa fiti.

Iliripotiwa kwamba Lyon na Liverpool zilifikia makubaliano ya uhamisho wa usajili wake kuwa pauni milioni 53 na tayari Mfaransa huyo alifanya mahojiano ya kukaribishwa na televisheni ya Liverpool kabla ya dili hilo kutangazwa limeshindikana dakika za mwisho.

Inaaminika kwamba, Liverpool ilijaribu kufanya tena makubaliano mengine baada ya kufanyiwa vipimo vya afya mjini Paris kwani ilionekana goti lake lina matatizo.

Fekir aliumia goti msimu wa 2015-16, lakini tangu hapo aliendelea kucheza bila kuwa na matatizo yoyote.

Na baada ya Liverpool kuachana nae, alijiunga na Real Betis kipindi hiki cha majira ya joto kwa ada ya pauni milioni 22.

Hata hivyo, katika mahojiano na gazeti la L'Equipe, Fekir sasa amedai kwamba hakukuwa na tatizo lolote kwenye goti lake na akasisitiza kuwa hadi sasa hajui kwanini dili hilo la kuhamia pale Anfield lilishindika.

"Uwongo mwingi ulizungumzwa na uliniathiri mimi," alisema. Na hasa kuhusu familia yangu. Iliwaumiza wao na mimi. Hasa ukijua kwamba kila kinachoandikwa ni uwongo.

"Kilichozungumzwa na kuandikwa hakikuwa cha kweli. Goti langu liko vizuri, nilifanyiwa uchugunzi pale Clairefontaine (Kambi ya mazoezi ya timu ya taifa ya Ufaransa) – goti langu halikuwa na matatizo.



# ABRAHAM: MAMA ALILIA MACHOZI NILIPOBAGULIWA



**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abraham amesema mama yake alimwaga machozi baada ya yeye kuonyeshwa ubaguzi wa rangi baada ya fainali ya kombe la Uefa Super.

Abraham alikosa penalti ya mwisho na kuiwezesha Liverpool kuibuka na ushindi kule Istanbul mwezi uliopita na yeye akakumbana na manyanyaso ya kubaguliwa katika mitandao ya kijamii.

"Nakumbuka nilikuwa nazungumza na mama, alionyesha huzuni kubwa, alikuwa analia," amesema nyota huyo mwenye umri wa miaka 21 akiiambia CNN.

Mapema mwanzoni mwa Agosti, golikipa wa Liverpool, Adrian aliidaka penalti ya Abraham na hivyo kuwafanya wekundu hao wa Anfield kupata ushindi wa penalti 5-4 kwenye mchezo huo ambao humkumtanisha bingwa wa Ligi ya mabingwa Ulaya na kombe la Europa.

Abraham, ambaye tangu hapo ameifungia mabao manne Chelsea katika mechi zilizopita, aliongeza: "Kwa uhakika haikuwa hali nzuri, kumuona mtoto akibaguliwa. Mama yangu alikuwa anafikiri kwa nini mimi?"

"Kwangu mimi, nilikuwa imara, haikuniathiri kwa kiasi kikubwa, lakini inawaumiza watu wengine ambao wapo nje ya uwanja.

"Nilikuwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na nikachukua simu yangu ya mkononi baada ya mchezo. Nilikutana na jumbe nyingi za kunikatisha tamaa, lakini nyingine zilikuwa zinaniunga mkono."

# *Ramos anaamini Pobga atatua Madrid*

**MADRID,** Hispania

SERGIO Ramos amepaza sauti kuhusu Paul Pogba na kumtaja kuwa "mmoja wa wachezaji bora" na ana matumaini kiungo huyo wa Manchester United atajiunga nae pale Real Madrid kwa siku zijazo.

Pogba na wakala wake, Mino Raiola, wote walizungumza kipindi cha majira ya joto na kusema kwamba nyota huyo anataka kuondoka Old Trafford kwa ajili ya kutafuta changamoto mpya, lakini United walikataa kumuuza nyota huyo wa Ufaransa.

United ilikataa ofa kutoka Real ya pauni milioni 27.6 pamoja na James Rodriguez kwa ajili ya kumchukua Pogba, ambaye alirudi kwenye Ligi Kuu ya England kutoka Juventus mwaka 2016 kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 89.

"Nafikiri Real Madrid mara zote mlango upo wazi kwa wachezaji wazuri kama yeye," amesema Ramos akiliambia gazeti la Daily Express.

Madrid ilitumia zaidi ya pauni milioni 270 kipindi cha majira ya joto chini ya kocha, Zinedine Zidane kwa ajili ya kuwasajili wachezaji kama Eden Hazard, Luka Jovic, Eder Militao, Rodrygo na Ferland Mendy kwa baadhi yao.


Pogba amecheza mechi nne kwa United za Ligi Kuu msimu huu na nahodha huyo wa Real, Ramos anaamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 atatua kikosini kwao siku moja.

"Kwangu mimi, Pogba ni mmoja wa wachezaji bora kabisa duniani," alisema Ramos.

"Yeye yuko tofauti na ameonesha thamani yake akiwa pale Juventus na sasa Manchester United.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUENDOUZI NA UBORA WA MIAKA 10 ARSENAL

## Inatisha kuwa ndiyo kwanza ana miaka 20 tu, anaweza kuwa katika nafasi ya kiungo...

**LONDON,** England

MATTEO Guendouzi ameonyesha ubora mapema tangu alipotua Arsenal mwaka jana, kwa mujibu wa straika wa zamani wa Tottenham Hotspur, Darren Bent, ambaye ameiona nyota yake iking'ara zaidi kwa kipindi cha miaka 10 ijayo.

**Guendouzi, ambaye alianzia soka lake Paris Saint-Germain akiwa kinda, alitengenezea jina lake Ufaransa na kuonekana zaidi wakati akiichezea Lorient. Na kipindi hicho kiungo huyo alicheza mechi 21 kwenye Ligue 2 msimu wa 2017/18.**

Na baada ya kumtazama kiungo huyo wa kati wa kimataifa wa Ufaransa akionyesha uwezo mkubwa katika ligi hiyo ya Daraja la Pili, Arsenal ilimpandia dau Guendouzi kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni saba.

Licha ya kuwa mgeni kwenye Ligi Kuu England, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, hakuwahi kutazama nje ya nafasi, akimvutia kila wakati kocha na mashabiki kwa mchezo wake.

Na kutokana na uwezo mkubwa aliouonyesha, umemfanya Guendouzi kuitwa timu ya Taifa ya Ufaransa 'Les Bleus' katika mechi za kimataifa zinazoendelea kwa sasa, akichukua nafasi ya Paul Pogba- ambaye anasumbuliwa na majeraha ya kifundo cha mguu kufuatia kuumia kwenye mechi dhidi ya Southampton.

Na Darren Bent, wakati wa mahojiano na Football Insider, alieleza sifa zake kwa Guendouzi kwa kueleza: "Anacheza kama mtu aliyeichezea Arsenal kwa miaka mingi. Inatisha kuwa ndiyo kwanza ana miaka 20 tu, anaweza kuwa katika nafasi ya kiungo ya Arsenal kwa miaka 10 ijayo, ni mzuri katika jukumu hilo."

"Hata anapotoa mpira, anataka kuwa na mpira wakati wote. Kamwe hatetereki katika hilo na hilo ndilo linalotakiwa kwenye idara ya kiungo ambalo huwezi kufundishwa, huwezi kufundisha hilo."

Guendouzi alitarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza katika kikosi cha wakubwa cha Ufaransa jana dhidi ya Albania kwenye dimba la Stade de France.

Baada ya mechi ya kufuzu ya 'Les Bleus' dhidi ya Andorra, Guendouzi atakwea pipa kurejea London kwa majukumu ya klabu tayari kuungana na wachezaji wenzake wa Arsenal kwa safari ya kuelekea kuivaa Watford kwenye mechi ya Ligi Kuu England.

## ZISIKUPITE

### UTD KUMFUATA RICE JANUARI

MANCHESTER United itajiunga katika mbio za kutoa ofa ya pauni milioni 90 kwa kiungo wa West Ham, Muingereza Declan Rice, 20, kwenye dirisha la Januari mwakani. ***(Express)***

### ERIKSEN KIPORO CHA MADRID

REAL Madrid itamrudia kwa mara nyingine kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen, majira ya joto yajayo kama Paul Pogba ataongeza mkataba wake Manchester United. Eriksen, 27, atamaliza mkataba wake mwaka 2020. ***(Sky Sports)***

### CHELSEA YAITA MAWAKALA

CHELSEA imewaeleza mawakala wake kuwa inaamini kifungo chao cha kusajili, ambacho kimewazuia kununua wachezaji majira haya ya joto, kitapunguzwa, hiyo ikiwa na maana wanaweza kununua wachezaji kwa mara nyingine katika dirisha la usajili la Januari. ***(Mirror)***

### RAMOS AMVUTA POGBA REAL

BEKI wa Real Madrid, Sergio Ramos, amemshauri kiungo Paul Pogba, 26, kuondoka Manchester United na kujiunga na miamba hiyo ya Hispania. ***(Express)***

### SARRI AMZUIA COSTA UNITED

JUVENTUS imekataa kumuuza winga Douglas Costa, 28, licha ya kutakiwa sana na Manchester United baada ya kocha wa Juve, Maurizio Sarri kufunga milango ya Mbrazil huyo kuondoka. ***(Mail)***

### CHELSEA KUMFUNGA EMERSON

CHELSEA imefungua meza ya mazungumzo ya mkataba mpya na beki wa pemebeni Mtaliano Emerson, 25. Winga wa England, Callum Hudson-Odoi, 18, pia yupo mbioni kukamilisha mkataba wake mpya wa miaka mitano na klabu hiyo utakaomfanya kulipwa pauni 180,000 kwa wiki. ***(Express)***

### MURIQI AIVUTIA NAPOLI, SPURS

TOTTENHAM ilituma wawakilishi wake kwenda kumtazama straika wa Fenerbahce, Vedat Muriqi, 25, wakati akiichezea Kosovo mwishoni mwa wiki. Mashushushu kutoka Lazio, Fiorentina na Napoli pia walikuwamo wakati Muriqi akiifungia Kosovo kwenye ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Jamhuri ya Czech Republic. ***(Sabah, via Four Four Two)***

### DE GEA KUVUTA KAMA POGBA

KIPA wa Manchester United, David de Gea, 28, yupo mbioni kukubali mkataba mpya utakaomwezesha kulipwa pauni 290,000 kwa wiki kiasi ambacho pia analipwa kiungo wa timu hiyo, Mfaransa Pogba. ***(Guardian)***

### MBAPPE AWINDWA JUVENTUS

Kylian Mbappe, 20, anawindwa na Juventus baada ya miamba hiyo ya Serie A kushindwa kuinasa saini ya mshambuliaji mwenza wa Mfaransa huyo katika klabu ya Paris St-Germain, Mbrazil Neymar, 27, majira haya ya joto. ***(Express)***

### FEKIR AKANA UZUSHI LIVER

KIUNGO mshambuliaji wa Real Betis, Nabil Fekir, 26, amekanusha madai kuwa uhamisho wake wa kwenda Liverpool mwaka 2018 akitokea Lyon ulishindikana kwa sasa ya kutofaulu vipimo vya afya. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

# Zanzibar kuchuja wa Cecafa kesho

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Vijana ya Taifa ya Zanzibar chini ya umri wa miaka 20 inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki kesho, Jumatano dhidi ya timu ya Taifa ya Jang'ombe inayoshiriki Ligi Daraja Kanda, lengo likiwa ni kuitumia mechi hiyo kwa mchujo wa kwanza wa kuwapata wachezaji 20 watakaoelekea nchini Uganda katika michuano ya vijana inayoandaliwa na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati, Cecafa.

Mchezo huo unaotarajiwa kupigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Soka la Vijana, Ramadhani Abdallah Manyama, alisema katika hatua hii ya awali kuna jumla ya wachezaji 35 ambao wanafanya mazoezi katika Uwanja wa Amaan kila siku saa mbili asubuhi kujiandaa na michuano hiyo.

Alisema lengo la mchezo huo wa kirafiki ni kuangalia uwezo wa wachezaji ulipofikia tangu walipoanza mazoezi Septemba 2, mwaka huu na kufanya mchujo wa kuwapata wachezaji wazuri watakaoiwakilisha Zanzibar kwenye michuano hiyo ya Cecafa.

Aidha, katibu huyo aliwaomba Wazanzibar kujitokeza kwa wingi kuipa hamasa timu yao ya vijana katika kipindi hiki cha kukiandaa kikosi hicho.

# Wimbo uchaguzi wa Serikali za Mitaa waja

**Na Shufaa Lyimo**

MSANII wa muziki nchini, Luiza Mbutu (pichani chini), amesema anatarajia kuachia nyimbo mpya hivi karibuni kwa lengo la kutoa hamasa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kupiga kura katika uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kama Katibu Msaidizi wa Uzalendo Kwanza, aliwataka vijana wazee pamoja na wanawake kujitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wenye weledi.

"Sasa hivi tunajiandaa kutunga wimbo ambao tutautumia kwenye kampeni za kuelekea uchaguzi huo," alisema Luiza.

Alisema anajivunia kitendo cha wasanii mbalimbali kujiunga na kuwa kitu kimoja kuhamasisha Watanzania kujiandikisha kwenye Daftari la Mpigakura.

Naye msanii wa kuigiza, Steve Nyerere, ambaye ni Mwenyekiti wa Wazalendo Kwanza, alisema uandikishaji wa kupiga kura utaanza Oktoba 8-14, mwaka huu na kudai Kinondoni ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa watu kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Mpigakura.



# BOCCO ATAMANI KUANZA KUIJARIBU MTIBWA IJUMAA

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wamezidi kuimarika safu yao ya ushambuliaji baada ya straika John Bocco kurejea kujifua na wenzake huku akieleza kwa sasa hali yake inaendelea vizuri na yupo tayari kupambana.

Bocco aliumia mguu wakati wa mechi ya marudiano ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji iliyopigwa Uwanja wa Taifa mwezi uliopita, na aliukosa mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania ambao Simba ilianza kwa ushindi wa mabao 3-1.

**Akizungumza na Nipashe jana, Bocco alisema yupo tayari kupambana katika mechi dhidi ya Mtibwa Sugar Ijumaa wiki hii, kama kocha atampa nafasi.**

"Kwa sasa nashukuru naendelea vizuri, nikipata nafasi ya kupangwa nitacheza," alisema mshambuliaji huyo.

Alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa kuwa malengo yao ni kushinda katika kila mchezo.

"Lengo langu ni kuipa mafanikio timu yangu na kutetea kombe letu la ubingwa msimu huu,"alisema.

Aliongeza kuwa Ligi Kuu msimu huu imeanza kwa ushindani mkubwa, huku akiwataka mashabiki wao kuendelea kuwapa ushirikiano ili waweze kufanya vizuri na hatimaye kutetea ubingwa wao.

Aidha, alisema licha ya kutolewa mapema katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Mashabiki wasikate tamaa na kuwaahidi watajipanga upya mwakani.

## NINJA HUYO...




Beki wa kikosi cha wachezaji wa akiba cha LA Galaxy, Mtanzania Abdallah Haji Shaibu 'Ninja' akiwa na mshambuliaji wa kikosi cha kwanza cha timu hiyo, Msweden Zlatan Ibrahimovich kwenye gym ya klabu hiyo jana jijini California, Marekani. **PICHA: MTANDAO**

# *KMKM, Jang'ombe kukata utepe Ligi Kuu*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, Mabaharia wa KMKM, Ijumaa watashuka katika Uwanja Amaan majira ya saa kumi alasiri kufungua pazia la ligi hiyo dhidi ya timu ya Jang'ombe Boys.

Pazia la Ligi Kuu Zanzibar linatarajia kufunguliwa rasmi Ijumaa ambapo zitapigwa mechi tatu katika viwanja vya Mau, Amaan na Gombani kisiwani Pemba.

Awali ligi hiyo ilipangwa kuanza Septemba 6, mwaka huu, lakini ilisogezwa mbele kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutoa muda kwa klabu shiriki kupitia pingamizi za usajili.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Rais wa Jang'ombe, Ali Othman maarufu Kibichwa, alisema katika kujiandaa na mchezo huo wamepiga kambi ya wiki moja ili kuhakikisha wanatoka na alama tatu.

Alisema msimu huu watahakikisha timu ya Jang'ombe Boys inafanya vizuri tangu mwanzo mwa ligi hiyo ili kuepuka kufanya vibaya kama msimu uliopita ambao walishindwa kumaliza ligi wakiwa nafasi za juu.

"Tumeweka kambi hapa hapa visiwani Zanzibar na lengo letu ni kuhakikisha wachezaji wanakuwa imara kuelekea mchezo huo wa ufunguzi ambao tunahitaji kushinda," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohamed, aliliambia gazeti hili kuwa klabu zote zinapaswa kufuata ratiba za ligi hiyo kama zilivyopangwa ikiwamo kwa timu ambazo zinapaswa kusafiri kuelekea kisiwani Pemba kufanya hivyo kama ratiba hiyo inavyoonyesha ili kuepuka changamoto ya usafiri.

Ligi Kuu ya Zanzibar ambayo bado haijapata mdhamini, inashirikisha jumla ya timu 16 ambazo ni KMKM, Mafunzo, JKU, KVZ, Polisi, Zimamoto, Chuoni, Malindi, Mlandege, Selem View, Mwenge, Chipukizi, Jamuhuri, Jang'ombe Boys, pamoja na timu mbili zilizopanda msimu huu, Kipanga kutoka Unguja na Machomane ya Pemba.

Michezo
Jumatano Septemba 11, 2019
Nipashe



Guendouzi na ubora wa miaka 10 UKURASA 30

NYAVU...



Beki wa kati wa Ubelgiji, Toby Alderweireld (kulia), akiiandikia timu yake bao la tatu kwa kuunganisha nyavuni kwa kichwa mpira wa kona iliyochongwa na Kevin De Bruyne wakati wakishinda 4-0 katika mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Scotland juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Kagere aanza na tuzo TFF, Ajibu atoa neno

●●● Agosti yawa tamu kwa Mnyarwanda baada ya kufungua msimu kwa mafanikio, huku makocha...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, akianza na tuzo Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20, straika aliyerejea nyumbani hapo mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam, Ibrahim Ajibu, amewataka mashabiki wa timu hiyo kutulia huku akiahidi kufanya vizuri.

**Jana Kamati ya Tuzo ya Ligi Kuu Bara, ilimtangaza Kagere kuwa Mchezaji Bora wa mwezi Agosti hiyo ikitokana na kiwango kikubwa alichokionyesha kwenye mechi yao ya ufunguzi dhidi ya JKT Tanzania.**

Kagere ambaye katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru alihusika katika mabao yote matatu wakati Simba ikishinda 3-1, amepewa tuzo hiyo akiwashinda wachezaji wenzake Lukas Kikoti wa Namungo FC na Seif Karihe wa Lipuli, aliofika nao fainali.

Katika mechi hiyo dhidi ya JKT Tanzania, Kagere alifunga mabao mawili na kutoa pasi ya mwisho kwa bao lililozamishwa nyavuni na Miraji Athumani.

Kwa upande wa Ajibu ambaye katika mechi hiyo aliingia dakika za mwisho akitokea benchi, baada ya kuwa katika wiki ngumu ya mazoezi na timu hiyo, jana aliwataka Wanasimba kuwaamini na kuwa pamoja nao huku akiahidi kufanya vizuri.

"Nawaomba Wanasimba watuamini, sisi tupo pamoja na wao wawe pamoja na sisi. Nawaahidi nitafanya vizuri. Nawapenda sana- @ibrahimajibu23," alitupia katika mtandao wa klabu hiyo.

Kwa muda wa siku tatu mfululizo Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, ameonekana kuna kitua anataka kukitengeneza kutoka kwa Ajibu kutokana na namna anavyopewa mazoezi.

Katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam, kocha wa viungo wa klabu hiyo, Adel Zrane amekuwa akibeba jukumu la kudili na mshambuliaji huyo aliyerejea Simba msimu huu akitokea kwa mahasimu wao, Yanga.

Ajibu, ambaye ana kipaji cha hali ya juu ya kutandaza soka, amekuwa akielezwa ni mvivu wa kufanya mazoezi na inadaiwa kocha haridhishwi na namna anavyojifua katika kuhakikisha analinda kipaji chake.

Kwa mujibu wa chanzo chetu cha uhakika kilichopo karibu na makocha hao, kilieleza si kwamba Ajibu hafanyi mazoezi bali kocha haridhishwi na kiwango chake cha kujifua na anataka kumtengeneza kuwa bora zaidi.

"Aussems amemfuatilia na kugundua hilo, hivyo ametoa jukumu kwa Zrane kudili naye katika mazoezi na uzuri Ajibu ni mwelewa mambo yatakuwa mazuri tu," kilieleza chanzo chetu.

Simba itashuka dimba la Uhuru keshokutwa, Ijumaa kuikaribisha Mtibwa Sugar iliyotoka kupoteza mechi yake ya ufunguzi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mabao 3-1 dhidi ya Lipuli FC.

## Zahera: Dawa Zesco Taifa tu

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kabla ya mchezo wao wa awali wa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco ya Zambia, Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, ameweka wazi kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini ni lazima kazi waimalizie Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana wa kirafiki dhidi ya Toto African ya Mwanza, Zahera alisema wamejipanga 'kumalizia kazi' Uwanja wa Taifa kwa kuwa anaamini mchezo wa marudiano nchini Zambia utakuwa mgumu zaidi.

"Unajua lazima tupambane sana kwenye mchezo wa nyumbani, ushindi mzuri utatupa nafuu kuelekea kwenye mechi ya marudiano na utatupa nafasi ya kujipanga zaidi na kujua nini tunatakiwa kwenda kufanya ugenini," alisema Zahera.

Alisema hana hofu na timu yake na yapo mambo aliyoyafanyia kazi ambayo anaamini yatawasaidia kwenye mchezo huo utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa.

"Kila mchezo una mipango yake, tumemaliza mchezo wa kwanza dhidi ya Township Rollers, hatutacheza kwa namna tulivyocheza... mchezo huu una mipango yake na tunaendelea kuifanyia kazi hatua za mwisho," aliongeza kusema Zahera.

Zahera, amesema kikubwa anataka kuona wachezaji wake wote wanakuwa kwenye afya nzuri mpaka siku ya mchezo ili kumpa wigo mpana kwa kuona wachezaji wa kuwatumia kutokana na mbinu atakazotumia kwenye mechi hiyo.

Katika hatua nyingine, winga wa timu hiyo, Issa Bigirimana anaendelea kupata nafuu kutokana na maumivu ya paja yanayomkabili.

Nyota huyo wa Yanga hakuweza kuungana na wenzake kwenye kambi mkoani Mwanza kutokana na maumivu hayo.

Baada ya mchezo huo wa Jumapili, Yanga itarudiana na wapinzani wao hao wiki mbili baadaye nchini Zambia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042